JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI
WANANCHI KIUCHUMI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI YA MWAKA 2004 KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023

Septemba 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI YA MWAKA 2004 KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023

**Kimeandaliwa Na:**

Ofisi ya Waziri Mkuu
(Sera, Bunge na Uratibu),
Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi,
Viwanja vya Nzunguni, Nanenane, Block Na.2, Kitalu A,
Barabara ya Kondoa,
S.L.P 792,
**DODOMA.**

**Kwa Kushirikiana Na:**

PASS Trust,
PSSF Commercial Complex,
5th Floor,
Sam Nujoma Road, Sinza C – Street,
S.L.P 9094,
**DAR ES SALAAM.**

**Septemba 2023**

## YALIYOMO

ORODHA YA VIFUPISHO ..... v

ORODHA YA MICHORO ..... viii

ORODHA YA MAJEDWALI ..... ix

UJUMBE MAHSUSI ..... 1

DIBAJI ..... 2

MUHTASARI MAHSUSI ..... 4

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 7**

1.1 Usuli ..... 7

1.2 Lengo la Taarifa ya Mwaka ya Uwezeshaji ..... 8

1.3 Mchakato wa Uandaaji wa Taarifa ..... 8

1.4 Muundo wa Taarifa ..... 9

**SURA YA PILI: UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023 ..... 10**

2.1 Utangulizi ..... 10

2.2 Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji ..... 12

2.3 Mfumo na Utawala wa Kodi, Sheria, Kanuni, Leseni na Huduma za Serikali ..... 28

2.4 Mitaji ..... 34

2.5 Kuinua Viwango vya Ujuzi na Uzoefu ..... 47

2.6 Miundombinu ya Kiuchumi ..... 57

2.7 Uwekezaji wa Masoko ya Mitaji na Umiliki wa Hisa ..... 65

2.8 Masoko ..... 71

2.9 Ushirika ..... 78

2.10 Ardhi ........ 82

2.11 Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji ........ 86

2.12 Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ........ 97

2.13 Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi ........ 100

**SURA YA TATU: MASUALA YA KUJIFUNZA NA SIMULIZI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........ 106**

3.1 Mambo ya Msingi ya Kujifunza na Kufanyiwa Kazi ........ 106

3.2 Simulizi na Shuhuda za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Taasisi ya Pass Trust ........ 107

**SURA YA NNE: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 115**

4.1 Hitimisho ........ 115

4.2 Mapendekezo ya Jumla ........ 115

**VIAMBATISHO:** Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji ........ 119

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGITF | Mfuko wa Pembejeo wa Taifa |
| AfDB | Benki ya Maendeleo ya Kilimo |
| ASDP | Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo |
| AMCOS | Chama cha Ushrika cha Msingi cha Mazao na Masoko |
| BBT | Programu ya Kilimo Biashara kwa Vijana |
| BEU | Kitengo cha Kuboresha Mazingira ya Biashara |
| BDS | Huduma za Maendeleo ya Biashara |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BRELA | Wakala wa Usajili Biashara na Leseni |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| CBE | Chuo cha Elimu ya Biashara |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| CFC | Mfuko wa Mazao Duniani |
| CMSA | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana |
| CRB | Bodi ya Usajili wa Makandarasi |
| CPB | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko |
| COSTECH | Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia |
| CSDR | Huduma za Uwekaji Dhamana na Usajili |
| DIT | Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam |
| DSE | Soko la Hisa Dar es salaam |
| EAC | Jumuiya ya Africa Mashariki |
| EACOP | Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki |
| e-GA | Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| EDI | Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali |
| ESG | Maendeleo ya Jamii na Utawala Bora |
| EPZA | Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji na Mauzo Nje ya Nchi |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| GAMIS | Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali |
| GePG | Mfumo wa Malipo ya Kieletroniki wa Serikali |
| GFS | Takwimu za Fedha za Serikali |
| GCLA | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali |
| GDP | Pato la Taifa |
| GPSA | Wakala wa Huduma ya Manunuzi ya Serikali |
| IFM | Chuo cha Usimamizi wa Fedha |

| | |
|---|---|
| IOSCO | Shirika la Kimataifa la Tume za Dhamana |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| KEEC | Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kahama |
| LATRA | Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini |
| MAJIIS | Mfumo wa Kusimamia Ankara na Rasimali za Maji |
| MKUMBI | Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji |
| MUVU | Mfumo wa kielektroniki wa Kusimamia Vyama vya Ushirika |
| NBC | Benki ya Taifa ya Biashara |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| NCB | Benki ya Taifa ya Ushirika |
| NEDC | Kamati ya Taifa ya kuendeleza Wajasiriamali |
| NEDF | Mfuko wa Taifa wa kuendeleza Wajasiriamali wananchi |
| NEEC | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi |
| NEMC | Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira |
| NFRA | Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula |
| NIDA | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| OR TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OSHA | Mamlaka ya Usimsmizi wa Usalama na Afya Kazini |
| OWM | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| PASS | Dhamana ya Kusaidia Sekta ya Kilimo Binafsi |
| PPRA | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| PSC | Kamati ya Uongozi ya Programu |
| REF | Mfuko wa Nishati vijijini |
| RITA | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini |
| SACCOS | Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika |
| SDL | Kodi ya Uendeshaji Ujuzi |
| SGR | Mradi wa Reli ya Kisasa |
| SIDO | Shiriki la Kuhudumia Viwanda Vidogo |
| SMEs | Biashara ndogo ndogo na Kati |
| SUA | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine |
| TAA | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania |
| TAESA | Mfumo wa Huduma za Ajira |
| TASAC | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania |

| | |
|---|---|
| TANECU | Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala |
| TANROAD | Wakala wa Barabara Nchini Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini Tanzania |
| TECC | Kituo cha Ushindani wa Ujasiriamali Tanzania |
| TEF | Mfuko wa Elimu Tanzania |
| TEDAP | Maendeleo na Upanuzi wa Nishati Tanzania |
| TCAA | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania |
| TCCIA | Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo |
| TCDC | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania |
| TCRA | Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania |
| TDL | Kodi ya Maendeleo ya Utalii |
| TDV | Dira ya Maendeleo ya Taifa |
| TIB | Benki ya Uwekezaji Tanzania |
| TIC | Kituo cha Uwekezaji Tanzania |
| TIRA | Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania |
| TIRDO | Shirika la Maendeleo ya Uwekezaji na Utafiti Tanzania |
| TPDC | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania |
| TPRI | Taasisi ya Udhibiti wa Viatilifu katika Ukanda wa Kitropiki |
| TPSF | Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TRC | Shirika la Reli Tanzania |
| TSB | Bodi ya Sukari Tanzania |
| TIW | Mfumo wa kusajili Uwekezaji Tanzania |
| TTCL | Shirika la Mawasiliano Tanzania |
| TBS | Shirika la Viwango Tanzania |
| TMDA | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania |
| TNBC | Baraza la Taifa la Biashara |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TWCC | Chama cha Biashara cha Wanawake Tanzania |
| UDSM | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| UNDP | Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa |
| UTT AMIS | Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali |
| VETA | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| WDF | Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake |
| WHI | Taasisi ya Nyumba kwa Watumishi |
| YDF | Mfuko wa Maendeleo ya Vijana |

## ORODHA YA MICHORO


**Mchoro Na.1:** Nguzo za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ..................... 10
**Mchoro Na.2:** Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa .......... 12
**Mchoro Na.3:** Mwenendo wa Ukuaji kwa baadhi ya Sekta (%) ....................... 13
**Mchoro Na.4:** Taasisi Zilizounganishwa na Huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao........................................................................ 32
**Mchoro Na.5:** Umiliki katika Benki .................................................................. 36
**Mchoro Na.6:** Usajili na Ushiriki wa Makandarasi katika Miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi ....................................................... 58
**Mchoro Na. 7:** Mwenendo wa Ajira Katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji........................................................................ 86

# ORODHA YA MAJEDWALI


**Jedwali Na. 1:** Mchanganuo wa Uchambuzi wa Taarifa za Wadau .................... 9
**Jedwali Na. 2:** Hali ya Utekelezaji wa Mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi...............................................................11
**Jedwali Na. 3:** Viwango vya Mfumuko wa Bei Nchi za SADCna EAC kwa mwaka 2021 – 2022.................................................................. 15
**Jedwali Na. 4**: Hali ya Mfumko wa Bei .......................................................... 17
**Jedwali Na. 5:** Uwekezaji kwa sekta na Aina ya Umiliki................................. 18
**Jedwali Na. 6:** Takwimu za Viwanda Vidogo, Kati na Vikubwa...................... 19
**Jedwali Na. 7:** Ajira Viwandani kwa Mwaka 2022/23 ................................... 20
**Jedwali Na. 8:** Miradi iliyosajiliwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ............... 21
**Jedwali Na. 9:** Umiliki wa Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa ........................ 22
**Jedwali Na.10:** Usajili na Ajira za Miradi ya Uwekezaji katika Mikoa ............ 22
**Jedwali Na. 11:** Changamoto na Mikakati katika Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji ......................................................... 27
**Jedwali Na. 12:** Marekebisho ya Sheria mbalimbali kuhusu Kodi..................... 29
**Jedwali Na. 13:** Mwenendo wa Usajili na Utoaji Leseni .................................. 31
**Jedwali Na. 14:** Mchanganuo wa Aina ya Huduma Zilizotolewa ...................... 32
**Jedwali Na. 15:** Changamoto na Mikakati ya Kuboresha Mfumo na Utawala wa Kodi, na Huduma za Serikali ............................................. 34
**Jedwali Na. 16:** Idadi ya Taasisi za Fedha Zilizosajiliwa na Kupewa Leseni .... 36
**Jedwali Na.17:** Mikopo Iliyotolewa na Benki na Hali ya Marejesho................ 37
**Jedwali Na. 18:** Viwango vya Riba za Benki na Riba za Mikopo...................... 38
**Jedwali Na.19:** Hali ya Matumizi ya Huduma za Fedha .................................. 38
**Jedwali Na.20:** Idadi ya Taasisi na Wakopoaji Waliosajiliwa katika Kazidata ya Wakopaji ......................................................................... 39
**Jedwali Na. 21:** Ajira za Watanzania na Wageni katika Benki........................... 39
**Jedwali Na.22:** Idadi ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji .......................... 40
**Jedwali Na. 23:** Mikopo na Ruzuku Iliyotolewa kutoka Mifuko na Programu za Uwezeshaji Kisekta............................................................. 41
**Jedwali Na. 24:** Mikopo kutoka katika Mifuko ya Uwezeshaji Kimkoa............ 41
**Jedwali Na. 25:** Mikoa Iliyonufaika na Mikopo ya SANVN Viwanda Scheme 43
**Jedwali Na. 26:** Mgawanyo wa Idadi ya Watoahuduma za Bima Waliosajiliwa 44
**Jedwali Na. 27:** Idadi ya Vituo Vilivyosajiliwa na Mfuko ................................ 45
**Jedwali Na. 28:** Hali ya Uzalishaji wa Vitambulisho ........................................ 45
**Jedwali Na. 29:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Upatikanaji wa Mitaji ... 47
**Jedwali Na. 30:** Uanzishaji wa Taasisi za Elimu ............................................... 48
**Jedwali Na. 31:** Idadi ya Shule, Wanafunzi na Walimu katika Shule za Msingi 49
**Jedwali Na. 32:** Idadi ya Bunifu Zilizosajiliwa ................................................. 51
**Jedwali Na. 33:** Idadi ya Wajasiriamali Waliojengewa Uwezo .......................... 51
**Jedwali Na. 34:** Aina ya Biashara zinazofanywa na Shule zinazonufaika na Programu ya Probono .............................................................. 55
**Jedwali Na. 35:** Changamoto na Mikakati ya Kuinua Ujuzi na Uzoefu............. 57

**Jedwali Na. 36:** Ushiriki wa Makandarasi Katika Miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi ........ 59
**Jedwali Na. 37:** Mwenendo wa Miradi ya Ubia ........ 60
**Jedwali Na. 38:** Changamoto na Mikakati ya Kuboresha Miundombinu ya Kiuchumi ........ 64
**Jedwali Na. 39:** Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja na Idadi ya Wawekezaji ........ 67
**Jedwali Na. 40:** Mchango wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ........ 68
**Jedwali Na. 41:** Uchangiaji wa Mapato kutoka UTT AMIS ........ 69
**Jedwali Na. 42:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Uwekezaji katika Masoko ya Mitaji na Ununuzi wa Hisa ........ 70
**Jedwali Na. 43:** Mwenendo wa Mauzo ya Mazao ya Nafaka Nje ya Nchi 2022/23 ........ 71
**Jedwali Na. 44:** Ununuzi wa Bidhaa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania........ 72
**Jedwali Na. 45:** Mauzo ya Madini kwa mwaka 2022/23 ........ 73
**Jedwali Na. 46:** Masoko Tengefu ........ 74
**Jedwali Na. 47:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Masoko ........ 77
**Jedwali Na. 48:** Idadi ya Wanufaishwa wa Elimu na Mafunzo ya Ushirika ...... 79
**Jedwali Na. 49:** Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Vyama vya Ushirika 81
**Jedwali Na. 50:** Hali ya Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria 82
**Jedwali Na. 51:** Hali ya Upimaji wa Maeneo ........ 83
**Jedwali Na. 52:** Umiliki wa Maeneo ........ 84
**Jedwali Na. 53:** Changamoto na Mikakati katika Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi ........ 85
**Jedwali Na. 54:** Manunuzi katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji........ 87
**Jedwali Na. 55:** Hali ya Urithishaji wa Ujuzi na Uhaulishaji wa Teknolojia kwa Watanzania ........ 89
**Jedwali Na. 56:** Idadi ya Watanzania Walionufaika na Uhaulishaji wa Teknolojia ........ 91
**Jedwali Na. 57:** Hali ya Huduma kwa Jamii kupitia Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji ........ 92
**Jedwali Na. 58:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Ushiriki wa Watanzania 96
**Jedwali Na. 59:** Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Vituo vya Uwezeshaji Kiuchumi........ 100
**Jedwali Na. 60:** Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Yaliyoanzishwa........ 102
**Jedwali Na. 61:** Idadi ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake yaliyoanzishwa kwa Kila Mkoa ........ 102
**Jedwali Na. 62:** Changamoto na Mikakati ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi........ 105

## UJUMBE MAHSUSI



Bodi imeendelea kusimamia majukumu ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi(NEEC) kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004. Katika mwaka 2022/23, Bodi iliendelea kuhakikisha kuwa, Baraza linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004, ikiwa ni pamoja na: Kukuza na kusaidia shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na Watanzania; Kuwapa Watanzania fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za Kiuchumi; na Kuhimiza Watanzania kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za kiuchumi.

Pamoja na kutoa ushauri na maelekezo kwa Baraza lenye mlengo wa kukuza uwezeshaji ili kuwezesha wananchi kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi, Bodi inahakikisha kuwa, Baraza linatekeleza mikakati ambayo itachochea uanzishaji na uendelezaji wa shughuli za kiuchumi kwa lengo la kupunguza mzunguko wa umaskini katika jamii na kuwa na Taifa lenye uchumi endelevu. Hivyo, wanufaika wakuu wa huduma za uwezeshaji ni wananchi wa Tanzania wakiwemo wakulima, wavuvi, wafugaji, wenye viwanda, wafanyabiashara, wanamichezo, wasanii, wabunifu, machinga, na watumishi katika sekta ya umma na sekta binafsi.

Kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi ya Baraza, naipongeza Menejimenti na watumishi wote wa Baraza kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma katika kuhakikisha kuwa Baraza linatekeleza vyema majukumu yake ya kukuza uwezeshaji. Aidha, natoa shukrani za dhadi kwa Wizara, Mikoa, Halmashauri, taasisi za sekta ya umma na sekta binafsi kwa kutoa huduma za uwezeshaji katika sekta mbalimbali na wananchi kwa ushirikiano wao katika kusaidia Baraza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Niwaombe muendelee kutekeleze wajibu wenu ipasavyo katika kuhakikisha kuwa huduma bora za uwezeshaji zinaimarishwa na kuwafikia wananchi wa Tanzania hasa maeneo ya pembezoni na vijijini.

Bodi ya Baraza, chini ya Uenyekiti wangu itaendelea kutoa maelekezo na ushauri kwa Menejimenti ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi ili kuwahakikishia wananchi wa Tanzania wananufaika na utoaji huduma za uwezeshaji wenye ufanisi na tija unaochochea ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi.

Prof. Aurelia K. N. Kamuzora
**Mwenyekiti wa Bodi - NEEC**

# DIBAJI



Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC) limeanzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi Na. 16 ya mwaka 2004 kupitia Kifungu 4 (1) kama Chombo cha juu Kitaifa chenye jukumu la kuratibu, kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004. Sera hiyo inalenga kuwawezesha wananchi wa Tanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga na kumiliki uchumi wa nchi yao. Katika mwaka 2022/23, Baraza kwa kushirikiana na Wizara, Mikoa, Halmashauri na taasisi za sekta za umma na sekta binafsi limetekeleza kwa mafanikio makubwa jukumu la kuratibu, kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004.

Taarifa ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka fedha 2022/23 inabainisha jitihada na mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa nguzo za Sera ambazo ni: kukuza uchumi na kujenga mazingira ya uwekezaji; mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni na huduma za Serikali; mitaji; kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu; miundombinu ya kiuchumi; uwekezaji wa mitaji na dhamana; masoko; ushirika; na ardhi.

Jitihada zilizotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wa maendeleo zimechochea ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Jitihada hizo, zinaakisi dhamira ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukuza uwezeshaji nchini.

Natambua shauku walionayo wananchi wa Tanzania ya kutaka kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kilimo, uvuvi, ufugaji, viwanda, sanaa, michezo, biashara, elimu, afya na utamaduni. Kutokana na sababu hiyo, sisi kama Baraza lenye dhamana ya kukuza uwezeshaji nchini, tutaendelea kuboresha mazingira wezeshi kwa ajili ya kuhahakisha kuwa maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu yanafikiwa katika kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Baraza limejielekeza katika kukuza uwezeshaji kwa kusimamia, na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa mwaka 2022/23 yametokana na jitihada za wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wizara, Mikoa, Halmashauri na taasisi za sekta ya umma na sekta binafsi. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa kila mmoja kwa jitihada anazotekeleza katika

kukuza uwezeshaji nchini. Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza watumishi wote wa Baraza na niwaombe wazidi kuwa na ari na kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Kipekee pia, shukrani za dhati ziende kwa Mwenyekiti na wajumbe wa Baraza kwa maelekezo na ushauri wao unaowezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza kwa ufanisi na tija.

CPA., Beng'i M. Issa
**Katibu Mtendaji - NEEC**

# MUHTASARI MAHSUSI

Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Na.16 ya mwaka 2004 kwa lengo la kuhakikisha sehemu kubwa ya uchumi wa nchi inamilikiwa na watanzania wenyewe. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi inatoamwongozo wa jumla unakaotumika kutafsiri uwezeshaji unavyokuwa katika sehemumbalimbali kulingana na mazingira ya sekta husika. Mikakati inayobuniwa nasekta mbalimbali, inafafanua uwezeshaji katika shughuli za kiuchumi kwa sekta husika. Kutokana na nguzo za Sera, ni wajibu wa kila sekta kufafanua na kuchanganua jinsi ya kutekeleza Sera hii kulingana na majukumu yake. Aidha, Serikali imekuwa na utaribu wa kila mwaka kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuandaa taarifa ya tathmini ya hali halisi ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi. Mbinu mbalimbali zimekuwa zikifanyika kuhakikisha wadau wa kisekta wanawasilisha taarifa ambazo zinafanyiwa kazi kwa kuchakatwa, kuchambuliwa kwa kina ili kukamilisha taarifa ya Mwaka ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo huzinduliwa katika Kilele cha Kongamano la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Matokeo ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa kipindi cha mwaka 2021/22 yanaonesha umiliki wa watanzania katika benki ulikuwa **asilimia 40.6** ikilinganishwa na **asilimia 59.4** inayomilikiwa na wageni kwa mwaka 2022/23 huku pia idadi ya taasisi za fedha ikifikia **44,441** kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na **31,319** kwa mwaka 2021/22 na idadi ya benki zikifikia **44.** Ajira katika benki na taasisi z afedha zikiwa ni **17,528** ambapo za watanzania zikiwa ni **17,477** na wageni **51** kwa mwaka 2021/22 na ajira **18,071** ambapo kati ya hizo ajira za watanzania zilikuwa **18,023** na wageni **48** kwa mwaka 2022/23. Hivyo, uwekezaji katika benki umekuwa na mchango chanya kwa maendeleo ya nchi. Aidha, kanzidata ya taarifa za wakopaji (Credit Reference Bureau) imewezesha usajili wa wakopaji **5,035,031** waliopata huduma katika taasisi **166** zilizojisajili kwa mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na idadi ya wakopaji **4,215,210** waliosajiliwa kwa mwaka 2021/2022.

Mifuko na programu za uwezeshaji iilifanikiwa kutoa jumla ya shilingi **bilioni 743.7** kwa wanufaika wapatao **6,064,957** wakiwemo wanaume ni **2,776,771** na wanawake **3,288,186.** Kati ya fedha hizo zilizotolewa, mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja na ile inayotoa dhamana imekopesha shilingi **bilioni 430.5** kwa wanufaika **932,442** ambapo wanaume ni **498,912** na wanawake ni 433,530. Kiasi cha shilingi **billioni 313.2** kilitolewa na mifuko inayotoa ruzuku kwa wanufaika wapatao **5,132,515** ambapo wanaume ni 2,277,859 sawa na **asilimia 44** na wanawake ni **2,854,656** sawa na **asilimia 56**. Fedha hizo zilizotolewa zimewezesha kuzalisha ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zipatazo **7,764,975** ambapo ajira za wanawake zilikuwa **4,208,616** sawa na **asilimia 54** na wanaume zilikuwa **3,556,359** sawa na **asilimia 46**. Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Vya Kati (SANVN Viwanda Scheme) ulifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 3.83** kwa miradi midogo na ya kati **65** katika mikoa **13** ambayo ni Mwanza **(11),** Arusha

**(22),** Dar Es Salaam **(7),** Kilimanjaro **(3),** Mbeya **(6),** Geita (3), Songwe **(1),** Dodoma **(2),** Shinyanga **(1),** Iringa **(4),** Njombe **(2),** Singida **(1),** Pwani **(1)** na Rukwa **(1).** Katika kipindi cha 2022/23, jumla ya ajira **9,983** zimetengenezwa ambapo ajira za moja kwa moja ni **1,995** za ajira zisizo za moja kwa moja ni **7,988.** Mpango umefanikisha viwanda vidogo na vya kati **62** pamoja na wafanyakazi kujiandikisha katika mfuko wa Hifadhi za Jamii (NSSF).

Tathmini pia inaonesha wafanyabiashara **5,268,655** ndiyo wenye TIN ambapo kati yao **1,893,810** ni wafanyabiashara na **3,374,845** ni wale ambao hawafanyi biashara. Mifumo ya kodi iliendelea kuboreshwa ambapo wafanyabiashara wamekua wakitumia katika kujaza ritani na kulipa kodi kwa wakati na hivyo kuwezesha jumla ya wafanyabiashara waliosajiliwa VAT kufikia **32,616** kwa mwaka 2022/2023.

Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 uliongezeka kwa **asilimia 4.21** na kufikia shilingi **trilioni 10.83** ikilinganishwa na shilingi **trilioni 10.39** katika kipindi kilichoishia Juni, 2022. Katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 2.4 na kufikia shilingi trilioni 3.30, ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.22 zilizorekodiwa mwaka 2021/22. Mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 yaliongezeka kwa **asilimia 19.6** na kufikia shilingi **milioni 981.93**, ikilinganishwa na shilingi **milioni 821.04** zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni, 2022. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine. Aidha, mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 ulikuwa mzuri. Thamani ya uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa **asilimia 56.79** na kufikia shilingi **trilioni 1.52** katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 kutoka shilingi **bilioni 971.68** mwaka 2021/22.

Tathmini ya utekelezaji ilibaini kuwa**,** jumla ya tozo, ada na faini 39 zimefutwa au kupunguzwa ambazo zimekuwa ni kero katika ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Baadhi ya tozo hizo ni zile zilizokuwa zikitozwa na: Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Bodi ya Sukari Tanzania (TSB), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FFR). Aidha, kupitia mapendekezo ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, jumla ya tozo 61 zimependekezwa kufutwa au kupunguzwa. Tozo hizo ni zile zilizokuwa zikitozwa katika sekta za Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Ujenzi na Uchukuzi; Maliasili na Utalii; Kilimo; Mifugo na Uvuvi. Aidha, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA); na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) zimefanya marekebisho ya kupunguza baadhi ya tozo zake.

Tathmini inaonesha vituo vya uwezeshaji kwa mwaka 2022/23 vimefikia **19** sawa na asilimia **10.3** ya lengo la kuwa na vituo hivyo ikilinganishwa na idadi ya halmashauri

**184.** Tathmini inaonesha mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 6.3** ilitolewa kwa wajasiriamali **964** na taasisi ndogo za kifedha **25** ambazo zilipatiwa mkopo wa **shilingi bilioni 0.57**.

Katika kukuza vyama vya ushirika, tathmini inaonesha kuwa, Mtaji wa Benki ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika umeongezeka kutoka Shilingi **bilioni 1.8** na kufikia shilingi **bilioni 5.7** sawa na **asilimia 31.6.** Jitihada zinaendelea kufanyika ili kufikia mtaji wa shilingi **bilioni 15** unaotakiwa kisheria kukamailisha usajili wa Benki ya Taifa ya Ushirika. Serikali kupitia mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ulifanikiwa kusajili vyama vya ushirika **4,661** ambapo pia utaongeza upatikanaji wa taarifa za uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia ushirika na hivyo kuhamasisha ukuaji wa vyama vyenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2022/23, kuna changamoto zinzathiri ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Changamoto hizo ni pamoja na: ukosefu wa miundombinu wezeshi na rafiki katika maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji. Miundombinu hiyo ni barabara, maji, umeme wa uhakika, reli na bandari hivyo kupelekea uwekezaji mwingi wa miradi kujazana katika mikoa yenye miundombinu imara kama Dar es Salaam, Pwani, Arusha, na Mwanza; bidhaa zinazozalishwa ndani kushindwa kuhimili ushindani katika soko kutokana na ukosefu wa ubora; ukosefu wa umeme wa uhakika na kuathiri shughuli za uzalishaji na biashara kwa ujumla; uelewa mdogo juu ya fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji na ununuzi wa hisa pamoja na Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja; kiwango kidogo cha walipakodi ikilinganishwa na nguvukazi iliyopo nchini; uwepo wa idadi kubwa ya biashara ndogo zinazofanywa na wananchi katika mifumo isiyo rasmi; uwepo wa mikopo chechefu; kutokuwepo kwa Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi; kampuni za ndani bado zinakabiliwa na changamoto za ukosefu wa mitaji ikiwemo mitambo katika kutekeleza miradi; kuwepo kwa mlolongo mrefu wa uhaulishaji wa ardhi; na *kutokuwepo kwa Sera na Sheria ya Taifa ya Local Content kama miongozo ya jumla kwa sekta zote ili kuwezesha ushiriki wa watanzania wenye tija kwa kampuniza ndani pamoja na ukuaji wa sekta binafsi.*

Kutokana na changamoto zilizopo, tathmini pamoja na mambo mengine inapendekeza masuala ya msingi ya kufanyiwa kazi katika jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na: Kuimarisha Upatikanji wa Ardhi Iliyopimwa, Kuboresha Miundombinu ya Kiuchumi, Kuandaa Sera na Sheria ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania , Uanzishaji wa Taasisi na Mifuko ya Uwezeshaji (*Wakala wa Dhamana ya Mikopo (Tanzania Credit Guarantee Agency)na* Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi), Mapitio ya Mfumo wa Elimu Unaozingatia Elimu na Ujuzi na kuanzisha *Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI),* Uanzishwaji wa Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, na kuimarisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**.**

# SURA YA KWANZA:

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Samia, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania imeendelea kutekeleza, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 katika kipindi cha mwaka 2022/23 kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC). Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ni sehemu ya mikakati na vipaumbele vya Serikali vya kuhakikisha sehemu kubwa ya uchumi wa Tanzania unamilikiwa na watanzania wenyewe katika jitihada za kufikia shabaha ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV) ifikapo mwaka 2025. Maendeleo hayo yanajumuisha Watanzania wote pamoja na kutoa nafasi kwa makundi yote kujiendeleza kikamilifu hasa yale makundi yenye uwezo mdogo. Pamoja na kuwapa nafasi zaidi wanyonge, yamewekwa mazingira bora ya ujenzi wa uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani katika soko la dunia katika mazingira ya utandawazi. Mwelekeo wa Sera ya uwezeshaji unazingatia uendelezaji na kuipa nafasi kubwa zaidi sekta binafsi pamoja na kuzingatia masharti ya kuendesha uchumi katika mazingira ya nguvu ya soko. Mbinu na mikakati inayotumika katika kuwawezesha wananchi kiuchumi inatambua pia mchango wa sekta isiyo rasmi na kuchukua hatua za kuiboresha. Hivyo, utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji unalenga maeneo yenye kuleta matokeo ya haraka hasa yale yanayogusa maisha ya wananchi katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu, ujenzi, biashara, afya, michezo, sanaa, utalii, madini, nishati, viwanda, na usafirishaji. Sera pia imeainisha mikakati ya makusudi kuwawezesha wananchi walioko tayari katika sekta hizo kufanya vizuri zaidi katika maeneo yao ambayo yanafaa kuachiwa watanzania peke yao na yale yatakayofanywa kwa ubia na wageni.

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi pia inatoa mwongozo wa jumla unaohakikisha kwamba, wananchi wanapata fursa za kiuchumi katika sekta mbalimbali. Kwa maana hiyo, Sera za kisekta zitalenga katika kuwainua wananchi kwa kuwapendelea zaidi ikibidi na kuwawezesha kuwa na kauli na ushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na mambo mengine inajielekeza katika *kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi; kuboresha mfumo na utawala wa kodi, kurekebisha sheria, kanuni na taratibu ili ziendane na dhana ya uchumi unaoendeshwa kwa nguvu za soko; kuboresha na kurahisisha utoaji wa leseni kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi, kuboresha ufanisi wa huduma zitolewazo na Serikali; kurahisisha upatikanaji wa mitaji na kuwezesha wananchi kukopesheka; kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu; kuimarisha miundombinu na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za miundombinu; kuboresha mazingira yatakayowezesha wananchi kushiriki kikamilifu zaidi katika uwekezaji, masoko ya mitaji na umiliki wa hisa; kuimarisha uwezo wa kuzalisha bidhaa bora, kutoa huduma za kutafuta masoko na kutumia manunuzi ya Serikali kuwasaidia wananchi kupata masoko; kuhimiza na kuimarisha maendeleo*

*ya ushirika; kutumia ardhi kama chombo cha kuweka chachu ya uwezeshaji; na kuweka mfumo thabiti wa usimamizi wa sera ya uwezeshaji.*

Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeweka utaratibu wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kila mwaka ili kuandaa taarifa ya mwaka ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo huzinduliwa katika Kongamano la Mwaka la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Taarifa ya mwaka ya uwezeshaji ni muhimu katika kupima na kutathmini jitihada za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilizofanywa na wizara, mikoa, halmashauri na taasisi za sekta ya umma na sekta binafsi. Taarifa hii imeainisha namna utekelezaji wa mikakati na shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilivyofanyika na hivyo kutoa taswira ya kubaini mafanikio, changamoto na mapendekezo ya kufanyiwa kazi na kufuatiliwa ipasavyo. Sanjari na hayo, Kongamano la Saba la mwaka la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2023 (7$^{th}$ Annual Economic Empowerment Forum 2023) limebebwa na kaulimbiu isemayo ***"Uwezeshaji kwa Uchumi Endelevu"*** ambayo inaakisi chachu ya kuendelea kuweka na kuboresha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika kufanikisha vipaumbele vya mipango na mikakati ya Serikali kwa maendeleo ya wananchi wake.

**1.2 Lengo la Taarifa ya Mwaka ya Uwezeshaji**

Lengo kuu la taarifa hii ni kupima na kutathmini jitihada za uwezeshaji kiuchumi zilizofanyika kwenye sekta mbalimbali katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Malengo mahsusi pamoja na mambo mengine yalikuwa ni kupima hali halisi ya utekelezaji wa mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004 kupitia nguzo za uwezeshaji ambazo ni:- kukuza uchumi na kujenga mazingira ya uwekezaji; mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni na huduma za serikali; mitaji; kuinua viwangio vya ujuzi na uzoefu; miundombuinu ya kiuchumi; uwekezaji wa mitaji na ununuzi wa hisa; masoko; ushirika na ardhi. Taarifa hii pia inalenga kupima hali halisi ya ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji (local content), kutoa hali halisi ya uanzishaji na utekelezaji wa vituo vya uwezeshaji katika mikoa na halmashauri, kupima hali halisi ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kwenye mikoa kupitia majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, na kutathmini mwelekeo wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi.

**1.3 Mchakato wa Uandaaji wa Taarifa**

Taarifa hii imeandaliwa chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Baraza la Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na Wizara, Mikoa, Halmashauri, Taasisi za sekta za umma na binafsi, asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali, vikundi vya kifedha vya kijamii, mifuko na program za uwezeshaji, taasisi za utafiti na elimu na wadau wengine. Uandaji wa taarifa hii ulitumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi wa taarifa kutoka kwenye Wizara, Mikoa, Halmashauri, Taasisi za Umma na Binafsi pamoja na kufanya vikao vya majadiliano na wataalam mbalimbali kuhusu taarifa zilizowasilishwa. Sampuli ya tathmini ilitegemewa kuwa na wadau 231 walibainishwa ili kupata taarifa

kutoka katika vyanzo mbalimbali ambazo zilitumika katika uandaaji wa taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa mwaka 2022/23. Wadau 149 waliwasilisha taarifa ambazo zimechangia ukamilishaji wa uandishi wa taarifa ya mwaka ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mwaka 2022/2023. Makundi ambayo yalilengwa kuwasilishwa taarifa yameainishwa kama **Jedwali Na.1**.

**Jedwali Na. 1:** Mchanganuo wa Uchambuzi wa Taarifa za Wadau

| Kundi la Wadau | Idadi ya *respondents* | Urejeshaji wa taarifa | Taarifa ambazo hazikuwasilishwa | % ya urejeshaji |
|---|---|---|---|---|
| Wizara | 16 | 11 | 5 | 68.8 |
| Taasisi za Serikali | 51 | 42 | 9 | 82.4 |
| Mikoa | 26 | 17 | 9 | 65.4 |
| Mifuko na Programu za Uwezeshaji | 71 | 23 | 48 | 32.4 |
| Taasisi za Elimu na Vyuo Vikuu | 12 | 5 | 7 | 41.7 |
| Taasisi za sekta binafsi, NGOs/ Asasi za Kiraia | 10 | 6 | 4 | 60.0 |
| Vituo vya Uwezeshaji | 19 | 19 | - | 100 |
| Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi | 26 | 26 | - | 100 |
| **Jumla** | **231** | **149** | **82** | |

***Chanzo:*** *Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, 2023*

### 1.4 Muundo wa Taarifa

Muundo wa taarifa ya mwaka ya uwezeshaji wananchi kiuchumi una sura tano (5). **Sura ya kwanza** ni **utangulizi** inayotoa maelezo kuhusu usuli na malengo ya taarifa. Sura hii pia imeainisha umuhimu, muundo na mchakato wa kuandaa taarifa. **Sura ya pili** imeeleza kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa nguzo na mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji (Local Content), Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Sura hii pia imeainisha mafanikio, changamoto na kuainisha mapendekezo ya kufanyiwa kazi katika kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi. **Sura ya tatu** imeeleza kuhusu mambo ya msingi ya kujifunza (best practices and lessons learned). **Sura ya nne** inatoa hitimisho **na mapendekezo**.


## SURA YA PILI:

## UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI JUNI, 2023

### 2.1 UTANGULIZI

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kila mwaka ili kupima matokeo ya utekelezaji wa mikakati na shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinaotekelezwa na wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi. Ufuatiliaji na tathmini ya Sera umekuwa ukifanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kufahamu hali ya utekelezaji wa mikakati 83 ya nguzo tisa (9) za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama inavyooneshwa katika **Mchoro Na. 1**.

**Mchoro Na.1:** Nguzo za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi




***Chanzo:*** *Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, 2023*

Katika tathmini hii, **Jedwali Na.2** linaonesha utekelezaji wa mikakati 83 ya nguzo 9 za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Tathmini imebaini kuwa, jumla ya mikakati 69 kati ya 83 sawa na asilimia 83.1 ilitekelezwa kikamilifu, mikakati 12 ilitekelezwa kwa wastani sawa na asilimia 14.5, na mikakati miwili sawa na asilimia 2.4 haikutekelezwa ipasavyo ambayo ni pamoja na kuanzisha taasisi ya kusimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi. Taasisi hii ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneurship Development Institute - EDI) na Wakala wa Dhamana ya Mikopo

(Tanzania Credit Guarantee Agency - TCGA) bado hazijaanzishwa. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, EDI itakuwa na jukumu la kuandaa mitaala ambayo vyuo mbalimbali nchini vitatumia katika kukuza ujuzi kwa wananchi, huku TCGA itakuwa na kazi ya kutathmini miradi ya wananchi na pale inaporidhika, kutoa dhamana ili wananchi waweze kukopeshwa na mabenki ya ndani na ya kimataifa, au kutoa mitaji kwa wananchi watakaoanzisha makampuni ya ubia na wawekezaji wa nje. Tathmini pia imeainisha jitihada zilizofanyika katika kipindi cha mwaka 2022/23 katika kukuza ushiriki wa watanzania (*local content)*, vituo vya uwezeshaji wananchi kichumi pamoja na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi.

**Jedwali Na. 2:** Hali ya Utekelezaji wa Mikakati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi


| Nguzo za Uwezeshaji | Idadi ya Mikakati | Utekelezaji wa Mikakati | | | (%) ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kikamilifu | Wastani | Haikutekelezwa Ipasavyo | |
| 1. Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji | 9 | 8 | 1 | - | **88.9** |
| 2. Mfumo na Utawala wa Kodi, Sheria, Kanuni, Leseni na Huduma Nyingine za Serikali | 15 | 13 | 2 | - | **86.7** |
| 3. Mitaji | 17 | 14 | 3 | 1 | **82.4** |
| 4. Kuinua Viwango vya Ujuzi na Uzoefu | 5 | 4 | - | 1 | **80.0** |
| 5. Miundombinu ya Kiuchumi | 13 | 11 | 2 | - | **84.6** |
| 6. Uwekezaji wa Masoko ya Mitaji na Umiliki wa Hisa | 3 | 2 | 1 | - | **66.7** |
| 7. Masoko | 7 | 6 | 1 | - | **85.7** |
| 8. Ushirika | 10 | 8 | 2 | - | **80.0** |
| 9. Ardhi | 4 | 3 | 1 | - | **75.0** |
| **Jumla** | **83** | **69** | **12** | **2** | |

***Chanzo:*** *Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, 2023*

## 2.2 KUKUZA UCHUMI NA KUJENGA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI

Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi nchini zinazoendana na ukuaji wa uchumi unaojumuisha na kunufaisha watanzania walio wengi, kuongeza vipato vyao pamoja na kuinua hali zao za maisha. Sera inaweka mazingira wezeshi yanayochochea uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa zenye kukidhi ubora kwa ajili ya masoko ya ndani, ya kanda na ya kimataifa. **Mchoro Na.2**. unaonesha mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la ukuaji wa sekta za kiuchumi kwa mwaka 2022.

**Mchoro Na.2:** Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023*

Katika utekelezaji wa nguzo hii, mikakati mbalimbali imetekelezwa katika kipindi cha mwaka 2022/23 ili kukuza uchumi madhubuti na kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, kama ilivyobainishwa katika kipengele cha 2.1.2 hadi 2.1.9.


### 2.2.1 Sera za Kisekta za Kuwawezesha Wananchi Kushiriki kikamilifu Katika Uchumi

#### (a) Ukuaji wa Uchumi

Hali ya uchumi inaonesha thamani halisi ya Pato la Taifa ilifikia shilingi milioni **141.87** ikilinganishwa na shilingi milioni **135.48** mwaka 2021, sawa na ukuaji wa **asilimia 4.7** (NBS, 2023). Kiwango hicho cha ukuaji kilitokana na: mikakati iliyochukuliwa na Serikali kukabiliana na athari za vita nchini Ukraine; uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu, barabara, reli na viwanja vya ndege; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini husussan makaa ya mawe, jasi, chumvi, almasi, mawe ya chokaa na shaba; na kuongezeka kwa shughuli za utalii. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji kilipungua kwa nukta ya asilimia **0.2**

ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia **4.9** mwaka 2021 kutokana na athari ya vita kati ya Urusi na Ukraine iliyosababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji katika baadhi ya sekta pamoja na mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini **(Mchoro Na. 3).** Aidha, sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji mwaka 2022 ni pamoja na: sanaa na burudani iliyokua kwa asilimia **19.0;** madini (asilimia **10.9**); fedha na bima (asilimia **9.2**); malazi na huduma ya chakula (asilimia **9.0**) na umeme (asilimia **7.6)**.

**Mchoro Na.3:** Mwenendo wa Ukuaji kwa baadhi ya Sekta (%)




***Chanzo:*** *Ofisi ya Takwimu ya Taifa, 2023*

**(b) Sera za Kiuchumi**

Katika kuhakikisha sera za kiuchumi zinatabirika, Wizara ya Fedha iliendelea kushirikisha wadau mbalimbali ili kupata maoni na maboresho katika utungaji na utekelezaji wa sera za kodi. Hii inajumuiasha uratibu wa Kikosi Kazi cha Maboresho ya Sera za Kodi (*Task Force on Tax Reforms*) ambacho hukusanya na kuchambua maoni ya wadau kuhusu maboresho ya kodi, na tafiti kwa ajili ya kusaidia katika kufanya maamuzi (. Aidha, katika kuiwezesha nchi kuwa na sera za kodi zinazotabirika na kuweka mazingira bora ya uwekezaji pamoja na mambo mengine, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 ilifanyiwa marekebisho na kuanzisha utaratibu wa kurekebisha viwango vya Ushuru wa Bidhaa kila baada ya miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2023/24 badala ya viwango hivyo kurekebishwa kila mwaka.

**(c) Maeneo ya Kipaumbele ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Sekta ya Kilimo**

Katika kukuza uchumi Serikali imeandaa maeneo ya kipaumbele ambayo yanalenga kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia Sekta ya Kilimo ikiwemo utekelezaji wa ajenda 10/30 ambayo inalenga kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo cha mazao

kutoka asilimia 4.1 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 ambapo inatarajiwa mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi kuongezeka kutoka 1.2 bilioni mwaka 2022 hadi kufikia bilioni 5 ifikapo mwaka 2030. Azma hii, inaenda sambamba na utekelezaji wa Sera, Programu na Mipango ya Kitaifa ikiwemo Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), FYDPIII na ASDP. Katika kufanikisha hayo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imefanikiwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kushiriki kwenye uwekezaji wa mashamba makubwa ya pamoja kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT); kuhamasisha uwekezaji kwenye mazao yenye mahitaji makubwa ndani ya nchi ambayo yamekuwa yakitumia fedha nyingi kuagiza kutoka nje ambayo ni mafuta ya kula, ngano na sukari.

Serikali pia imeendelea kutoa vivutio vya kikodi kwa wawekezaji wa sekta ya mbolea ambayo uzalishaji umeshaanza katika kiwanda cha Itracom Fertilizer Limited kilichopo Nala Jiji la Dodoma chenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 180 na kinatarajiwa kutoa ajira za kudumu kwa wafanyakazi takriban 3,000 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 600,000 kwa mwaka. Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo imetoa mikopo 20 yenye thamani ya Shilingi 704,278,062.50. Aidha, Serikali kupitia AGITF imeanzisha huduma ya mikopo nafuu (*soft loan)* kwa ajili ya uwezeshaji vijana na wanawake kupata mitaji ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za kilimo. Huduma hiyo imewezesha upatikanaji wa mikopo ya Shilingi Milioni 200.

### 2.2.2 Kudumisha Hali ya Amani na Utulivu

Tanzania imeendelea kuwa nchi yenye amani na utulivu suala ambalo ni la msingi katika kuvutia uwekezaji nchini na pia kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika hatimaye kuchangia maendeleo ya Taifa. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara ya Mambo ya Ndani ilihakikisha usalama wa watu na mali zao pamoja na amani na utulivu kuendelea kuwepo. Katika kutekeleza jukumu hili masuala yafuatayo yalifanyika:-

(a) Serikali ilitoa kibali cha ajira mpya **6,608** kwa majeshi yaliyopo chini ya Wizara. Aidha, jumla ya maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia **7,282** walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili kuimarisha utendaji, kuwaongezea ujuzi, maarifa na stadi katika utekelezaji wa majukumu yao;

(b) Wizara ilishirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa. Jumla ya mashauri ya jinai **45,455** yalishughulikiwa pamoja na misako, doria na operesheni zilifanyika kwa ajili ya kupambana na uhalifu wa aina zote ambapo operesheni hizo zimewezesha kukamatwa kwa silaha mbalimbali na watuhumiwa 169 waliopatikana na silaha kinyume na sheria; na

(c) Jeshi la Polisi liliratibu kampeni ya usalimishaji wa silaha haramu kwa hiari ambapo jumla ya silaha 1,220 zilisalimishwa na jumla ya silaha 6,208 ziliteketezwa. Aidha, kuanzia mwezi Julai 2022, Jeshi la Polisi lilipeleka

askari katika Kata 3,956. Hatua hiyo ililenga kuimarisha ulinzi na usalama na kupambana na uhalifu.

### 2.2.3 Kuhakikisha Sera za Kiuchumi Zinatabirika na Kudhibiti Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei katika mwaka 2022 uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 3.7 mwaka 2021. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kulitokana na vita kati ya Urusi na Ukraine iliyosababisha kuongezeka kwa bei ya baadhi ya bidhaa muhimu kama mafuta, mbolea na ngano; kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika baadhi ya maeneo kutokana na mabadiliko ya tabianchi hususan katika maeneo yanayotegemea mvua za vuli; na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za chakula katika nchi jirani. Pamoja na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, bado upo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 5.0 na vigezo vya kikanda vya mtangamano wa kiuchumi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) vya asilimia 8.0 na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) asilimia kati ya 3 na 7 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.3**. Aidha, mfumuko wa bei ni mdogo ikilinganishwa na mfumuko wa bei katika nchi nyingi wanachama wa EAC na SADC.

**Jedwali Na. 3:** Viwango vya Mfumuko wa Bei Nchi za SADCna EAC kwa mwaka 2021 – 2022

| S/Na. | Nchi za SADC | | | Nchi za EAC | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Nchi** | **2021** | **2022** | **Nchi** | **2021** | **2022** |
| 1. | Angola | 25.8 | 21.4 | Tanzania | 3.7 | 4.3 |
| 2. | Botswana | 6.7 | 12.2 | Uganda | 2.2 | 6.8 |
| 3. | Tanzania | 3.7 | 4.4 | Kenya | 6.1 | 7.6 |
| 4. | DRC | 9.0 | 9.0 | Rwanda | 0.8 | 13.9 |
| 5. | Eswatin | 3.7 | 4.8 | Burundi | 8.3 | 18.9 |
| 6. | Lesotho | 6.0 | 8.2 | Sudani ya Kusini | 30.2 | 17.6 |
| 7. | Madagascar | 5.8 | 8.2 | DRC | 9.0 | 9.0 |
| 8. | Malawi | 9.3 | 20.8 | **Wastani wa Afrika Mashariki** | **8.6** | **11.2** |
| 9. | Mauritius | 4.0 | 10.8 | | | |
| 10. | Msumbiji | 5.7 | 9.8 | | | |
| 11. | Namibia | 3.6 | 6.1 | | | |
| 12. | Seychelles | 9.8 | 2.7 | | | |
| 13. | Africa Kusini | 4.6 | 6.9 | | | |
| 14. | Zambia | 22.0 | 11.0 | | | |
| 15. | Zimbabwe | 98.5 | 193.4 | | | |
| **Wastani kwa nchi za SADC** | | **14.5** | **22.0** | | | |

***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (World Economic Outlook), 2023*

Kufuatia kuongezeka kwa mfumuko wa bei, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kupunguza makali ya ongezeko la bei katika maisha ya wananchi kama inavyoonesha katika kipengele (a) hadi (c).

**(a) Kuongeza bajeti ya Sekta ya Kilimo**

Serikali iliongeza bajeti katika sekta za uzalishaji ikiwemo kilimo na nishati kutokana na fursa zilizopo katika sekta hizo na uwezo wa kuhimili changamoto ikiwemo UVIKO 19 na vita vya Ukraine. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanaonesha kuwa bajeti ya sekta ya kilimo iliongezeka kutoka shilingi bilioni **630.4** mwaka 2021/22 hadi shilling bilioni **1,216.2** mwaka 2022/23. Ongezeko la bajeti pamoja na mambo mengine iliwezesha utoaji wa ruzuku katika pembejeo za kilimo hususan mbolea pamoja na kuboresha miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji na hivyo kupunguza kasi ya mfumuko wa bei katika muda wa kati na mrefu.

**(b) Kutoa Ruzuku ya Mafuta ya Petroli**

Katika kipindi cha mwezi Juni hadi Desemba 2022, Serikali ilitoa ruzuku ya mafuta ya shilingi bilioni **479.4** kwa ajili ya kukabaliana na ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia. Aidha, ruzuku hii iliwezesha bei ya mafuta ya petroli katika soko la ndani kupungua na hatimaye kuchangia kupunguza gharama za uzalishaji pamoja na usafirishaji wa bidhaa na huduma.

**(c) Sera ya Fedha yenye Kupunguza Kasi ya Ujazi wa Fedha**

Mwaka 2022/23 Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza sera ya fedha yenye kupunguza kasi ya ujazi wa fedha wa kuimarisha mwenendo wa bei (*price stabilisation*) na kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, sera hiyo ilitekelezwa kwa lengo la kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa kati ya asilimia **3.0** hadi **7.0.** Kutokana na jitihada zilizochukuliwa na Serikali mfumuko wa bei uliendelea kupungua na kufikia asilimia **3.6** mwezi Juni, 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia **4.4** katika kipindi kama hicho mwaka 2022 kama inavyoonesha **Jedwali Na.4**. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza Sera ya Fedha yenye kupunguza kasi ya ujazi wa fedha na kuimarisha mwenendo wa bei (price stabilization) na kuendelea kuchochea ukuaji wa uchumi. Sera hiyo ilitekelezwa kwa lengo la kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa kati ya asilimia 3 hadi 7.

**Jedwali Na. 4**: Hali ya Mfumko wa Bei

| Mwaka | Vyakula na Vinywaji Baridi | Vinywaji Vikali na Tumbaku | Mavazi na Viatu | Makazi, Maji, Umeme, Gesi na Nishati Nyinginezo | Samani, Vifaa vya Nyumbani na Ukarabati wa Makazi | Afya | Usafiri | Habari na Mawasiliano | Burudani, Michezo na Utamaduni | Huduma za Elimu | Migahawa na Huduma za Malazi | Huduma za Bima na Fedha | Usafiri Binafsi, Hifadhi ya Jamii na Bidhaa na Huduma Mchanganyiko | Fahirisi Bidhaa Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Wakazi Wenye Kipato Cha Chini** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 0.6 | 7.3 | 3.1 | 2.9 | 3.9 | 1.9 | 7.4 | 1.4 | 3.8 | 10.3 | 5.5 | 0.0 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 7.5 | 0.5 | 3.7 | 3.9 | 6.3 | 2.9 | 2.1 | 1.8 | 13.3 | 2.3 | 3.0 | 0.0 | 3.5 | 4.7 |
| **Wakazi Wenye Kipato Cha Kati** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 1.2 | 4.2 | 0.7 | -1.1 | 4.1 | 4.0 | 2.7 | 1.3 | 0.5 | 5.4 | 10.1 | 0.4 | 0.7 | 2.4 |
| **2022** | 9.5 | 0.5 | 2.6 | 5.0 | 4.5 | 1.8 | 7.3 | 0.2 | 16.5 | 1.2 | 3.7 | 0.1 | 3.4 | 5.8 |
| **Wakazi Wenye Kipato Cha Juu** | | | | | | | | | | | | | | |
| **2021** | 3.9 | 11.2 | 3.4 | 0.1 | 8.2 | 3.3 | 1.8 | 1.3 | -1.3 | 3.0 | 7.0 | 0.2 | 1.5 | 3.0 |
| **2022** | 4.8 | 2.3 | 3.1 | 3.4 | 2.5 | 2.0 | 5.9 | 1.1 | 2.3 | 0.8 | 4.0 | 0.0 | 2.3 | 3.8 |

***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023*

### 2.2.4 Uwezeshaji Watanzania Kuingia Ubia na Wawekezaji wa Nje

Ili kuongeza ushiriki wa watanzania katika shughuli za kiuchumi sera, sheria na mikakati imeandaliwa kupitia sekta mbalimbali ili kuwezesha watanzania kuingia ubia na wawekezaji wa nje. Lengo la kuwawezesha watanzania kuingia ubia na wawekezaji wa nje ni pamoja na kujengea uwezo wa kampuni za ndani kwenye masuala ya uendeshaji wa biashara na kuhaulisha teknolojia. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 369 ambayo inakadiriwa kuwekeza kiasi cha mtaji wa Dola za Marekeani milioni 5,394.83 na kutoa jumla ya ajira 53,871 ikilinganisha na miradi 274 iliyosajiliwa katika mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la asilimia 35. Ongezeko hili lilitokana na hatua madhubuti za uhamasishaji zilizochukuliwa kuweka mazingira wezeshi ya kuwavutia wawekezaji ambapo kati ya miradi 369 iliyosajiliwa, miradi 89 ilikuwa miradi yenye ubia. Sekta ambazo zina idadi kubwa ya miradi ya ubia ni viwanda (41), usafirishaji (16) na utalii (11). **Jedwali Na.5** linaonesha sekta na idadi ya miradi katika sekta husika iliyofanyika kwa ubia.

**Jedwali Na. 5:** Uwekezaji kwa sekta na Aina ya Umiliki

| Sekta | Idadi ya miradi | Miradi Mipya | Miradi ya Upanuzi | Miradi inayomilikiwa na watanzania | Miradi inayomilikiwa na wageni | Miradi ya Ubia | Ajira | Mtaji ($M) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwanda | 160 | 157 | 3 | 50 | 69 | 41 | 23,070 | 3,334.47 |
| Usafirishaji | 80 | 73 | 7 | 40 | 24 | 16 | 15,994 | 1,140.64 |
| Utalii | 37 | 36 | 1 | 14 | 12 | 11 | 2,149 | 117.66 |
| Majengo ya Biashara / Ujenzi | 33 | 32 | 1 | 13 | 16 | 4 | 2,415 | 526 |
| Kilimo | 28 | 27 | 1 | 6 | 16 | 6 | 7,740 | 168.53 |
| Huduma | 17 | 17 | 0 | 3 | 8 | 6 | 1,407 | 41.22 |
| Rasilimali watu | 7 | 7 | 0 | 1 | 2 | 4 | 549 | 11.81 |
| Miundom-binu ya Uchumi | 4 | 4 | 0 | 2 | 2 | 0 | 164 | 30.68 |
| Nishati | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 13 | 19.83 |
| Madini na Petroli | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 370 | 4.00 |
| **Jumla** | **369** | **356** | **13** | **131** | **149** | **89** | **53,871** | **5,394.83** |

***Chanzo:*** *Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2023*

### 2.2.5 Uzalishaji Bidhaa Bora zenye Bei Shindani

Katika kuhakikisha watanzania wanazalisha bidhaa zenye ubora, Serikali kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilifanikiwa kutoa jumla ya leseni **874** za alama ya ubora kwa bidhaa ambapo leseni **429** sawa na **asilimia 49.1** zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo sawa na ongezeko la **asilimia 21.5** ikilinganishwa na leseni **353** zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2021/2022. Jumla ya leseni **686** ziliongezewa muda wa matumizi ya alama ya ubora. Aidha, mafunzo **61** yalitolewa kwa wajasiriamali wadogo (MSEs) na wadau mbalimbali wapatao **1,724** katika dhana nzima ya kuwawezesha kuzalisha bidhaa zinazokidhi matakwa ya viwango vya ubora na usalama ili kuwezesha kukidhi ushindani wa masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Mikoa iliyonufaika na mafunzo hayo ni *Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Singida, Pwani, Kigoma, Mara, Mtwara, Lindi, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, na Geita.*

Serikali iliendelea kuhimiza uwekezaji katika viwanda ili kukuza uchumi wa nchi pamoja na kuzalisha bidhaa zilizo bora. Takwimu zinaonesha mwaka 2022/23 idadi ya viwanda ilikuwa **43,151** ambapo viwanda vikubwa vilikuwa **358**, vya kati **34,488** na vidogo **8,305** kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.6.** Uwepo wa viwanda hivyo, umewezesha kuzalisha idadi ya ajira **225,036** ambapo mchanganuo waajiriwa wenye ujuzi wa juu wakiwa **45,007**, ujuzi wa kati **67,508** na wasio na ujuzi **112,526**.

**Jedwali Na. 6:** Takwimu za Viwanda Vidogo, Kati na Vikubwa

| Mkoa | Ukumbwa wa Kiwanda | | | Idadi ya Ajira | Ujuzi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Vidogo | Kati | Vikubwa | | Juu | Kati | Wasio na Ujuzi |
| Dodoma | 600 | 2,278 | 8 | 441 | 89 | 132 | 220 |
| Arusha | 693 | 1,547 | 69 | 709 | 142 | 213 | 356 |
| Kilimanjaro | 629 | 1,146 | 17 | 912 | 182 | 274 | 456 |
| Morogoro | 820 | 3,731 | 39 | 23,264 | 4,652 | 6,979 | 11,633 |
| Pwani | 213 | 58 | 10 | 16,569 | 3,313 | 4,970 | 8,286 |
| Dar es Salaam | 1,147 | 6,334 | 118 | 94,932 | 18,986 | 28,479 | 47,467 |
| Lindi | 13 | 820 | 13 | 4,240 | 848 | 1,272 | 2,120 |
| Mtwara | 222 | 1,235 | 7 | 5,450 | 1,090 | 1,635 | 2,725 |
| Ruvuma | - | 1,473 | - | 2,994 | 599 | 898 | 1,497 |
| Singida | 472 | 2,141 | 6 | 9,528 | 1,905 | 2,858 | 4,765 |
| Tabora | 190 | 1,448 | 8 | 5,626 | 1,125 | 1,687 | 2,814 |
| Shinyanga | 962 | 1,041 | 16 | 12,750 | 2,550 | 3,825 | 6,375 |
| Kagera | 468 | 2,917 | 9 | 10,054 | 2,010 | 3,016 | 5,028 |
| Mwanza | 764 | 1,960 | 18 | 12,709 | 2,542 | 3,813 | 6,354 |
| Mara | 813 | 4,188 | 19 | 18,245 | 3,649 | 5,474 | 9,122 |
| Simiyu | 158 | 796 | - | 2,732 | 546 | 819 | 1,367 |
| Geita | 141 | 1,375 | 1 | 3,881 | 776 | 1,164 | 1,941 |
| **Jumla** | **8,305** | **34,488** | **358** | **225,036** | **45,007** | **67,508** | **112,526** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara, 2023*

Ajira za watanzania kwenye viwanda zimekuwa zikiongezeka katika kila aina ya ujuzi huku pia ajira za wageni zikiongezeka hali ambayo inachangia kurithisha ujuzi na kuhaulisha teknolojia katika shughuli za viwanda. Hivyo, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa na Serikali imeendelea kuchukua jitihada za makusudi ili kuwezesha watanzania kunufaika na uwekezaji unaofanyika nchini kwenye viwanda ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la wageni wenye ujuzi wa juu kutoka **980** mwaka 2021/22 hadi kufikia **16,202** kwa mwaka 2022/23. Hali hii inaonesha kuwa, Serikali imeendelea kuweka na kuboresha vivutio vinavyochochewa na uwepo wa mazingira wezeshi ya uwekezaji ambapo pia pamoja na mambo mengine umechangia kuongezeka kwa viwanda nchini. Tathmini inaonesha kuwa, ushiriki wa watanzania kwenye viwanda umekuwa mkubwa katika eneo la ajira za wasio na ujuzi ambapo mwaka 2022/23 zikiwa **77,638** ikilinganishwa na wageni wakiwa **6,131;** wakati watanzania wenye ujuzi wakiwa ni **36,569** na wageni wakiwa ni **24,642** huku wale wenye ujuzi wa kati watanzania wakiwa ni **62,446** na wageni ni **17,610** kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.7**. Kutokana na hali hii, jitihada za kuboresha mfumo wa elimu ziongezwe ili kuongeza idadi ya ajira za watanzania wenye ujuzi wa juu na wa kati kunufaika na mageuzi makubwa ya uwekezaji katika viwanda na hatimaye ajira nyingi viwandani kuajiriwa watanzania wenye maarifa, ujuzi na uzoefu.

**Jedwali Na. 7:** Ajira Viwandani kwa Mwaka 2022/23

| Aina ya Viwanda | Watanzania | | | Wageni | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ujuzi wa Juu | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | Ujuzi wa Juu | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi |
| Vidogo | 5,064 | 15,189 | 30,380 | 563 | 4,782 | 281 |
| Vya Kati | 12,602 | 18,903 | 31,505 | 7,877 | 4,726 | 3,150 |
| Vikubwa | 18,903 | 28,354 | 15,753 | 16,202 | 8,102 | 2,700 |
| **Jumla** | **36,569** | **62,446** | **77,638** | **24,642** | **17,610** | **6,131** |
| **Ajira Viwandani kwa Mwaka 2021/2022** | | | | | | |
| **Aina ya Viwanda** | **Watanzania** | | | **Wageni** | | |
| | **Ujuzi wa Juu** | **Ujuzi wa Kati** | **Wasio na Ujuzi** | **Ujuzi wa Juu** | **Ujuzi wa Kati** | **Wasio na Ujuzi** |
| Vidogo | 333 | 665 | 2,328 | 158 | 17 | - |
| Vya Kati | 2,311 | 3,466 | 5,777 | 1,027 | 193 | 64 |
| Vikubwa | 560 | 2,241 | 2,801 | 980 | 280 | 140 |
| **Jumla** | **3,204** | **6,372** | **10,906** | **2,165** | **490** | **204** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara, 2023*

### 2.2.6 Usajili wa Miradi na Mitaji

Katika kipindi cha mwaka wa fedha, 2022/23, tathmini inaonesha kuwa idadi kubwa ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa ipo katika sekta za: Uzalishaji viwandani miradi 160 (43.36%), Usafirishaji miradi 80 (21.68%), Utalii miradi 37 (10.03%), sekta ya

Ujenzi wa majengo ya biashara miradi 33 (948%) na Kilimo miradi 28 (7.59%). **Jedwali Na.8** linaonesha sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kuwa na mtaji wa jumla za Dola za Marekani Milioni 3,334.47 sawa na asilimia 61.81% ikifuatiwa na Sekta ya Usafirishaji kwa mtaji wa Dola za Marekani Milioni 1,140.64 sawa na asilimia 21.14%, na Sekta ya Majengo ya Biashara/Ujenzi yenye mtaji wa Dola za Marekani Milioni 526 sawa na asilimia (9.75%). Aidha, kwa upande wa ajira za moja kwa moja, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa uzalishaji wa ajira kwa kuwa na jumla ya ajira 23,070 sawa na asilimia 42.82, ikifuatiwa na sekta ya usafirishaji 15,994 (29.69%) na Sekta ya Kilimo yenye jumla ya ajira 7,740 (14.37).

**Jedwali Na. 8:** Miradi iliyosajiliwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/23

| Sekta | Idadi ya Miradi | % ya Miradi iliyosajiliwa | Mtaji ($M) | Mitaji (%) | Ajira | Ajira (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Viwanda | 160 | 43.36% | 3,334.47 | 61.81% | 23070 | 42.82% |
| Usafirishaji | 80 | 21.68% | 1,140.64 | 21.14% | 15994 | 29.69% |
| Utalii | 37 | 10.03% | 117.66 | 2.18% | 2149 | 3.99% |
| Majengo ya Biashara/ Ujenzi | 33 | 8.94% | 526 | 9.75% | 2415 | 4.48% |
| Kilimo | 28 | 7.59% | 168.53 | 3.12% | 7740 | 14.37% |
| Huduma | 17 | 4.61% | 41.22 | 0.76% | 1407 | 2.61% |
| Rasilimali Watu | 7 | 1.90% | 11.81 | 0.22% | 549 | 1.02% |
| Miundombinu ya Uchumi | 4 | 1.08% | 30.68 | 0.57% | 164 | 0.30% |
| Nishati | 2 | 0.54% | 19.83 | 0.37% | 13 | 0.02% |
| Madini & Petroli | 1 | 0.27% | 4 | 0.07% | 370 | 0.69% |
| **Jumla** | **369** | **100.00%** | **5,394.84** | **5,394.84** | **53871** | **100.00%** |

***Chanzo:*** *Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2023*

Kati ya miradi 369 iliyosajiliwa kwa mwaka wa fedha, 2022/23, jumla ya miradi 131 (36%) inamilikiwa na watanzania, miradi 149 (40%) inamilikiwa na wageni na miradi 89 (24%) ni ya ubia kati ya watanzania na wageni kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.9**.

**Jedwali Na. 9:** Umiliki wa Miradi ya Uwekezaji Iliyosajiliwa

| Sekta | Miradi inayomilikiwa na Watanzania | Miradi inayomilikiwa na Wageni | Miradi ya Ubia |
|---|---|---|---|
| Kilimo | 6 | 16 | 6 |
| Majengo ya Biashara/ Ujenzi | 13 | 16 | 4 |
| Miundombinu ya Uchumi | 2 | 2 | 0 |
| Nishati | 1 | 0 | 1 |
| Rasilimali Watu | 1 | 2 | 4 |
| Viwanda | 50 | 69 | 41 |
| Madini & Petroli | 1 | 0 | 0 |
| Huduma | 3 | 8 | 6 |
| Utalii | 14 | 12 | 11 |
| Usafirishaji | 40 | 24 | 16 |
| **Jumla** | **131** | **149** | **89** |

***Chanzo:*** *Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2023*

### 2.2.7 Usajili wa Miradi kwa Mikoa

Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, inaonesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2022/23, Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kusajili miradi 154 (41.73%), ukifuatiwa na Mkoa wa Pwani kwa miradi 63 (17.07%), na Mkoa wa Arusha na Dodoma 18 (4.88) kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.10**. Aidha, Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Faciliation Centre) zilitolewa zlitolewa kwa wawekezaji kama vibali na ushauri ambapo jumla wawekezaji 9,156 walipata vibali na leseni mbalimbali. Pia, ushauri ulitolewa kwa wawekezaji na wadau 7,306. Mawasiliano na wawekezaji 3,022 walifikiwa kwa njia ya simu na ana kwa ana kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili pamoja na kujua hali ya uwekezaji ikilinganishwa na wa wawekezaji 1,196 waliofikiwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 152. Serikali kupitia TIC iliweza kutembelea miradi ya wawekezaji 461 ikilinganishwa na miradi 539 iliyotembelewa ili kutathmini utekelezaji wa miradi.

**Jedwali Na.10:** Usajili na Ajira za Miradi ya Uwekezaji katika Mikoa

| Mkoa | Idadi ya Miradi | % ya Miradi Iliyosajiliwa | Ajira | Mtaji ($) |
|---|---|---|---|---|
| Dar Es Salaam | 154 | 41.73% | 21,175 | 1,701.45 |
| Pwani | 63 | 17.07% | 14860 | 1,269.24 |
| Arusha | 18 | 4.88% | 1956 | 146.97 |
| Dodoma | 18 | 4.88% | 2083 | 119.55 |
| Mwanza | 15 | 4.07% | 994 | 32.72 |
| Tanga | 12 | 3.25% | 925 | 68.72 |

| Mkoa | Idadi ya Miradi | % ya Miradi Iliyosajiliwa | Ajira | Mtaji ($) |
|---|---|---|---|---|
| Kilimanjaro | 10 | 2.71% | 1206 | 15.63 |
| Shinyanga | 10 | 2.71% | 790 | 85.47 |
| Mbeya | 7 | 1.90% | 582 | 24.64 |
| Morogoro | 7 | 1.90% | 826 | 47.59 |
| Ruvuma | 7 | 1.90% | 1556 | 57.69 |
| Kigoma | 6 | 1.63% | 889 | 16.91 |
| Lindi | 5 | 1.36% | 117 | 8.11 |
| Mara | 5 | 1.36% | 263 | 32.98 |
| Njombe | 5 | 1.36% | 2903 | 1,584.76 |
| Geita | 4 | 1.08% | 146 | 9.65 |
| Manyara | 4 | 1.08% | 206 | 10.97 |
| Singida | 4 | 1.08% | 78 | 5.71 |
| Iringa | 3 | 0.81% | 532 | 76.05 |
| Katavi | 3 | 0.81% | 451 | 30.80 |
| Simiyu | 3 | 0.81% | 472 | 18.19 |
| Kagera | 2 | 0.54% | 393 | 15.31 |
| Tabora | 2 | 0.54% | 275 | 11.58 |
| Mtwara | 1 | 0.27% | 8 | 0.50 |
| Rukwa | 1 | 0.27% | 185 | 3.65 |
| **Jumla** | **369** | **100.00%** | **53871** | **5,394.83** |

***Chanzo:*** *Kituo cha Uwekezaji Tanzania, 2023.*

### 2.2.8 Mikataba ya Utekelezaji wa Wawekezaji wa Kimkakati

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia TIC ilisaini mikataba ya utekelezaji na kampuni **10** ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati iliyotokana na uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji yanayolenga kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wawekezaji. Miradi hiyo ina thamani ya Dola za Marekani Milioni 1805.12 na inatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja 16,355.

Miradi hiyo ni mradi wa kongani ya viwanda - Sinotan unaotekelezwa Kwala Mkoani Pwani; Mradi wa upanuzi wa Kilombero Sugar (Morogoro); Mradi wa WILMAR (Kihonda - Morogoro); Mradi wa Upanuzi wa kiwanda cha uzalishaji wa saruji wa Lake Cement (Kigamboni Dar Es Salaam); Mradi wa kusindika na kuhifadhi Gesi ya LPG na miundombinu ya Gas wa Oilcom (Dar Es Salaam); Mradi wa *Wild Flower and Oil Mills* (Manguanyuki Singida); Mradi wa Mufindi Paper Mills (Kigoma); Mradi wa Lodhia Steel (Mkuranga – Pwani); Miradi ya Dangote Cement unaotekelezwa Mkoani Mtwara; na Mradi wa Mount Meru Millers unaotekelezwa Mkoani Singida.

### 2.2.9 Matumizi ya Teknolojia ya Kisasa katika Shughuli za Kiuchumi

Katika kipindi cha mwa 2022/23, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kukuza uchumi wa kidigitali katika kuhimiza matumizi ya teknolojia za kisasa katika shughuli za kiuchumi. Katika mwaka 2022/23, Serikali imeboresha mfumo wa kidijitali wa anwani za Makazi unaojulikana kama NaPA kwa kuwezesha mfumo kutambua zilipo huduma za kijamii na kiuchumi na kuwezesha taasisi za Serikali na sekta binafsi kutumia taarifa zilizopo kwenye mfumo huo. Aidha, Serikali ilitengeneza mfumo jumuishi utakowezesha kuwa na taarifa zote za wabunifu wa TEHAMA nchini, kampuni za TEHAMA, wawekezaji katika huduma na bidhaa za ubunifu katika TEHAMA, vituo atamizi vya TEHAMA, Vituo vya uendelezaji bunifu za kidijitali pamoja na taasisi za fedha zinazotoa mitaji kwa wabunifu wa TEHAMA. Lengo la mfumo huo ni kutambua bunifu kwa lengo la kukuza pato la Taifa na kuongeza fursa za ajira.

Serikali kupitia Tume ya TEHAMA imewezesha kampuni changa (ICT startups) 9 kuanza kutoa huduma na imekamilisha upembuzi yakinifu kuhusu kuanzishwa kwa Taasisi ya TEHAMA (zonal soft centers) na vituo vinne vya ubunifu wa TEHAMA. Lengo la Taasisi hii ni kukuza ubunifu wa TEHAMA nchini na kuleta mapinduzi ya kidijitali; na kuiongezea uwezo minara inayotumia teknolojia ya 2G pekee ili iweze kutoa pia huduma ya intaneti kwa kiwango cha 3G na 4G na kuwawezesha wananchi kupata huduma za kidijitali. Hali halisi ya utekelezaji inaonesha hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya minara 227 imeongezewa uwezo ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

### 2.2.10 Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara

Serikali iliandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI) mwaka 2018 kwa lengo la kuboresha taratibu za udhibiti, kuondoa mwingiliano wa majukumu, kukuza uwazi, na kuanzisha muundo wa ufuatiliaji na tathmini wenye ufanisi katika kukuza uwekezaji na biashara. Ili kutekeleza Mpango huo, Mpango Kazi wa utekelezaji uliandaliwa na kuanza kutumika mwaka 2019. MKUMBI unatekelezwa na sekta mbalimbali ambapo unaongozwa na Kamati ya Makatibu Wakuu chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu).

MKUMBI unalenga kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kupunguza au kuondoa changamoto mbalimbali katika taratibu za uwekezaji na ufanyaji biashara kama vile majukumu ya taasisi yanayofanana/yanayoingiliana, ucheleweshwaji wa vibali vya uwekezaji na biashara, na gharama kubwa ya ada na tozo. MKUMBI unalenga kufanya maboresho mbalimbali kwa: kufanya mapitio ya Sheria zilizobainika kukwamisha/kuchelewesha uanzishwaji na uendeshaji wa uwekezaji na biashara; kufanya mapitio ya tozo ambazo ni kero na kupendekeza kupunguza au kufutwa; kuunganisha majukumu ya taasisi yanayofanana na kuondoa yale yanayoingiliana; na kuweka mifumo ya kieletroniki ya utoaji huduma kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwazi kwa jumuiya ya wawekezaji na wafanyabiashara. Katika kipindi cha  kuanzia Julai, 2022 hadi Juni, 2023 shughuli mbalimbali za MKUMBI zilitekelezwa kama zilivyoainishwa katika kipengele (a) hadi (f).

**(a) Tathmini ya Utekelezaji wa MKUMBI**
Mwezi Julai, 2022 Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa MKUMBI (*Blueprint Impact Assessment Report*). Tathmini hiyo ililenga kubainisha athari chanya na hasi za utekelezaji wa MKUMBI katika ukuzaji uwekezaji na biashara kwa kipindi cha utekelezaji kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22.

**(b) Kitengo cha Mazingira ya Biashara**
Serikali imeanzisha kitengo maalumu cha kuratibu utekelezaji wa MKUMBI. Kitengo hiki kinajulikana kama Kitengo cha Kuboresha Mazingira ya Biashara (*Business Environment Unit – BEU*). Lengo ni kuongeza kasi ya utekelezaji, uratibu na mawasiliano kuhusu utekelezaji wa MKUMBI.

**(c) Marekebisho ya Sheria**
Serikali imepitia na kurekebisha Sheria na Kanuni 14 hususan katika Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Kilimo, Ufugaji, Afya, na Maliasili na Utalii ili kuboresha mazingira ya biashara. Marekebisho ya sheria hizo yamesaidia kupunguza ushuru na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji, kukuza biashara na uchumi kwa ujumla. Aidha, Sheria ya Taifa ya Uwekezaji (1997) ilifanyiwa maboresho na kutungwa Sheria mpya ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 ambayo tayari imechapishwa katika Gazeti la Serikali namba 45 toleo la 10 la tarehe 02 Desemba 2022. Aidha, kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, kati ya sheria 16 zilizopendekezwa kufanyiwa maboresho, sheria 13 zinahusu maboresho yanayolenga ama kupunguza au kuondoa kodi, ada, tozo na kupunguza au kuweka misamaha ya ushuru wa forodha. Sheria hizo ni: Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148; Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290; Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, 2015 na Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306; Sheria ya Uhamiaji, SURA 54; Sheria ya Ardhi, SURA 113; Sheria ya Madini, SURA 123; Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41; Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196; na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

**(d) Kuondoa Majukumu Yanayoingiliana au Kufanana**
Serikali imeondoa muingiliano wa majukumu uliokuwepo kati ya Taasisi ya Udhibiti na Viatilifu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI) na Idara ya Mimea. Pia, Serikali imeondoa haki ya upekee (*exclusive mandate*) kwa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) ya kutoa huduma ya uondoaji na usafirishaji wa shehena kwa njia ya maji (*clearing and forwarding*) kwa kuipunguzia idadi ya bidhaa zilizokuwa ni lazima kufanywa na Shirika hilo.

**(e) Vituo vya Huduma za Mahali Pamoja na Dirisha moja la Huduma**
Serikali imefanya marekebisho kwenye Kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Urban Authority) SURA, 287 ili kuweka sharti la Mamlaka za Miji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya uratibu, uhamasishaji na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara. Aidha, imefanya marekebisho kwenye Kifungu cha

113 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (District Authorities) Sura 288 ili kuweka sharti la Mamlaka za Vijiji kuanzisha vituo vya pamoja kwa ajili ya uratibu, uhamasishaji na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara.

### 2.2.11 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji

Kutokana na jitihada zilizofanyika katika kukuza uchumi na kujenga mazingira ya uwekezaji, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(i) Kituo cha Uwekezaji Tanzania kimeboresha na kuainisha taarifa za miradi ipatayo 184 inayotafuta wawekezaji (Ubia) wa aina tofauti tofauti. Miradi hiyo 184 imeanishwa katika Sekta za Kilimo, Nishati, Usafirishaji, na Viwanda. Jumla ya miradi 133 iko katika sekta ya umma na miradi 51 iko katika sekta binafsi ikionesha fursa za uwekezaji zilizopo pembezoni mwa mradi wa Reli ya Kisasa - SGR pindi itakapokamilika na sehemu mbalimbali nchini. Serikali kupitia TIC ilisaini mikataba ya utekelezaji na kampuni 13 za utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati na kimkakati maalum. Miradi kumi (10) ya kimkakati na Kimkakati Maalum ambayo imesaini mikataba ya utekelezaji na TIC ina thamani zaidi ya Dola za Marekani Milioni 1805.12 na inatarajiwa kuzalisha ajira za moja kwa moja zaidi ya 16,355;

(ii) Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2023 jumla ya miradi 13 iliweza kusajiliwa kwa ajili ya kufanya upanuzi na inategemea kuzalisha ajira 2,102 na kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani Milioni 213.83 ambapo katika kipindi kama hicho kwa mwaka, 2022 hakukuwa na miradi ya upanuzi iliyosajiliwa; na

(iii) Kuimarishwa kwa Kituo cha Utoaji wa Huduma za Mahali Pamoja kilichopo TIC *"One Stop Facilitation Centre"*. Hadi Juni, 2023, taasisi 12 za Serikali zinatoa huduma katika Kituo cha mahali pamoja. Taasisi hizo ni Wizara ya Kazi, Wizara ya Ardhi, Uhamiaji, NIDA, NEMC, TRA, BRELA, TBS, TMDA, OSHA, TANESCO na TIC yenyewe. Maboresho mengine yaliyofanyika ni pamoja na kuboresha mfumo wa kusajili miradi ya uwekezaji yaani "Tanzania Investment Window (TIW)" ambao unapatikana kwa mtandao ***https://onestopshop.tic.go.tz***. Hivyo, umetoa urahisi kwa mwekezaji kusajili mradi wake TIC akiwa mahali popote duniani bila kufika TIC ndani ya siku moja hadi tatu. Serikali imeanzisha Kituo cha Mawasiliano kwa Wawekezaji "Tanzania Investment Call Centre" ambayo mtu yeyote anayetaka ufafanuzi, elimu na taratibu kuhusu masuala ya uwekezaji anaweza kupiga simu na kupata ufafanuzi au ufumbuzi wa jambo lolote linalohusiana na uwekezaji.

Pamoja na mafanikio hayo bado kuna changamoto zinazoathiri katika kukuza uchumi na kujenga mazingira ya uwekezaji. Changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo ni kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 11.**

**Jedwali Na. 11:** Changamoto na Mikakati katika Kukuza Uchumi na Kujenga Mazingira ya Uwekezaji

| ***Changamoto*** | ***Mikakati ya Kutatua Changamoto*** |
|---|---|
| *(i) Uanzishwaji wa Tozo, Leseni na Vibali vipya.* | *(i) Kuendelea kufanya mapitio ya Sheria, Kanuni na Taratibu ambazo zinazozorotesha uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.* |
| *(ii) Baadhi ya huduma zinazotolewa kwa njia ya mifumo kushindwa kupatikana kwa wakati kutokana na mtandao kutokuwa mzuri.* | *(ii) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu kama barabara, bandari, viwanja vya ndege, ambavyo vinahitaji kufanyiwa maboresho kwa ajili ya kuifanya nchi kuwa mahala salama pa uwekezaji. Hatua Madhubuti ni muhimu zikachukuliwa katika kuwa na sera na vivutio vinavyoendana na mabadiliko na fursa zilizopo dunia.* |
| *(iii) Kukosekana kwa miundombinu wezeshi na rafiki katika maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji. Miundombinu hiyo ni barabara, maji, umeme wa uhakika, reli na bandari hivyo kupelekea uwekezaji mwingi wa miradi kujazana katika mikoa yenye miundombinu imara kama Dar es Salaam, Pwani, Arusha, na Mwanza.* | *(iii) Kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu wezeshi kwa kutoa kipaumbele katika maeneo yaliyotengwa maalum kwa ajili ya uwekezaji.* <br> *(iv) Kutekeleza mikakati ya kubuni na kuvumbua vyanzo mbadala vya kuzalisha umeme ili kukuza uchumi.* |
| *(iv) Ukosefu wa umeme wa uhakika na kuathiri shughuli za uzalishaji na biashara kwa ujumla.* <br> *(v) Bidhaa zinazozalishwa ndani kushindwa kuhimili ushindani katika soko kutokana na ubora mdogo.* | *(v) Ajira kwa watanzania wenye ujuzi kwenye viwanda vikubwa zinaonesha kuwa pungufu ya wageni kwa idadi ya 420 sawa na 42%. Jitihada za kuboresha mfumo wa elimu ziongezwe ili kuongeza idadi ya ajira za watanzania wenye ujuzi. Vilevile, idadi ya watanzania wasio na ujuzi inaonesha kuwa juu ukilinganisha na wageni. Serikali inapaswa kufanya jitihada za makusudi ili kupunguza idadi ya watanzania wasio na ujuzi. Idadi ya ajira za wageni wasio na ujuzi zinaonesha kuongezeka ukilinganisha na mwaka 2021/22, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa na mamlaka ili kuwezesha watanzania kunufaika na uwekezaji unaofanywa nchini.* |
| *(vi) Ukosefu wa maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa ambayo tayari yamelipwa gharama za fidia na kodi za pango la ardhi* | *(vi) Ushiriki wa watanzania unaonesha kuongezeka ukilinganisha na mwaka 2021/22, jitahada ziongezwe na mamlaka ili kuleta tija zaidi kwa maslahi ya Taifa.* |

## 2.3 MFUMO NA UTAWALA WA KODI, SHERIA, KANUNI, LESENI NA HUDUMA ZA SERIKALI

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Wizara za kisekta imeendelea kusimamia mifumo ya kodi nchini ili kutatua changamoto zinazowakabili wananachi ikiwa ni pamoja na wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanyabiashara, wenye viwanda, wasanii na watumishi. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kusimamia kodi. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ndio chombo kikuu kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.11 ya mwaka 1995, kwa lengo la kusimamia kwa uadilifu kodi mbalimbali za Serikali Kuu.

Mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imefanya mapitio kwenye Sheria mbalimbali za kodi yenye lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara. Aidha, Serikali kupitia taasisi za udhibiti imeanza matumizi ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu (Single Window Payment System) na kuweka utaratibu mzuri wa ukaguzi ambao hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo. Katika kuboresha mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma za Serikali, mikakati mbalimbali imetekelezwa kama ilivyobainishwa katika kipengele 2.3.1 hadi 2.3.6.

### 2.3.1 Marekebisho ya Kodi Yaliyofanywa

Serikali imefanya marekebisho ya Sheria na Kanuni 14 hususan katika Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Kilimo, Ufugaji, Afya na Maliasili na Utalii ili kuboresha mazingira ya biashara. Marekebisho ya sheria hizo yamesaidia kupunguza ushuru na kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji, kukuza biashara na uchumi kwa ujumla. Aidha, Sheria ya Taifa ya Uwekezaji (1997) ilifanyiwa marekebisho na kutungwa Sheria mpya ya Uwekezaji ya Mwaka 2022 ambayo tayari imechapishwa katika Gazeti la Serikali namba 45 toleo 10 ya tarehe 02 Desemba 2022.

Katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023, imefanya marekebisho ya Sheria 13 kati ya sheria 16 zilizopendekezwa kufanyiwa maboresho. Marekebisho hayo yalilenga ama kupunguza au kuondoa kodi, ada, tozo na kupunguza au kuweka misamaha ya ushuru wa forodha. Sheria hizo ni kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.12**. Marekebisho haya yameleta matokea chanya kwenye sekta ya uwekezaji na biashara kwa kuongeza idadi ya wawekezaji na wafanyabiashara nchini kutoka miradi 256 iliyosajiliwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi kufikia miradi 293 iliyosajiliwa mwaka wa fedha 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 14.5 kwa mujibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

**Jedwali Na. 12:** Marekebisho ya Sheria mbalimbali kuhusu Kodi

| Na | Sheria | Sura |
|---|---|---|
| 1 | Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani | 148 |
| 2 | Sheria ya Kodi ya Mapato | 332 |
| 3 | Sheria ya Ushuru wa Bidhaa | 147 |
| 4 | Sheria ya Usimamizi wa Kodi | 438 |
| 5 | Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa | 290 |
| 6 | Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa 2015 | 148 |
| 7 | Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki | 306 |
| 8 | Sheria ya Uhamiaji | 54 |
| 9 | Sheria ya Ardhi | 113 |
| 10 | Sheria ya Madini | 123 |
| 11 | Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi | 82 |
| 12 | Sheria ya Michezo ya Kubahatisha | 41 |
| 13 | Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi | 196 |
| 14 | Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 | |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara, 2023*

### 2.3.2 Idadi ya Walipa Kodi

Serikali imeendeleza jitihada madhubuti ili kuhakikisha mazingira ya biashara yanaboreshwa nchini. Jitihada hizo zimepelekea mabadiliko chanya katika sekta ya biashara chini kwa kuongeza idadi ya walipa kodi. Hadi kufikia Juni 30, 2023 Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imesajili jumla ya walipa kodi **4,696,999,** sawa na asilimia **16** ya idadi ya nguvu kazi iliyopo nchini ambayo ni takribani watu milioni **33**. Walipa kodi hao watapelekea ongezeko la ajira kwa watanzania, kuboresha miundombinu mbalimbali hata kuongeza pato la Taifa ili kuelekea kwenye nchi zenye uchumi wa juu.

### 2.3.3 Kodi Kero Zilizofutwa

Serikali imefuta au kupunguza jumla ya tozo, ada na faini **100** ambazo zimekuwa ni kero katika ufanyaji biashara na uwekezaji nchini. Kati ya tozo hizo, **tozo 39** zilikuwa zikitozwa na: Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Bodi ya Sukari Tanzania (TSB), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (FFR). Aidha, jumla ya tozo **61** zilikuwa zikitozwa na na Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Ujenzi na Uchukuzi; Maliasili na Utalii; Kilimo na Mifugo na Uvuvi.

### 2.3.4 Unafuu wa Kodi kwa Wawekezaji Wakubwa

Serikali imeendelea kutekeleza utaratibu wa kuwapa wawekezaji wakubwa unafuu wa kodi ikiwa ni pamoja na kupanuliwa kwa lengo la kuwahusisha pia wananchi

ili nao wapate unafuu huo kama wawekezaji wengine. Hali halisi ya utekelezaji inaonesha katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 Serikali ilifanya maboresho ya Sheria za Kodi ili kuwianisha Sheria za Kodi na Sheria ya Uwekezaji. Aidha, Serikali ilitangaza Sheria Mpya ya Uwekezaji ya mwaka 2022 ambapo Kifungu cha 2 (2) cha Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2022 mwekezaji mzawa atapatiwa nafuu ya uwekezaji ikiwemo kupata nafuu ya kodi na kinga pale atakapowekeza mtaji wa kiasi cha Dola za Marekani 50,000.

**2.3.5 Kodi ya Uendelezaji Ujuzi**

Kodi ya Uendelezaji Ujuzi (SDL) iliendelea kuchangiwa na waajiri kwa lengo la kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu. Serikali imeendelea kupunguza kodi ya uendelezaji ujuzi kutoka **asilimia 6** na baadaye kuwa **asilimia 4** na katika kipindi cha mwaka 2022/23 imepungua na kufikia **asilimia 3.5.** Puguzo hilo lilifanywa katika marekebisho ya kwenye Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, SURA 82 katika mwaka wa fedha 2023/24 ambapo imepungua kwa **asilimia 0.5** kutoka kiwango cha tozo cha **asilimia 4** ambacho kilikuwa kinachangiwa na waajiri. Mabadiliko haya yanalenga kufanikisha utekelezaji wa mikakati ya kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu kama vilivyoainishwa na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004**.** Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali imeelekeza matumizi ya kodi ya uendelezaji ujuzi yatakuwa kwa wanufaikaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) na Wizara yenye dhamana ya Ajira.

**2.3.6 Leseni, Usajili na urasimishaji**

Serikali iliendelea kuhimiza urasimishaji ili kuwezesha biashara kutambulika na mifumo rasmi ya kisheria kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya uendeshaji biashara. Urasimishaji ambao ni uwezeshaji wananchi kiuchumi una mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa nchi na umekuwa ukifanyika kupitia sekta na taasisi mbali mbali kama vile NIDA, BRELA, TRA, TBS, TMDA, MKURABITA, GS1 Tanznia, na Halmashauri.

**(a) Usajili wa Majina ya Biashara, Kampuni na utoaji wa Leseni za Biashara na Viwanda**

Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni na Viwanda katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 umekuwa na mafanikio makubwa ikilinganishwa na mwaka 2021/2022. Jedwali hapa chini linaonesha mchanganuo wa mwenendo wa hali ya utekelezaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) Leseni za biashara za Daraja A;
(ii) Kampuni zilizosajiliwa;
(iii) Majina ya biashara yaliyosajiliwa;
(iv) Leseni za viwanda Zilizotolewa;
(v) Alama za Biashara na Huduma zilizosajiliwa; na
(vi) Hataza zilizotolewa.

Mwenendo wa takwimu unaonesha kumekuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 17 katika shughuli za sajili na utoaji leseni kwa mwaka 2021/22 ikilinganishwa na mwaka 2022/23 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.13.**

**Jedwali Na. 13:** Mwenendo wa Usajili na Utoaji Leseni

| Aina ya Huduma | 2021/2022 | | | 2022/2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi Iliyokadiriwa | Idadi Zilizotolewa | (%) Ya Utekelezaji | Idadi Iliyokadiriwa | Idadi Zilizotolewa | (%) Ya Utekelezaji |
| Usajili wa Kampuni | 11,000 | 12,583 | 114 | 13,100 | 14,701 | 112 |
| Usajili wa majina ya biashara | 19,500 | 23,780 | 122 | 25,100 | 27,212 | 108 |
| Utoaji wa Leseni za Biashara | 13,200 | 13,262 | 98 | 13,750 | 16,333 | 119 |
| Utoaji wa vyeti vya usajili wa Viwanda | 44 | 24 | 55 | 44 | 40 | 91 |
| Utoaji wa Leseni za Viwanda | 200 | 117 | 59 | 200 | 193 | 97 |
| Usajili wa Alama za Biashara na huduma | 4,120 | 3,555 | 86 | 4,120 | 3,931 | 95 |
| Maombi ya Hataza | 35 | 34 | 97 | 35 | 74 | 211 |

***Chanzo:*** *BRELA, 2023*

Mwaka 2022/23 umekuwa na mabadiliko makubwa, katika usajili na utoaji wa leseni kutokana na uboreshaji wa kiutendaji wa kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya usajili na utoaji leseni kwa njia ya mtandao, elimu kwa umma na kuongeza kaguzi elimishe za leseni za viwanda na biashara. Taratibu za urasimishaji wa biashara kwa kusajili na kutoa leseni za biashara na viwanda kwa nia ya mtandao kupitia BRELA zimewezesha kuvutia wawekezaji, na kuchochea ongezeko la ajira na ukuaji wa uchumi wa nchi kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 14**.

**Jedwali Na. 14:** Mchanganuo wa Aina ya Huduma Zilizotolewa


| Na | Aina ya Huduma | 2021/22 | 2022/23 | Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| | | Idadi Zilizotolewa | Idadi Zilizotolewa | |
| 1. | Usajili wa Kampuni | 12,583 | 14,701 | 112 |
| 2. | Usajili wa majina ya biashara | 23,780 | 27,212 | 108 |
| 3. | Utoaji wa Leseni za Biashara | 13,262 | 16,333 | 119 |
| 4. | Utoaji wa vyeti vya usajili wa Viwanda | 24 | 40 | 91 |
| 5. | Utoaji wa Leseni za Viwanda | 117 | 193 | 97 |
| 6. | Usajili wa Alama za Biashara na huduma | 3,555 | 3,931 | 95 |
| 7. | Maombi ya Hataza | 34 | 74 | 211 |

***Chanzo:*** *BRELA, 2023*

**(b) Uimarishaji wa Mifumo ya TEHAMA**

Serikali imesanifu na kutengeneza mfumo unaowezesha mifumo mbalimbali ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa kwa urahisi na usalama unaojulikana kama *Government Enterprise Service Bus (GovESB*). Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 mifumo 55 ya Taasisi 50 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa. Idadi ya taasisi za Serikali 356 zilifanikiwa kuunganishwa kwenye mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Govnet) kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na 323 kwa mwaka 2021/22. Kwa upande wa Mfumo wa Huduma za Simu za Mkononi, jumla ya taasisi 320 ziliunganishwa ikilinganishwa na taasisi 282 kwa mwaka 2021/22 kama inavyoonesha katika Mchoro Na. 4.

**Mchoro Na.4:** Taasisi Zilizounganishwa na Huduma za Mamlaka ya Serikali Mtandao




***Chanzo:*** *Mamlaka ya Serikali Mtandao, 2023*

Mfumo wa eMrejesho umeendelea kuboreshwa ikiwa ni dirisha la mawasiliano kati ya Taasisi za Umma na Wananchi ambapo Mwananchi anaweza kutuma Lalamiko, Pendekezo, Ulizo na Pongezi moja kwa moja kwenda kwenye Taasisi yoyote ya Umma. Mfumo wa Huduma za Ajira (TAESA) umejengwa na jumla ya watanzania 18,249 wanaotafuta kazi, waajiri 81 na mawakala binafisi wa kuwaunganisha watafuta kazi kwa waajiri 59 na pia mfumo huo uliwezesha kuwaunganisha watafuta kazi 1,055 nje ya Nchi. Jumla ya Taasisi za Umma na watoa huduma 973 wameunganishwa na wanatumia Mfumo wa Malipo wa Serikali Kielekroni (Government e-Payment Gateway- GePG). Mfumo wa kusimamia Ankara na rasilimali za Maji (MAJIIS) umeendelea kuboreshwa na unatumia na Wizara pamoja na Mamlaka zote 94 za Maji, pamoja na ZAWA ya Zanzibar.

### 2.3.7 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya kuboresha Mfumo na Utawala wa Kodi, Sheria, Kanuni, Leseni na Huduma za Serikali

Utekelezaji wa mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma za Serikali umewezesha mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Idadi ya walipakodi waliosajiliwa mwaka 2022/23 walikuwa **4,455,028** ambapo kati ya hao wenye TIN za biashara ni **1,641,173** na wenye TIN zisizo za biashara ni **2,813,855;**

(ii) Kuboresha mifumo ya kikodi kwa kuendelea kupunguza kiwango cha tozo ya kodi ya uendelezaji ujuzi kutoka **asilimia 4** na kufikia **asilimia 3.5** ambapo pia miaka ya 2004 waajiri walichangia **asilimia 6;**

(iii) Mfumo wa Kutoa Huduma kwa njia ya Simu za Mkononi umeboreshwa na huduma tatu zilizopo: Push SMS, PULL SMS and USSD Short Code zimeendelea kusimamiwa ipasavyo. Taasisi za umma 320 zimeunganishwa katika Mfumo wa Huduma za Simu za Mkononi na kurahisisha Utoaji wa Huduma kwa Umma. Aidha, Ofisi za Taasisi za Umma 356 zimeuganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Communication Network- GovNet);

(iv) Mamlaka iliendelea kuboresha Mfumo wa Ubadilishanaji wa Taarifa (Government Enterprise Service Bus- GovESB) na hadi kufikia Juni 2023, jumla ya Taasisi za Umma 60 zinatumia na Mifumo 77 inabadilishana Taarifa kupitia mfumo huu. Ujenzi wa Mifumo Tumizi ya Kisekta na Kitaasisi imeendelea kujengwa na kuboreshwa ambapo, jumla ya Mifumo 15 imejegwa na 21 imeboreshwa ili kurahisisha Utoaji wa Huduma kwa Umma kwa njia rahisi. Mapitio ya Usalama wa Mifumo (Security Assessment) yamefanyika kwa Taasisi 621; Viwango na Miongozo 11 ya Serikali Mtandao imeandaliwa na Taasisi 456 zimejengewa uwezo na uelewa kwenye eneo la Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao; na

(v) Mapitio kwenye Sheria mbalimbali za kodi yamefanyika yenye lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara. Serikali ilianza matumizi ya mfumo wa pamoja wa ukusanyaji wa ada, tozo na adhabu za taasisi za udhibiti (Single Window Payment System) na taasisi za udhibiti kuweka utaratibu mzuri

wa ukaguzi ambao pamoja na mambo mengine hautasababisha usumbufu kwa wafanyabiashara bila kuathiri majukumu ya msingi ya taasisi hizo.

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuboresha mfumo na utawala wa kodi, sheria, kanuni, leseni na huduma za Serikali lakini bado kuna changamoto. Changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo ni kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 15**.

**Jedwali Na. 15:** Changamoto na Mikakati ya Kuboresha Mfumo na Utawala wa Kodi, na Huduma za Serikali

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Bado baadhi ya mifumo ya kitaasisi haijauganishwa ili kuwezesha kusomana kwa mifumo hiyo* | *(i) Kuongeza utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya nchi.* |
| *(ii) Kiwango kidogo cha walipa kodi ikilinganishwa na nguvukazi iliyopo nchini* | *(ii) Kuendelea kuunganisha Mifumo ya Taasisi za Umma kwenye Mfumo wa Serikali wa kubadilishana Taarifa (Government Enterprise Service Bus-GovESB).* |
| *(iii) Uwepo wa idadi kubwa ya biashara ndogo zinazofanywa na wananchi katika mifumo isiyo rasmi.* | *(iii) Kuongeza kasi ya urasimishaji biashara na shughuli za kiuchumi ili kupanua wigo wa walipa kodi .* |
| *(iv) Elimu ndogo kwa wananchi kuhusu sheria ya kodi, viwango na elimu mbalimbali za kodi kwa wananchi* | |

## 2.4 MITAJI

Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuhakikisha benki na taasisi za fedha zinachochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kuwezesha sekta binafsi kuanzisha na kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa mitaji kwa kuimarisha na kuboresha vyanzo vya akiba. Serikali pia imeendelea kuchukua hatua za kuondoa vikwazo mbalimbali ili kuwezesha benki kukopesha kikamilifu amana zilizopo na kwa gharama nafuu, na kuweka mikakati ambayo utekelezaji wake utainua hali na hadhi ya wananchi ili wakopesheke. Serikali pia iliendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na huduma za vikundi vya fedha vya kijami na huduma za fedha.

Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti katika maeneo ya kuimarisha vyanzo vya akiba na mitaji kwa wananchi na kuhakikisha wananchi wengi wananufaika na fursa za mitaji kupitia fursa za mikopo, dhamana, ruzuku kupitia benki, taasisi za fedha, sekta binafsi, mashirika ya kimataifa, mifuko na programu za uwezeshaji pamoja na huduma za bima. Jitihada za kuhamasisha wadau mbalimbali zimeendelea kuhimizwa na Serikali ili kubuni mbinu na kujiongezea mitaji, na kuweka mikakati ya kupunguza vikwazo vya upatikanaji wa mitaji kutoka katika benki na taasisi za fedha kwa ujumla wake. Hali ya utekelezaji wa nguzo ya mitaji ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kama ilivyoainishwa katika kipengele cha 2.4.1 hadi 2.4.4.

### 2.4.1 Benki na Taasisi za Fedha


Benki na taasisi za fedha zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi kwa kukopesha fedha kwa wananchi ili kuanzisha na kuendeleza biashara na shughuli za kiuchumi. Benki na taasisi za fedha zinawezesha huduma mbalimba ikiwa ni pamoja na: kutoa mitaji kwa sekta binafsi; kupokea na kutunza amana za Serikali na taasisi za umma; na kutunza na kuendesha akaunti za Serikali au taasisi za umma husika.

#### 2.4.1.1 Umiliki wa Watanzania na Wageni wa Benki na Taasisi za Fedha

Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kuhamasisha ongezeko la umiliki wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya uchumi unamilikiwa na watanzania. **Mchoro Na. 5** linaonesha mwenendo wa umiliki ulivyokuwa kwa mwaka 2021/22 ambapo umiliki kwa watanzania wa benki na taasisi za fedha ulikuwa ni 40.7 ikilinganishwa na wageni wenye umiliki 59.3. Aidha katika mwaka 2022/23 umiliki kwa wageni ulikuwa asilimia 59.4 ikishuka kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na asilimia 40.6 ambapo ilipungua kwa asilimia 0.1 ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Aidha, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa mwongozo wa kusimamia viashiria vya hasara vinavyosabishwa na athari za mazingira kwa benki na taasisi za fedha pamoja na mwongozo wa namna ya kupima uwezo wa benki na taasisi za fedha kuhimili misukosuko mbalimbali ya biashara ikiwemo athari za UVIKO-19 ambazo zimeendelea kuathiri sekta ya mabenki na taasisi za fedha. Serikali vilevile imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na mabadiliko hayo ili kuwezesha ukuaji wa sekta ya fedha kwa maendeleo ya wananchi wa watanzania. Jedwali hapa chini linaonesha hali ya umiliki kwa wageni na watanzania katika mabenki.

**Mchoro Na. 5**: Umiliki katika Benki




***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

**2.4.1.2 Idadi ya Taasisi za Fedha Zilizosajiliwa na Kupewa Leseni**

Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2022/23 inaonesha Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutoa leseni kwa taasisi mbalimbali za kifedha. Takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2022/23 Serikali imefanikiwa kutoa leseni 44,441 kwa taasisi mbalimbali za fedha ikinganishwa na 31,318 kwa mwaka 2020/21. Ongezeko la taasisi za fedha 13,023 zilizosajiliwa limetokana na mazingira wezeshi kuendelea kuboreshwa na Serikali na kuvutia uwekezaji katika benki na taasisi za fedha ambazo zina mchango mkubwa wa upatikanaji wa mitaji na ajira kwa wananchi wa watanzania. **Jedwali Na.16** linaonesha mchanganuo na ulinganifu wa aina ya taasisi zilizosajiliwa na kupewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania.

**Jedwali Na. 16:** Idadi ya Taasisi za Fedha Zilizosajiliwa na Kupewa Leseni

| Na. | Aina ya Taasisi | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|
| 1. | Benki | 45 | 44 |
| 2. | Taasisi za Karadha | 5 | 5 |
| 3. | Taasisi zinazotoa mikopo ya nyumba (Mortgage financing) | 2 | 2 |
| 4. | Taasisi za Karadha (Financing Leasing Institutions) | 2 | 2 |
| 5. | Mifuko ya Pensheni | 4 | 4 |
| 6. | Bureau De Change | 4 | 10 |
| 7. | Tier II Microfinance | 883 | 1,307 |
| 8. | Tier III Microfinance | 692 | 810 |
| 9. | Tier Iv Microfinance | 29,682 | 42,257 |
| **Jumla** | | **31,319** | **44,441** |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

Mchango wa benki 44 umewezesha uwepo wa jumla ya matawi ya kutolea huduma 998 katika mikoa yote ya Tanzania ambayo kwa namna moja ama nyingine yamewezesha kuwafikia wateja wengi zaidi, kukuza amana za benki na kupunguza gharama za kuwafikia wateja wengi, kukuza amana za benki na kupunguza gharama za riba kutokana na ongezeko la amana zenye gharama nafuu. Benki 28 kati ya benki 44 zimeanzisha huduma za kibenki kwa njia ya uwakala. Kupitia huduma ya uwakala iliyoanzishwa imewezesha uwekaji wa amana kwa mihamala 20,431,261 yenye thamani ya shilingi bilioni 17,699.8.

**2.4.1.3 Mikopo Iliyotolewa na Marejesho katika Benki**

Serikali imeendelea kutekeleza mikakati ya kuinua hadhi ya wananchi ili wakopesheke katika benki ili kutekeleza Sera za Fedha pamoja na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliendelea kusimamia benki zote na kuhakikisha kuwa benki za kibiashara zinawezesha upatikanaji wa huduma za mikopo kwa sekta binafsi. Kwa mwaka 2022/23 kiwango cha mikopo kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, licha ya kuongezeka kwa kiwango cha mikopo kinachotolewa lakini kiwango cha urejeshaji kimeendelea kuwa chini kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.17**.

**Jedwali Na.17:** Mikopo Iliyotolewa na Benki na Hali ya Marejesho

| Mwaka | Mikopo Iliyotolewa | Marejesho |
|---|---|---|
| 2022/23 | 13,272,901,117,476.30 | 9,593,742,578,808.97 |
| 2021/22 | 12,225,443,956,813.20 | 10,519,984,012,805.10 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

**2.4.1.4 Riba za Benki na Mikopo ya Kuinua Hadhi ya Wananchi Kukopesheka**

Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuimarisha viwango vya riba kama mkakati endelevu wa kuinua hadhi ya wananchi kukopesheka katika mabenki na taasisi za fedha. Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni agenda endelevu ya Serikali inayohimiza kushusha viwango vya riba ili kuongeza wigo mpana kwa wananchi wakopaji. Takwimu za Benki Kuu ya Tanzania zinaonesha kuwa, katika mwaka 2022/23 wastani wa viwango vya riba katika soko la fedha baina ya benki ulikuwa asilimia 4.5 kwa mwaka ikilinganishwa na riba ya asilimia 4.4 kwa mwaka 2021/22.

Aidha, viwango vya riba katika soko la fedha baina ya benki uliendelea kuwa chini na tulivu kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha uliowezesha kuwa na kiwango cha ukwasi kinachoendana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Viwango vya riba za mikopo viliendelea kupungua japo kwa kiwango kidogo ambapo wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 16.18 ikilinganishwa na asilimia 16.59 kwa mwaka 2021/22.

Mwenendo huu ulitokana na hatua za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuchochea ongezeko la ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Hatua hizo

ziliwezesha baadhi ya benki kutoa mikopo kwenye sekta ya kilimo kwa riba ya chini ya asilimia 10. **Jedwali Na.18** linaonesha mwenendo wa viwango vya riba za benki na riba za mikopo kwa vipindi tofauti hadi kufikia mwaka 2022/23.

**Jedwali Na. 18:** Viwango vya Riba za Benki na Riba za Mikopo

| Mwaka | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| Riba ya mikopo ya Benki | 5.13 | 4.5 | 4.4 | 4.5 |
| Riba ya mikopo ya Wananchi | 16.97 | 16.66 | 16.59 | 16.18 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

### 2.4.1.5 Matumizi ya Huduma za Fedha

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, matumizi ya huduma za fedha kwa wanaopata huduma za kibenki yaliongezeka hadi kufikia asilimia 22.2 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na asilimia 16.7 kwa mwaka 2017/18 na asilimia 14 kwa mwaka 2013/14. Matumizi kwa wananchi ambao hawapati huduma za benki lakini wanatumia huduma rasmi za fedha iliongezeka na kufikia asilimia 53.5 kwa mwaka 2022/23 na kwa mwaka 2017/18 ilikuwa ni asilimia 48.6 zaidi ya asilimia 43 ilikuwa mwaka 2013/14. Aidha, tathmini inaonesha kuwa wananchi ambao hawapati huduma za benki lakini wanatumia huduma za fedha zisizo rasmi ilipungua hadi kufikia asilimia 5.7 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na asilimia 6.7 kwa mwaka 2017/18 na asilimia 16 kwa mwaka 2013/14. **Jedwali Na.19** linaonesha wananchi ambao hawatumii huduma za fedha nayo ilizidi kushuka kutoka asilimia 27 kwa mwaka 2013/14 ikilinganishwa na asilimia 18.7 kwa mwaka 2022/23 na pia iliongezeka mwaka 2017/18 na kufika asilimia 28. Matokeo ya kupiungua kwa wananchi ambao hawatumii huduma za fedha unatokana na uendelevu wa Serikali kuhimiza wananchi kuweka akiba, na kuongeza matumizi ya huduma za fedha katika mifumo ili rasmi.

**Jedwali Na.19:** Hali ya Matumizi ya Huduma za Fedha

| Na. | Matumizi ya Huduma za Fedha | 2013 | 2017 | 2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wanapata huduma za kibenki | 14 | 16.7 | 22.2 |
| 2. | Hawapati huduma za benki lakini wanatumia huduma rasmi za fedha | 43 | 48.6 | 53.5 |
| 3. | Hawapati huduma za benki lakini wanatumia huduma za fedha zisizo rasmi | 16 | 6.7 | 5.7 |
| 4. | Hawatumii huduma za fedha | 27 | 28 | 18.7 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

### 2.4.1.6 Kanzidata ya Taarifa za Wakopaji

Serikali imeendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Kanzidata ya Taarifa za Wakopaji (Credit Reference Bureau) ambapo idadi ya taasisi na wakopaji wanaoorodheshwa katika kanzidata imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo hadi Juni, 2023 jumla ya taasisi 166 zimejisajili na zinazotumia kanzidata ya taarifa za wakopaji nchini. Matumizi ya kazidata hiyo imewezesha usajili wa

wakopaji 5,035,031waliopata huduma katika taasisi 166 zilizojisajili kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na idadi ya wakopaji 4,215,210 waliosajiliwa kwa mwaka 2021/22 **(Jedwali Na.20).** Katika kuhakikisha kuwa taasisi za fedha zinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kuwezesha upatikanaji wa mitaji, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa nyaraka mbalimbali ikiwemo waraka kwa taasisi zinazokidhi masharti ya kupata nafuu ya riba; waraka unaoelekeza watoa huduma ndogo za fedha kujisajili na kanzidata ya ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za walipa kodi na waraka unaohusu utekelezaji wa makubaliano ya pili na tatu kuhusu usimamizi wa benki na taasisi za fedha.

**Jedwali Na.20:** Idadi ya Taasisi na Wakopoaji Waliosajiliwa katika Kazidata ya Wakopaji

| Mwaka | Idadi ya Taasisi Zilizosajiliwa | Idadi ya Wakopaji Waliosajiliwa |
|---|---|---|
| 2022/23 | 166 | 5,035,031 |
| 2021/22 | 155 | 4,215,210 |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

### 2.4.1.7 Ajira za Watanzania na Wageni katika Benki

Serikali imeendelea kukuza ajira za watanzania katika benki na taasisi za fedha. Kulingana na taarifa za Benki Kuu ya Tanzania inaonesha kuna jumla ya ajira 18,071 katika benki kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na ajira 17,528 kwa mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la ajira 543. Takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka 2022/23 wanaume walioajiriwa katika benki ni 9,582 sawa na asilimia 53 ikilinganishwa na ajira za wanawake 8,489sawa na asilimia 47. Kwa mwaka 2022/23, ajira za watanzania katika benki zilikuwa ni 18,023 sawa na asilimia 99.7 ambapo wanaume ni 9,539 na wanawake ni 8,484 ikilinganishwa na ajira za wageni 48 sawa na asilimia 0.3 ambapo wanaume walikuwa ni 43 na wanawake 5. Ajira za wageni ziliendelea kupungua kutoka ajira 51 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia ajira 48 kwa mwaka 2022/23 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 21**.

**Jedwali Na. 21:** Ajira za Watanzania na Wageni katika Benki

| Ajira | 2021/22 | | | 2022/23 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Watanzania | 9,252 | 8,225 | 17,477 | 9,539 | 8,484 | 18,023 |
| Wageni | 46 | 5 | 51 | 43 | 5 | 48 |
| **Jumla** | **9,298** | **8,230** | **17,528** | **9,582** | **8,489** | **18,071** |

***Chanzo:*** *Benki Kuu ya Tanzania, 2023*

## 2.4.2 Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Serikali ilianzisha Mifuko na Programu za uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kupanua wigo wa utoaji huduma za uwezeshaji ikiwa ni pamoja na huduma za kifedha ili kuwawezesha wananchi washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi

wa nchi. Mifuko na programu hizo zimejikita katika kutatua changamoto zinazozuia wananchi kukopesheka kwa kuwepo kwa vikwazo ikiwemo: gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo, ukosefu wa utambulisho rasmi, kutokuwa na taarifa muhimu za waombaji mikopo, ukosefu wa dhamana, ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, na ukosefu wa mitaji ya kuchangia uanzishaji wa miradi nk. Walengwa wakuu wa mifuko na program za uwezeshaji ni wananchi wa Tanzania wanaofanya shughuli za kiuchumi katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kilimo, mifugo, maliasili na utalii, afya, ardhi, viwanda na biashara, ujenzi, mawasiliano na uchukuzi, nishati, na elimu.

Mifuko na programu za uwezeshaji imegawanyika katika makundi manne kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji na walengwa. Kuna jumla ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi 72 hadi kufikia Juni, 2023 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 22** na **Kiambatishao Na.1**. Mifuko na programu hizo zimegawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni Mifuko inayotoa mikopo, Mifuko inayotoa dhamana kwa kushirikiana na taasisi za fedha, Mifuko inayotoa ruzuku na Programu za Uwezeshaji. Kati ya mifuko na programu hizo, mifuko na programu 63 zinamilikiwa na Serikali na mifuko na programu 9 zinamilikiwa na Sekta binafsi.

**Jedwali Na.22:** Idadi ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji

| Na. | Kundi la Mfuko | Aina Ya Umiliki | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Serikali | Binafsi | |
| 1 | Mifuko inayotoa mikopo Moja kwa Moja | 20 | 1 | 21 |
| 2 | Mifuko inayotoa Dhamana | 7 | 3 | 10 |
| 3 | Mifuko inayotoa Ruzuku | 26 | 2 | 28 |
| 4 | Programu za uwezeshaji | 10 | 3 | 13 |
| **Jumla** | | **63** | **9** | **72** |
| **Asilimia (%)** | | **87.5** | **12.5** | **100** |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

### 2.4.2.1 Mikopo Iliyotolewa na Mifuko na Programu za Uwezeshaji

Katika kipindi cha mwaka 2022/ 23, mifuko na programu za uwezeshaji ilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 743.7 kwa wanufaika wapatao 6,064,957 ambapo miongoni mwao wanaume ni 2,776,771 sawa na asilimia 46 na wanawake 3,288,186 sawa na asilimia 54. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, mifuko na programu za uwezeshaji inayotoa mikopo moja kwa moja na inayotoa dhamana imekopesha shilingi bilioni 430.5 kwa wanufaika 932,442 ambapo wanaume ni 498,912 na wanawake ni 433,530. Kiasi cha shilingi bilioni 313.2 kilitolewa na mifuko inayotoa ruzuku kwa wanufaika wapatao 5,132,515 ambapo wanaume ni 2,277,859 sawa na asilimia 44, wanawake ni 2,854,656 sawa na asilimia 56. Fedha hizo zilizotolewa zimewezesha kuzalisha ajira za moja kwa moja na zizizo za moja kwa moja zipatazo 7,764,975 ambapo ajira za wanawake zilikuwa 4,208,616 sawa na asilimia 54 na wanaume zilikuwa 3,556,359 sawa na asilimia 46. Kutokana na

uchambuzi uliofanyika, imebainika kuwa katika mwaka 2022/23 kuna ongezeko la asilimia 4 kwa fedha zilizotolewa na mifuko na programu za uwezeshaji kwa shilingi bilioni 743.7 ikilinganishwa na mwaka 2021/22 ambapo kiasi cha shilingi 713.8 kilitolewa.

Tathmini ya utekelezaji wa mifuko na programu za uwezeshaji inaonesha kuwa, sekta ya kilimo na ufugaji ndiyo imenufaika zaidi na fedha hizo kwa asilimia 45 ikifuatiwa na sekta ya viwanda na biashara kwa asilimia 15. Sekta ya Afya ndiyo imenufaika kwa kiwango kidogo zaidi kwa asilimia 2.5 ikilinganishwa na sekta nyingine kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.23**.

**Jedwali Na. 23:** Mikopo na Ruzuku Iliyotolewa kutoka Mifuko na Programu za Uwezeshaji Kisekta

| Na. | Sekta Zilizonufaika | Thamani ya Fedha Iliyotolewa | % ya Mikopo Iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1. | Elimu | 87,683,998,000.00 | 11.80 |
| 2. | Afya | 19,776,201,000.00 | 2.50 |
| 3. | Madini | 54,564,450,000.00 | 7.30 |
| 4. | Kilimo, Mifugo na Uvuvi | 339,875,130,000.00 | 45.70 |
| 5. | Utalii | 67,176,945,000.00 | 9.00 |
| 6. | Viwanda na Biashara | 112,211,356,000.00 | 15.00 |
| 7. | Nishati | 43,512,600,000.00 | 5.80 |
| 8. | Nyinginezo | 18,859,948,119.63 | 2.90 |
| **Jumla** | | **743,660,628,119.63** | **100.00** |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

Katika mwaka wa fedha 2022/23, tathmini inaonesha kuwa mikoa ambayo ilinufaika kwa kiwango kikubwa zaidi ilikuwa ni mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma, Tanga na Kagera. Aidha, mikoa iliyonufaika kwa kiwango kidogo zaidi ilikuwa ni mkoa wa Njombe na Katavi kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.24.**

**Jedwali Na. 24**: Mikopo kutoka katika Mifuko ya Uwezeshaji Kimkoa

| Na. | Mikoa | Thamani ya Mikopo Iliyotolewa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1 | Arusha | 32,814,901,027.05 |
| 2 | Dar Es Salaam | 58,669,503,369.07 |
| 3 | Dodoma | 33,152,223,805.63 |
| 4 | Geita | 27,283,003,436.89 |
| 5 | Iringa | 23,118,987,728.04 |
| 6 | Kagera | 32,127,675,912.64 |
| 7 | Katavi | 18,682,800,478.04 |
| 8 | Kigoma | 31,192,641,294.04 |

| Na. | Mikoa | Thamani ya Mikopo Iliyotolewa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 9 | Kilimanjaro | 24,060,784,471.04 |
| 10 | Lindi | 24,767,454,027.70 |
| 11 | Manyara | 26,224,017,756.04 |
| 12 | Mara | 26,301,825,824.04 |
| 13 | Mbeya | 26,687,855,209.79 |
| 14 | Morogoro | 28,088,234,390.84 |
| 15 | Mtwara | 29,293,215,864.27 |
| 16 | Mwanza | 34,753,900,409.04 |
| 17 | Njombe | 19,475,165,925.04 |
| 18 | Pwani | 24,339,618,704.39 |
| 19 | Rukwa | 24,845,143,309.04 |
| 20 | Ruvuma | 32,925,722,845.07 |
| 21 | Shinyanga | 28,115,663,958.04 |
| 22 | Songwe | 20,378,021,675.04 |
| 23 | Simiyu | 26,253,952,008.04 |
| 24 | Singida | 29,492,250,330.29 |
| 25 | Tabora | 27,729,878,796.04 |
| 26 | Tanga | 32,886,185,564.48 |
| **Jumla (Tshs)** | | **743,660,628,119.63** |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

### 2.4.2.2 Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na Vya Kati (SANVN Viwanda Scheme)

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuratibu utekelezaji Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya kati (SANVN Viwanda Scheme). Programu hii inalenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa ujuzi, masoko, teknolojia na mitaji katika miradi ya viwanda vidogo na vya kati katika eneo la kuongeza mnyororo wa thamani wa kuchakata mazao ya kilimo. Mpango wa SANVN unatoa mikopo ya kuanzia shilingi Milioni 8 hadi Milioni 50 kwa miradi midogo na shs Milioni 51 hadi Milioni 500 kwa miradi ya kati. Mikopo hii imegawanyika katika makundi mawili ambayo ni mikopo ya uwekezaji (Investments loan) na mikopo ya uendeshaji wa miradi (Working Capital loan).

Kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Juni, 2023 jumla ya maombi 20 yenye thamani ya Shilingi **trilioni 1.78** yalipokelewa ambapo kati ya maombi hayo, maombi 10 yalitoka kwenye Kampuni, 9 kutoka kwa watu binafsi na 1 kutoka kwa kikundi. Baada ya uchambuzi wa kina wa maombi hayo, viwanda 15 vilikidhi vigezo na kufanikiwa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi **bilioni 1.38** sawa na **77.75 %** ya maombi yaliyopokelewa. Mikoa iliyonufaika na mikopo hiyo

ni Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya na Mwanza kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 25**.

**Jedwali Na. 25:** Mikoa Iliyonufaika na Mikopo ya SANVN Viwanda Scheme

| Na. | Mkoa | 2021/22 | | 2022/23 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Fedha Zilizotolewa | Idadi ya Viwanda | Fedha Zilizotolewa | Idadi ya Viwanda |
| 1 | Arusha | 378,000,000 | 9 | 1,076,339,256 | 8 |
| 2 | Dar Es Salaam | 36,250,000 | 2 | 192,000,000 | 3 |
| 3 | Dodoma | 20,000,000 | 1 | | |
| 4 | Geita | 35,000,000 | 2 | | |
| 5 | Iringa | | | 15,000,000 | 1 |
| 6 | Kilimanjaro | 182,847,651 | 2 | | |
| 7 | Mbeya | 418,000,000 | 9 | 5,000,000 | 1 |
| 8 | Mwanza | 132,000,000 | 3 | 95,000,000 | |
| 9 | Shinyanga | 70,000,000 | 1 | | |
| 10 | Songwe | 15,000,000 | 1 | | |
| | **Jumla** | **1,287,097,651** | **30** | **1,383,339,256** | **13** |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

Mpango wa SANVN Viwanda Scheme umekuwa na mafanikio chanya tangu uanzishwe mwaka 2020 ambapo hadi kufikia Juni, 2023 umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni **4.4** kwa miradi midogo na ya kati 65 katika mikoa 14 ambayo ni Mwanza (11), Arusha (22), Dar Es Salaam (7), Kilimanjaro (3), Mbeya (6), Geita (3), Songwe (1), Dodoma (2), Shinyanga (1), Iringa (4), Njombe (2), Singida (1), Pwani (1) na Rukwa (1)**.** Kutokana na utekelezaji wa Mpango huo, katika kipindi hicho jumla ya ajira **9,983** zimetengenezwa ambapo ajira za moja kwa moja ni **1,995 na** ajira zisizo za moja kwa moja ni **7,988.** Mpango umefanikisha viwanda vidogo na vya kati **62** pamoja na wafanyakazi kujiandikisha katika mfuko wa Hifadhi za Jamii (NSSF).

### 2.4.3 Huduma za Bima

Huduma za bima zina mchango mkubwa katika kukuza shughuli za kiuchumi na kuwezesha wananchi kufanya shughuli z akiuchumi kw autulivu. Huduma za bima zinatoa mchango mkubwa wakati majanga mbalimbali yanapotokea ikiwemo mafuriko, moto, wizi, kuharibika mali na ugonjwa.

#### 2.4.3.1 Leseni za Huduma za Bima Zilizotolewa

Serikali imeendelea kutekeleza Sheria ya Bima ya mwaka 2009 kwa lengo la kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa za bima nchini ambapo katika mwaka 2022/23, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima imetoa leseni 1,251 zikijumuisha Kampuni za bima 34, Mawakala wa Bima 960, madali wa bima 107, Mawakala

wa Benkibima 26, Watathmini na Wakadiriaji Hasara 27, Kampuni za Takwimu za Bima 2, Wachunguzi wa Bima 4, Wakadiriaji 13, Bima mtawanyo zenye idhibati 27, Ushauri na Udalali zenye idhibati 35, Bima Mtawanyo za Ndani 0, Kampuni za Bima mtawanyo 3, na Washauri na Madalali wa Bima Mtawanyo 8. Aidha, makampuni ya bima yaliongezeka na kufikia 34 kwa mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na 32 yaliyosajiliwa mwaka 2021/2022. Madalali wa bima waliongezeka kutoka 81 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia kampuni 107 kwa mwaka 2022/23.

Ongezeko la kampuni hizo zilitokana na jitihada za Serikali kupitia TIRA katika kuongeza kampuni za bima na kuwepo kwa sheria ya bima na usimamizi madhubuti. Serikali imefanya ukaguzi kwa watoa huduma za bima ikiwa ni pamoja na: kampuni za bima 18, matawi ya kampuni za bima 18, madalali wa bima 8; benki wakala 8 na mawakala wa bima 68; na kufanya ukaguzi wa bima kwa vyombo vya moto 33,160,000. Aidha, malalamiko 284 ya bima yamepokelewa na yalishughulikiwa ambapo malalamiko 68 yalipatiwa ufumbuzi na kulipwa, malalamiko 22 yalikataliwa, 11 yalipelekwa mahakamani, 18 yalipelekwa kwa Msuluhishi wa Migogoro ya Bima na 135 bado yanaendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi. **Jedwali Na.26** linaonesha mgawanyo wa idadi ya watoahuduma za Bima waliosajiliwa mwaka 2022/2023.

**Jedwali Na. 26:** Mgawanyo wa Idadi ya Watoahuduma za Bima Waliosajiliwa

| Na. | Aina ya kampuni | Idadi |
|---|---|---|
| 1. | Kampuni za Bima | 34 |
| 2. | Washauri na Madalali wa Bima | 114 |
| 3. | Mawakala wa Bima | 960 |
| 4. | Mawakala wa Benkibima | 26 |
| 5. | Watathmini na Wakadiriaji Hasara | 27 |
| 6. | Kampuni za Takwimu za Bima | 2 |
| 7. | Wachunguzi wa Bima | 4 |
| 8. | Wakadiriaji | 13 |
| 9. | Bima mtawanyo zenye idhibati | 27 |
| 10. | Ushauri na Udalali zenye idhibati | 35 |
| 11. | Bima Mtawanyo za Ndani | 0 |
| 12. | Kampuni za Bima mtawanyo | 3 |
| 13. | Washauri na Madalali wa Bima Mtawanyo | 7 |
| | **Jumla** | **1,252** |

***Chanzo:*** *TIRA, 2023*

### 2.4.3.2 Vituo vya Utoaji Huduma vilivyosajiliwa na Bima

Huduma za bima ya afya zimeendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko wa Bima ya Afya vimefikia 9,178 kwa ngazi tofauti za utoaji huduma kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.27**.

**Jedwali Na. 27:**Idadi ya Vituo Vilivyosajiliwa na Mfuko

| Ngazi ya kituo | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|
| Zahanati | 5,401 | 5,753 | 6,485 | 6,252 | 6,582 |
| Vituo vya afya | 713 | 766 | 853 | 832 | 912 |
| Maduka ya dawa | 349 | 449 | 597 | 560 | 685 |
| Hospitali | 286 | 298 | 346 | 381 | 417 |
| Cliniki maalum | 73 | 130 | 211 | 265 | 360 |
| Maduka ya dawa muhimu | 202 | 200 | 461 | 179 | 207 |
| Vituo vya uchunguzi | 6 | 9 | 16 | 13 | 14 |
| Vituo vya uokozi | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **Jumla** | **7,031** | **7,606** | **8,970** | **8,483** | **9,178** |

***Chanzo:*** *NHIF*

### 2.4.4 Vitambulisho vya Taifa

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya Mwaka 2004, ilielekeza kuanzishwa kwa utaratibu wa kutoa vitambulisho kwa raia wote nchini kwa nia ya kusaidia kupunguza gharama za benki kutafuta taarifa muhimu za wakopaji. Utaratibu wa utoaji wa vitambulisho vya Taifa pamoja na malengo mengine pia unalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wakopaji na kupunguza gharama za benki kuwatafuta wateja wake wakati wa kufanya marejesho. Katika kufikia malengo hayo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeendelea kusajili na kuwatambua wananchi wanaoishi nchini waliofikia umri wa miaka 18 na kuendelea. Katika kipindi cha mwaka 2022/ 23 jumla ya wananchi **762,046** wamesajiliwa na kufikia jumla ya wananchi **23,965,371** waliosajiliwa na kutambuliwa tangu kuanza kwa usajili huo mwaka 2012.

Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 namba za Utambulisho 739,863 zimezalishwa hivyo kufanya jumla ya NIN 20,222,032 zilizozalishwa tangu mwaka 2012. Aidha, vitambulisho 1,849,941 vimezalishwa katika kipindi cha mwaka 2022/23 na kufanya jumla ya vitambulisho 12,863,269 vilivyozalishwa tangu mwaka 2012. Vitambulisho 781,118 vimesambazwa na kugawiwa kwa wananchi na hivyo kufanya jumla ya vitambulisho 10,905,273 vilivyosambazwa na kugawiwa kwa wananchi tangu mwaka 2012 **(Jedwali Na.28).**

**Jedwali Na. 28:** Hali ya Uzalishaji wa Vitambulisho

| Aina | 2022/23 | 2012/13 – 2022/23 |
|---|---|---|
| Wananchi Waliosajiliwa na Kutambuliwa | **762,046** | **23,965,371** |
| Namba za Utambulisho zilizozalishwa | **739,863** | **20,222,032** |
| Vitambulisho vilivyozalishwa | **1,849,941** | **12,863,269** |
| Vitambulisho vimesambazwa na kugawiwa kwa wananchi | **781,118** | **10,905,273** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, 2023*

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali imeunganisha mfumo wa NIDA kutoa taarifa na mifumo ya kupokea taarifa ya Taasisi **8** ili kuwezesha Taasisi hizo kupata taarifa za wateja wao zilizopo NIDA. Kuunganishwa kwa mifumo hiyo, kunafanya jumla ya mifumo ya Taasisi iliyounganishwa na mfumo wa NIDA kufikia **75** (**34** ni Taasisi za umma na **41** ni Taasisi binafsi) hivyo kuwezesha uhakiki wa taarifa za watu wanaopatiwa huduma katika taasisi hizo na kupunguza/kuondoa udanganyifu wa taarifa zinazotolewa na wateja hususan kwa Taasisi zinazotoa huduma za kifedha zikiwemo Benki na hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wakopaji na kuwezesha ufuatiliaji na hivyo kupungua kwa vihatarishi wa mikopo (risk premium) na hivyo kupunguzwa kwa viwango vya riba.

### 2.4.5 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kukuza Mitaji

Katika kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wananchi ikiwa na huduma za mikopo, ruzuku na bima, mafanikio mbalimbali yamepatikana kwa mwaka 2022/23 ikiwa ni pamoja na:-

(a) Ajira za benki ziliongezeka na kufikia 18,071 mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na ajira 17,528 kwa mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la ajira mpya 543;

(b) Mifuko na programu za uwezeshaji ilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani jumla ya shilingi bilioni 743.7 kwa wanufaika 6,064,957 ambapo miongoni mwao wanaume ni 2,776,771 (46%) na wanawake 3,288,186 (54%);

(c) Viwanda 15 vilikidhi vigezo na kufanikiwa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.38 katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya na Mwanza. Aidha, Jumla ya Ajira 3,421 zimetengenezwa ambapo ajira za moja kwa moja ni 726 na ajira zisizo za moja kwa moja ni 2,695; na

(d) Kupungua kwa mikopo chechefu kutoka asilimia 7.8 Juni 2022 hadi asimia 5.3 Juni 2023.

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa wananchi hasa maeneo ya vijijini, lakini bado kuna changamoto. Changamoto na mikakati ya kutatua changamoto hizo ni kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 29.**

**Jedwali Na. 29:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Upatikanaji wa Mitaji

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Kuwepo kwa mikopo chechefu.*<br><br>*(ii) Ukosefu wa dhamana kwa baadhi ya wananchi na kushindwa kukopesheka.*<br><br>*(iii) Kutokuwepo kwa taasisi ya wakala wa dhamana Tanzania (Tanzania Credit Guarantee Agency) ili kusaidia katika upatikanaji wa mitaji kwa wananchi.* | *(i) Elimu ya mikopo inapaswa kuendelea kutolewa ili kuwezesha wananchi kunufaika na fursa rasmi za mifumo ya fedha na kuwezesha kufanya marejesho.*<br><br>*(ii) Kuongeza kasi ya upimaji ardhi kwa lengo la kuwezesha wananchi kuwa na hati ili kuwezesha wigo mpana kwa wakopaji ambao ni wananchi.*<br><br>*(iii) Kuanzisha Taasisi ya Wakala wa Dhamana Tanzania (Tanzania Credit Guarantee Agency) kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata mitaji na dhamana kwa ajili ya miradi wanayoanzisha wao wenyewe au ile ya ubia na wageni.* |

## 2.5 KUINUA VIWANGO VYA UJUZI NA UZOEFU

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi inasisitiza umuhimu wa kuinua kiwango cha ujuzi na uzoefu ili kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Kiwango cha elimu kinachangia kukuza ujuzi kwa wananchi na upeo wa maendeleo. Katika mwaka 2022/23, Serikali imeendelea kuboresha mfumo wa elimu kujenga ujuzi kwa wananchi kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi na kuwa na uchumi endelevu. Mfumo wa elimu na mafunzo unawezesha ujuzi kulingana na mahitaji ya ushindani katika soko la ndani na kimataifa.

### 2.5.1 Uanzishwaji wa Taasisi mbalimbali za Elimu

Serikali katika kuhakikisha kuwa ujuzi unaandaliwa na kuendelezwa, ilianzisha na kusimamia taasisi mbalimbali za elimu nchini kuanzia ngazi ya awali hadi chuo kikuu. Serikali, pia imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuanzisha taasisi za elimu ili kuchangia uendelezaji wa ujuzi na uzoefu kwa wananchi. **Jedwali Na.30** linaonesha mchanganuo wa taasisi mbalimbali za elimu zilizoanzishwa kwa vipindi tofauti na Serikali au sekta binafsi. Taasisi hizo zimewezesha usajili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu kwa kuwajengea maarifa na ujuzi wa kuweza kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi.

**Jedwali Na. 30:** Uanzishaji wa Taasisi za Elimu

| Ngazi ya Elimu | 2021/22 | | | 2022/23 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Serikali | Sekta Binafsi | Jumla | Serikali | Sekta Binafsi | Jumla |
| Elimu ya Awali | 16,602 | 1,952 | 18,554 | 17,130 | 2,154 | 19,284 |
| Elimu ya Msingi | 16,656 | 1,890 | 18,546 | 17,405 | 2,268 | 19,673 |
| Elimu ya Sekondari | 4,002 | 1,287 | 5,289 | 4,211 | 1,329 | 5,540 |
| Vyuo vya Ufundi Stadi | 123 | 703 | 826 | 125 | 705 | 830 |
| Vyuo vya Kati | 178 | 251 | 429 | 180 | 285 | 465 |
| Vyuo Vikuu | 21 | 31 | 52 | 21 | 31 | 52 |
| **Jumla** | **37,582** | **6,114** | **43,696** | **39,072** | **6,772** | **45,844** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

### 2.5.2 Uendelezaji Elimu ya Awali

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuboresha na kusimamia utekelezaji wa mitaala mbalimbali inayolenga kuwaandaa watanzania na kuhamasisha utoaji wa mafunzo yanayoendana na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi. Serikali pamoja na sekta binafsi zimeendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwenye ngazi ya elimu ya awali kwa ajili ya kuwaandaa watoto wa kitanzania kupata elimu itakayowezesha upatikanaji wa ujuzi na maarifa mbalimbali.

Takwimu zinaonesha kuwa, kuna shule za awali 19,284 ambapo shule 17,130 zinamilikiwa na Serikali na shule 2,154 ni za sekta binafsi. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, shule za awali zimeweza kusajili jumla ya wananfunzi 1,543,843 ambapo wasichana ni 759,005 na wanaume ni 784,838. Kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 1,435,735 walisajiliwa na Shule za Serikali ambapo wasichana ni 706,261 na wavulana ni 729,474. Katika kuwezesha upatikanaji wa elimu bora shule za awali za Serikali zimeajiri jumla ya walimu 10,093 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanafunzi ambapo kati yao, walimu 6,867 ni wanawake na 3,226 ni wanaume.

### 2.5.3 Elimu Msingi

Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuhakikisha kuwa watanzania wote wanapata elimu ya msingi ili kuweza kupata maarifa ya msingi kwa ajili ya kupata ujuzi na maarifa kwa kujenga shule, kuajiri walimu na kununua vifaa vya kufundishia. Aidha, sekta binafsi pia imeendelea kushiriki katika kuhakikisha kuwa jamii ya watanzania inaelimika kuendana na mahitaji ya soko la elimu. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, kulikuwa na jumla shule za msingi 19,673 ambapo shule 17,405 zinamilikiwa na Serikali na shule 2,268 ni uwekezaji wa sekta binafsi. Uwekezaji huu umewezesha upatikanaji wa ujuzi unaohitajika kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali na uwekezaji katika shughuli za kiuchumi. Idadi ya wanafunzi katika shule za elimu ya msingi ilikuwa 11,420,973 ambapo kati yao, wasichana walikuwa 5,783,977 na wavulana 5,636,996.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali ilikuwa 10,872,508 (wasichana 5,509,054 na wavulana 5,363,454) ikilinganishwa na wanafunzi 10,687,593 (wasichana 5,384,325 na wavulana 5,303,268) mwaka 2021/22. Ongezeko hlii lilitokana na kuendelea kuimarika kwa mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwemo utekelezaji wa Programu ya Elimu Msingi bila ada pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya elimu kupitia fedha za Mpango wa Mapambano dhidi ya Uviko19. Aidha, Idadi ya wanafunzi katika shule binafsi ilikuwa 548,465 (wasichana 274,923 na wavulana 273,542) mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wanafunzi 509,195 (wasichana 254,756 na wavulana 254,439) mwaka 2021/22. Mwaka 2022/23, watahiniwa 1,350,881 (wasichana 709,556 na wavulana 641,325) walifanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba. Kati ya hao, watahiniwa 1,073,402 (wasichana 558,825 na wavulana 514,577) walifaulu, sawa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 79.5.

Katika kuimarisha ujuzi na maarifa kwa wananchi, hadi kufikia Juni, 2023 idadi ya walimu katika shule za msingi za Serikali ilifikia 173,276 (wanawake 86,166 na wanaume 87,110) ambapo uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi ulikuwa 1:63. Uwiano huo ulizidi kiwango halisi cha uwiano wa 1:45 unaokubalika kitaifa na hivyo kuhitaji jitihada zaidi za kuajiri walimu wapya ili kuendana na mahitaji. **Jedwali Na.31** linaonesha mwenendo wa idadi ya shule, wananfunzi na walimu kwa kipindi cha miaka mitano. Upungufu wa walimu, katika kipindi cha 2020/21 kulichangiwa sababu mbalimbali ikwemo baadhi ya walimu kuvutiwa na taaluma nyingine, kustaafu, kuachishwa kazi na vifo.

**Jedwali Na. 31:** Idadi ya Shule, Wanafunzi na Walimu katika Shule za Msingi

| Mwaka | Idadi ya Shule | Idadi ya Wanafunzi | Idadi ya Walimu |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 19,673 | 11,420,973 | 173,276 |
| 2021/22 | 19,424 | 11,196,788 | 171,993 |
| 2020/21 | 18,152 | 10,925,896 | 170,569 |
| 2019/20 | 17,804 | 10,605,430 | 174,806 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia*

### 2.5.4 Elimu ya Sekondari

Katika kuendeleza elimu katika ngazi ya elimu ya sekondari, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na masomo kwa ngazi ya Sekondari. Jitihada hizo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa shule, maboma, kuongeza madawati, ununuzi wa vitabu na kuajiri walimu. Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya shule za Sekondari kutoka shule 5,831 mwaka wa fedha 2021/22 hadi shule za sekondari 6,037 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kati shule hizo, shule 4,492 zinamilikiwa na Serikali na shule 1,545 ni za sekta binafsi. Ongezeko hilo lilitokana na hatua za Serikali za kuanzisha shule za sekondari ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita ilikuwa 2,823,588 ikilinganishwa na wanafunzi 2,671,927 mwaka 2021/23, sawa na ongezeko la asilimia 5.7. Kati yao, wasichana walikuwa 1,476,369 (asilimia 52.3) na wavulana 1,347,219. Idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za Serikali ilikuwa 2,529,699 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wanafunzi 2,379,945 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne ilikuwa 2,645,115. Kati ya hao, wanafunzi katika shule za Serikali (I – IV) walikuwa 2,387,525 ikilinganishwa na wanafunzi 2,256,489 mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Ongezeko hilo lilitokana na idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitimu darasa la saba na kujiunga na kidato cha kwanza.

### 2.5.5 Elimu ya Ufundi na Mafunzo

Serikali imeendelea kuimarisha mafunzo ya ufundi katika vyuo vya kati kwenye sekta mbalimbali ambapo Vyuo hivyo vimekuwa vikitoa fursa za mafunzo ya ufundi kwa vijana mbalimbali waliohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23, kulikuwa na jumla ya vyuo vya mafunzo ya ufundi 459. Vyuo hivyo vimewezesha upatikanaji wa mafunzo ya ufundi katika fani mbalimbali kwa wanafunzi 185,818 ikilinganishwa na wanafunzi 157,420 mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la asilimia 18.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya elimu ya ufundi katika soko la ajira. Kati ya wanafunzi hao, wanawake walikuwa 90,787 (asilimia 48.9) na wanaume walikuwa 95,031. Aidha, kuna jumla ya vyuo vya ufundi stadi 830 ambapo vyuo 125 vinamilikiwa na Serikali na vyuo 705 ni uwekezaji wa sekta binafsi.

### 2.5.6 Mafunzo ya Ufundi Stadi

Serikali imeendelea kusajili na kutoa elimu ya ufundi stadi katika vyuo mbalimbali vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Vyuo hivyo, vinatoa mafunzo kwa kozi fupi na ndefu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata ujuzi unaohitajika katika soko. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya ufundi stadi vinavyomilikiwa na VETA ilikuwa 141,854 (wanawake 46,072 na wanaume 95,782). Aidha, wanafunzi 46,589 (wanawake 15,140 na wanaume 31,449) walihitimu mafunzo ya ufundi stadi kwa kozi ndefu. Katika kuendeleza mafunzo ya ufundi kwa wananchi, Serikali ilifanya ujenzi, upanuzi na ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi 48 vinavyomilikiwa na VETA pamoja na kuboresha mitaala 19 ili kuendana na mahiaji ya soko la ajira nchini.
Seriklai pia imeendelea kukuza ujuzi kwa wananchi kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi. Katika mwaka 2022/23, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya maendeleo ya wananchi ilikuwa 16,457 (wanawake 6,939 na wanaume 9,518). Serikali imefanya ujenzi, upanuzi pamoja na ukarabati wa vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi ili kuwezesha wanafunzi wengi kujiunga katika vyuo hivyo.

### 2.5.7 Ukuzaji Ubunifu

Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kuchochea ubunifu na ugunduzi nchini. katika mwaka 2022/23, wabunifu na wagunduzi 862 walitambuliwa ikilinganishwa na wabunifu na wagunduzi 714 waliotambuliwa

mwaka 2021/22. Bunifu hizo zinazokusudiwa kuleta tija ya uzalishaji wa huduma katika sekta ya kilimo, maji, nishati, madini, afya, TEHAMA na elimu. Kati yao, wabunifu mahiri 83 walitambuliwa na teknolojia 90 zilitambuliwa na kuhakikiwa na kufanya jumla ya teknolojia zilizozalishwa nchini na zilizotambuliwa kufikia 569 mwaka 2022/23 kutoka teknolojia 479 mwaka 2021/23. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na ubunifu nchini.

Hadi kufikia mwaka Juni 2023, wanafunzi takribani bunifu 64 (wanawake 8 na wanaume 56) wenye bunifu waliweza kufikia kilele. Aidha, bunifu mbalimbali zimeendelea kuibuliwa na kusimamiwa katika mikoa ya Dodoma,Iringa Mwanza, Dar es Salaam, Songwe,Katavi, Arusha, Morogoro, Njombe, Iringa na Mbeya. Bunifu hizo zimeendelea kulelewa na kusimamiwa na COSTECH pamoja na taasisi nyingine nchini ili kuaandaa kampuni kubwa za uwekezaji za ndani ya nchi kwenye nyanja mbalimbali kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.32**.

**Jedwali Na. 32:** Idadi ya Bunifu Zilizosajiliwa

| Na. | Jinsi | | Jumla ya Bunifu |
|---|---|---|---|
| | Wanawake | Wanaume | |
| 1. | 7 | 39 | 46 |
| 2. | 1 | 17 | 18 |
| 3. | **8** | **56** | **64** |

***Chanzo:*** *COSTECH, 2023*

### 2.5.8 Mafunzo ya Ujasiriamali

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa na huduma zinatolewa kwa kuzingatia ubora, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi imeendelea kuratibu taasisi mbalimbali za umma na binafsi nchini kujenga uwezo wa wajasiriamali kwa lengo la kuongeza maarifa na ujuzi wa kuanzisha na kusimamia biashara pamoja na kuzalisha bidhaa na kutoa huduma bora. Katika kuongeza idadi ya biashara mpya zinazoanzishwa, kurasimishwa na kukua na hatimaye kujenga uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla, wajasiriamali **118,752** (wanawake **67,756** na wanaume **50,996**) walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo mbalimbali kama inavyobainishwa katika **Jedwali Na.33**.

**Jedwali Na. 33:** Idadi ya Wajasiriamali Waliojengewa Uwezo

| Na. | Taasisi | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SIDO | 25,691 | 23,714 | 49,405 |
| 2 | UoI | 358 | 350 | 708 |
| 3 | IRDP | 44 | 31 | 75 |
| 4 | TET | 35 | 18 | 53 |
| 5 | OWM-KVAU | 1,396 | 1,289 | 2,685 |

| Na. | Taasisi | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Care International Tanzania | 17,136 | 32,000 | 49,136 |
| 7 | Aga Khan Foundation (AKF) | 2,002 | 2,168 | 4,170 |
| 8 | TWCC | - | 5,131 | 5,131 |
| 9 | Teach Man to Fish (TAMTF) | 265 | 441 | 706 |
| 10 | PASS Trust | 2,092 | 1,172 | 3,264 |
| 11 | UDSM | 126 | 117 | 243 |
| 12 | IFM | 1,351 | 825 | 2,176 |
| 13 | TETRATECH PSSA | 500 | 500 | 1,000 |
| **Jumla** | | **50,996** | **67,756** | **118,752** |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

### 2.5.9 Vituo Atamizi na Uendelezaji wa Teknolojia

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na Tume ya Sayansi na Technolojia na vyuo mbalimbali imeendelea kuhamasisha uanzisishaji na uendelezaji wa vituo atamizi nchini ili kuimarisha huduma za ulezi wa biashara changa na mawazo mapya ya kibiashara kwa zinazoanza. Aidha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kimeendelea kusimamia kituo atamizi cha Ujasiriamali na Ubunifu kinachoitwa Mipango Entrepreneurship and Innovation Center (MEI), ambapo Dira ya kituo ni kuwa kitovu cha ujasiriamali na ubunifu wa maendeleo vijijini na mijini nchini Tanzania. Lengo kuu la kituo ni kuendesha mafunzo na huduma za kuendeleza ujasiriamali na ubunifu kwa vitendo na kusaidia kutengeneza ajira kwa wahitimu wa Chuo, vijana na wananchi kwa ujumla, kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo na bidhaa za biashara ili kuimarisha uchumi wa viwanda na kupunguza umaskini kwa wananchi mjini na vijijini. Aidha, Chuo Kikuu cha Iringa kupitia Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu kimeendelea kuendesha shughuli za ubunifu na ujasiriamali kupitia atamizi yake ya ubunifu ya Kiota (Kiota Innovation Hub). Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu – CEI na atamizi yake kimeendelea kutumia mbinu mbalimbali zinazosaidia kuchochea fikra za ubunifu kwa vijana na hivyo kuwapatia msingi imara wa kuanza na kusimamia biashara.

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali kupitia COSTECH imezijengea uwezo kampuni changa 6 kupitia Atamizi ya Biashara ya Kiditali ya Dar es Salaam (Dar es Salaam Teknohama Business Incubator (DTBi) ambayo ipo ndani ya eneo la Tume ya Sayansi na Teknolojia. Aidha, kampuni hizo zimeweza kujengewa uwezo kwenye nyaja za kibiashara. Katika kukuza ubunifu,Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Chuo Kikuu Cha Iringa, Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE), Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo vyote vimemeendelea kutoa huduma atamizi kwa vijana ili kulea mawazo bunifu kupitia vituo vyao.

#### 2.5.10 Ukuzaji Nguvukazi

Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Taifa ya Ukuzaji Ujuzi kwa vijana kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, vijana 21,586 walipata mafunzo ya ujuzi unaohitajika katika soko la ajira ili waweze kuajiriwa na kujiajiri. Kati yao, vijana 8,318 walipata mafunzo ya uanagenzi; wahitimu 5,508 walipata mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi; na vijana 7,760 walipata mafunzo ya ufundi stadi na kurasimisha ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi.

Serikali kupitia Kitengo cha Huduma za Ajira kilisajili watafuta kazi 10,540 na kuwapatia ushauri nasaha kuhusu uchaguzi wa kazi. Kati yao, wanawake walikuwa 4,338 na wanaume walikuwa 6,202. Aidha, watafuta kazi 5,161 (wanaume 2,816 na wanawake 2,345) walipata mafunzo. Mafunzo hayo yalitolewa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutafuta kazi, kushindania fursa za ajira ndani na nje ya nchi pamoja na kujenga maadili ya kazi yanayohitajika na waajiri mbalimbali. Vijana 909 (wanaume 540 na wanawake 369) waliunganishwa na fursa za kazi kwa waajiri mbalimbali nchini.

#### 2.5.11 Programu ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana



Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa (National Service Act, No 16) ya mwaka 1964, Kwa lengo la kuwalea Vijana wa kitanzania, ili kuwajenga kinidhamu, uzalendo, ukakamavu na kuwafundisha ujuzi na hatimaye kuchangia katika ulinzi wa Taifa na Maendeleo ya kiuchumi. Dhima ya Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwalea vijana wa kitanzania iliawajenga kinidhamu, uzalendo, ukakamavu na kuwafundisha ujuzi na hatimaye kuchangia katika ulinzi wa Taifa na Maendeleo ya Kiuchumi. Katika kufanikisha adhima hiyo, mwaka 2022/23 Serikali kupitia JKT imefanikiwa kutoa mafunzo kwa jumla ya vijana 24,458 wa Mujibu wa Sheria wamepatiwa mafunzo, kati yao, vijana 17,942 wa kiume na 6,516 wa kike. Aidha, vijana 11,358 wa kujitolea wamepatiwa mafunzo, kati yao, 7,483 ni wa kiume na 3,875 ni wa kike kupitia kambi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: JKT-Rwamkoma-Mara, JKT Msange - Tabora, JKT Ruvu - Pwani, JKT-Mpwapwa, JKT-Makutupora Dodoma, JKT Mafinga - Iringa, JKT Mlale-Ruvuma, JKT Mgambo, JKT Maramba -Tanga, JKT Makuyuni -Arusha, JKT Bulombora, JKT Kanembwa, JKT Mtabila- Kigoma, JKT Itaka - Songwe, JKT Luwa, JKT Milundikwa - Rukwa, JKT Nachingwea – Lindi, JKT Kibiti- Pwani na Oljoro JKT- Arusha kwa Operesheni Jenerali Venance Mabeyo.

#### 2.5.12 Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inaetekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (Building a Better Tomorrow, Youth Involvement for Agribusiness (BBT –

YIA)) wa kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo kwa mwaka 2022 hadi 2030. Programu hiyo inalenga kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia sekta ya kilimo ikiwemo utekelezaji wa ajenda 10/30 kwa kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo cha mazao kutoka asilimia 4.1 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Inatarajiwa kuwa mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi yataongezeka kutoka 1.2 bilioni mwaka 2022 hadi kufikia bilioni 5 ifikapo mwaka 2030. Aidha, Programu hiyo inaenda sambamba na utekelezaji wa Sera, Programu na Mipango ya Kitaifa ikiwemo Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), FYDPIII na ASDP.

Katika kuongeza uzalishaji wa mazao na kupunguza gharama za kilimo cha mashamba makubwa ya pamoja; Wizara ya Kilimo imeainisha, imepima na kuweka mawe ya upimaji kwa ajili ya kuyapatia hati miliki mashamba makubwa ya pamoja 28 yenye jumla ya ekari 196,889.30 katika Mikoa ya Dodoma (ekari 34,613), Kagera (ekari 5,640.30), Mbeya (ekari 52,165), Njombe (ekari 87,501.25), Kigoma (ekari 14,874.75) na Pwani (ekari 2,095). Mashamba yaliyoainishwa yatagawiwa kwa vijana waliochaguliwa na kupatiwa mafunzo ya kilimo biashara.

Katika kuendeleza mafunzo ya vijana katika kilimo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilitangaza nafasi kwa vijana kujitokeza kuomba kujiunga na mafunzo ya kilimo biashara katika vituo atamizi vilivyoandaliwa kupitia tovuti www.bbt.kilimo.go.tz, ambapo vijana 20,227 waliomba kati yao wanawake ni 4,722 na wanaume ni 15,505. Baada ya kukamilisha taratibu za uchambuzi vijana 812 walikidhi vigezo vya kupata mafunzo ya kilimo biashara kwa awamu ya kwanza. Kati ya hao, wanawake ni 282 na wanaume ni 530.

Vijana hao waliwasili katika vituo atamizi 13 vilivyoandaliwa kwa ajili ya kupatiwa mafunzo kwa muda wa miezi minne. Vyuo vya mafunzo vilivyochaguliwa ni pamoja na Bihawana (ekari 22);Mlingano (Ekari 4), Uyole (Ekari 3), Mubondo (ekari 10), Ukiriguru (ekari8.9), NSI -Kidatu (ekari 2.4), Hort Tengeru (ekari4), Mtwara (ekari 10), Ilonga (ekari 3.5) na Tumbi (ekari 10). Baada ya kuhitimu mafunzo hayo vijana watapatiwa mashamba yenye ukubwa usiozidi ekari 10 kulingana na aina ya mazao.

### 2.5.13 Programu ya Ujasiriamali ya Probono ya Mashindano ya Biashara Mashuleni

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi kwa kushirikiana na *Probono Entrepreneurship Programme (PEP)* pamoja taasisi ya Teach A Man To Fish (TAMTF) inatekeleza PEP ya Mashindano ya Kibiashara Shuleni (Schools Enterprise Challenge) ambayo imejielekeza katika kuratibu utekelezaji wa Mshirikiano ya kibiashara Shuleni. Jitihada hizo zinalenga kufanikisha mikakati ya Serikali kama vile ya Mkakati Jumuishi wa Taifa wa Ujasiriamali (Inclusive National Enterpreneurship Strategy - INES) na Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji Ujasiriamali (NETF) nchini Tanzania. Programu hii inatekelezwa na Shirika la Tech A Man To Fish (TAMTF) kwa kushirikiana na shirika la Kijerumani la PROBONO chini ya usimamizi wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi. Programu inalenga kuwajengea uwezo wa kupanga biashara na utekelezaji wa biashara kwa wanafunzi shuleni.

Programu hii katika hatua ya awali imetekelezwa katika shule 11 za sekondari katika mikoa ya Dar es Salaam (3), Arusha (4) na Kilimanjaro (4). Programu hiyo imetoa mafunzo kwa wakufunzi 22 wa shule hizo ili kutekeleza programu ya mashindano ya kibiashara katika shule za Sekondari (School Enterprise Challenge). Aidha, Programu imewezesha kuanzishwa kwa klabu za wanafunzi zijulikanazo kama Probono Entrepreneurship Programme's Club (PEP Club). Utekelezaji wa Programu hiyo, umewezesha wanafunzi wenye miradi inayokopesheka kushindanishwa ili kuwajengea hamasa ya kujenga mitazamo chanya ya ujasiriamali.

Shule 11 zimefanikiwa kupiga hatua kutoka hatua ya awali kabisa ya BRONZE mwaka 2021 ambapo mwaka 2022 zikaingia katika hatua ya pili ya SILVER ambapo shule tayari zinaendesha biashara na zimeanza kuingiza kipato na wanafunzi wanajifunza elimu ya fedha na ujasiriamali. Mwaka 2023 shule hizo zimefanikiwa kuingia hatua ya mwisho na ya juu zaidi ya Gold, ambapo inategemewa kuwa zitaendelea kuboresha biashara zao na kuzifanya katika ubora zaidi, kutumia vipato walivyoingiza kupanua biashara zao au kuanzisha miradi mingine ya shule na pia kuanza kutoa elimu hii kwa shule jirani za msingi na sekondari na kuanza kuwalea kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 34**.

Idadi ya washiriki katika programu ya ujasiriamali kwa vijana shuleni imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Mwaka 2021 washiriki walikuwa 463 (wavulana 201 na wasichana 262). Mwaka 2022 washiriki walikuwa 534 (wavulana 206 na wasichana 328) na mwaka 2023 washiriki wamefikia 706 (wavulana 265 na wasichana 441). Hatua hii inaonesha namna shule na wanafunzi wameipokea vizuri programu hii na kuipenda na hata wengine wanapoona jinsi wenzao wanavyonufaika na wao wanavutika kujiunga na programu ili kupata mafunzo hayo.

**Jedwali Na. 34:** Aina ya Biashara zinazofanywa na Shule zinazonufaika na Programu ya Probono

| Shule Zilizonufaika | Aina ya Biashara |
|---|---|
| Mbonea Sekondari | Benki ya wanafunzi, sabuni za maji na vipande, ushonaji wa viatu |
| Kiluvya Sekondari | Vyungu vya maua, bangili za mikononi na jamvi ndogo za mezani |
| Mwanga Sekondari | Saluni na ufugaji wa kuku |
| Dr. Asha Rose Sekondari | Saluni na vyakula |
| Edmund Rice Sekondari | Benki ya wanafunzi na vyakula |
| St. Mary's Duluti | Sabuni za maji, vyungu vya maua, mapambo na vyakula |
| Losirway Sekondari | Sabuni za maji na ufugaji wa panya kwa ajili ya mitihani. |

***Chanzo:*** *NEEC, 2023*

**2.5.14 Mashirika Yasiyo ya Kiserikali**

Serikali imeendelea kufanya usajili, uratibu na kufuatlia utendaji kazi wa Mashirikia Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura Na. 56. Majukumu yanafanyika ili kuhakikisha mazingira wezeshi kwa Mashirika haya ili yaendelee kutoa michango katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Mashirika hayo yamekuwa yakiomba usajili ili kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo afya, maji, mazingira, elimu, kilimo na masuala ya haki za binadamu na hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya mashiriki 14,059 yalikuwa na usajili. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali ilifanikiwa kusajili Mashirika 1,106 yakiwemo Mashirika ya Kimataifa 49, Kitaifa 1,014, Mkoa 24 na Wilaya Mashirika 19. Hadi kufikia Aprili, 2023 kati ya Mashirika 14,059 yaliyosajiliwa, Mashirika 4,898 yalibainika kutozingatia Sheria ambapo tarehe 19 Januari, 2023 Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali iliyafutia usajili hivyo kubakia na Mashirika hai 9,161.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Taifa kupitia utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, hifadhi ya jamii, uwezeshaji kiuchumi, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu. Aidha, ajira 14,121 zilitolewa, ambapo kati ya hizo ajira 8,344 zilitolewa kwa watanzania sawa na asilimia 59.8 ya ajira zote na ajira 5,777 zilizotolewa kwa wasio watanzania sawa na asilimia 40.2 ya ajira zote.

Takwimu zinaonesha kuwa, katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 955 yaliyowasilisha taarifa inaonesha kuwa NGOs zilipokea Shilingi Trilioni 1.2 na kutumia Shilingi Trilioni 1.1 katika shughuli za maendeleo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: afya, elimu, hifadhi ya jamii, uwezeshaji kiuchumi, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu.

**2.5.15** Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kuinua Viwango vya Ujuzi na Uzoefu

Kutokana na jitihada zilizofanyika katika kuinua viwanga vya ujuzi na uzoefu, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Wabunifu na wagunduzi 862 walitambuliwa ikilinganishwa na wabunifu na wagunduzi 714 waliotambuliwa mwaka 2021/22. Bunifu hizo zinazokusudiwa kuleta tija ya uzalishaji wa huduma katika sekta ya kilimo, maji, nishati, madini, afya, TEHAMA na elimu;

(b) Elimu ya ujasiriamali ilitolewa kwa wajasiriamali 118,752 ambapo wanawake walikuwa 67,756 na wanaume 50,996. Mafunzo hayo yalitolewa na watoa huduma za biashara mbalimbali wakiwemo SIDO, NGOs, CSOs, na vyuo vikuu; na

(c) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 638 yalijengewa uwezo katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni zilizopo. Mashirika hayo ni kutoka katika mikoa ya Dodoma (45), Singida (51), Tabora (38), Shinyanga (53), Geita (35), 89 Njombe (50), Ruvuma (64), Rukwa (56),

Lindi (32), Mtwara (54), Iringa (62), Mbeya (60) na Tanga (38) na Wasajili Wasaidizi 110 kutoka katika mikoa iliyotajwa hapo juu ukijumuisha mkoa wa Songwe.

Pamoja na jitihada zilizofanyika katika kuinua ujuzi na uzoefu, bado kuna changamoto zinawakabili wananchi katika kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi kutokana na upungufu wa ujuzi na uzoefu kama inavyoonesha katikam **Jedwali Na.35**.

**Jedwali Na. 35:** Changamoto na Mikakati ya Kuinua Ujuzi na Uzoefu

| *Changamoto* | *Mikakati* |
|---|---|
| *(i) Kutoanzishwa kwa Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi.* | *(i) Kuanzisha Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi.* |
| *(ii) Mfumowa elimu haujengi fursa ya uendelezaji wa ujasiriamali.* | *(ii) Kuboresha mfumo wa elimu ili kuwajengea wananchi misingi imara kwa kuwa na ujuzi na uzoefu kulingana na mahitaji ya ushindani katika masoko mbalimbali.* |
| *(iii) Ukosefu wa baadhi ya ujuzi na uzoefu kwa wananchi kwenye maeneo mbalimbali katika kuzalisha bidhaa na utoaji wa huduma.* | *(iii) Kuboresha mfumo wa SDL ili kuwawezesha wanafunzi wa vyuo vikuu kupata ujuzi unaohitajika kwenye soko na kuwawezesha kuajiriwa na kujiajiri.* |
| *(iv) Mfumo wa matumizi ya fedha za SDL kutotumika kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ili kuwawezesha vijana kupata ujuzi unaohitajika kwenye soko na kuwawezesha kuajiriwa na kujiajiri.* | |

## 2.6 MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI


Sera ya Taifa ya uwezeshaji Kiuchumi inatambua mchango wa miundombinu ya kiuchumi katika kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Miundombinu ya kiuchumi iliyopo kama vile barabara, nishati na mtandao wa mawasiliano huwawezesha wananchi katika kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi kwa urahisi na kwa gharama nafuu na shindani. Serikali imeendelea na ujenzi na uboreshaji miundombinu ili kuwapa wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi. Katika mwaka 2022/23, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ili irahisishe harakati za kukuza uchumi na pia kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa za kiuchumi. Hali halisi ya utekelezaji wa mikakati ya

miundombinu ya kiuchumi kulingana kama ilivyobainishwa katika kipengele 2.6.1 hadi 2.6.12.

### 2.6.1 Usajili na Ushiriki wa Makandarasi katika Miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi

**Mchoro Na. 6** hapa chini linaonesha hali halisi ya usajili wa makandarasi waliopo katika rejesta ya Bodi ya usajili wa Makandarasi katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2023. Mwenendo wa usajili unaonesha idadi ya makandarasi waliosajiliwa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2020, makandarasi walikuwa **11,749** huku ya makandarasi wa kigeni wakiwa **442** na wa ndani wakiwa **11,307.** Aidha, katika kipindi cha mwaka 2022/2023 idadi ya makandarasi walikuwa **14,675** ambapo makandarasi wa kigeni walikuwa **542** na makandarasi wa ndani wakiwa ni **14,133** ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 ambapo kulikuwa na jumla ya makandarasi **14,034** huku makandarasi ya kigeni yakiwa ni **528** na makandarasi wa ndani wakiwa ni **13,506** hii ni sawa na ongezeko la makandarasi **641** hadi kufikia Juni, 2023 kama Mchoro hapa chini linavyoonesha

**Mchoro Na. 6: Usajili na Ushiriki wa Makandarasi katika Miradi ya Ujenzi**




| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 June |
|---|---|---|---|---|
| Idadi ya makandarasi waliosajiliwa | 11,749 | 12,693 | 14,034 | 14,675 |
| Makandarasi wa Kigeni | 442 | 480 | 528 | 542 |
| Makandarasi wa ndani | 11,307 | 12,213 | 13,506 | 14,133 |

***Chanzo:*** *Bodi ya Usajili Makandarasi (CRB), 2023*

Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhimiza ushiriki wa makandarasi wa ndani kunufaika na fursa za kazi zinazohitaji ujuzi na uzoefu.Jedwali hapa chini linaonesha ya miradi **4,708** yenye thamani ya shilingi **trilioni 8.149** ilitekelezwa hadi kufikia 2022/2023 ikilinganishwa na miradi **4,013** yenye thamani ya shilingi bilioni 6,128 iliyotekelezwa mwaka 2021/2022. Idadi ya miradi **4,578** yenye thamani ya shilingi **bilioni 3.57** ilifanywa na makandarasi wa ndani huku miradi

**130** yenye thamani ya shilingi **bilioni 4.58** ikifanywa na makandarasi wa kigeni. Takwimu za mwenendo wa ushiriki wa makampuni ya kitanzania katika miradi ya ujenzi nchini kwa kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia 2020 hadi Juni, 2023 zinaonesha makandarasi wa ndani bado wanazo changamoto zinazo wakabili katika kutekeleza miradi kama vile upungufu wa mitaji na ukosefu wa mitambo na hivyo kushindwa kutekeleza miradi yenye thamani kubwa.

**Jedwali Na. 36:** Ushiriki wa Makandarasi Katika Miradi ya Miundombinu ya Kiuchumi

| Mwaka | Idadi ya Miradi | Thamani ya Miradi (TZS Bn) | Idadi iliyofanywa na makandarasi wa ndani | Idadi ya miradi iliyofanywa na makandarasi wa Kigeni | Thamani ya miradi iliyofanywa na makandarasi wa ndani (TZS Bn) | Thamani ya miradi iliyofanywa na makandarasi wa kigeni (TZS Bn) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **2020** | 3,179 | 3,807 | 3,075 | 104 | 1,770 | 2,037 |
| **2021** | 3,878 | 5,270 | 3,775 | 103 | 2,803 | 2,467 |
| **2022** | 4,013 | 6,128 | 3,871 | 142 | 3,071 | 3,057 |
| **2023 June** | 4,708 | 8,148 | 4,578 | 130 | 3,570 | 4,578 |

***Chanzo:*** *Bodi ya Usajili wa Makandarasi, 2023*

Aidha, takwimu za Bodi ya Usajili wa Makandarasi zinaonesha makandarasi wa ndani wanafanya miradi mingi lakini yenye thamani ndogo kulinganisha na makandarasi wa nje wanaofanya miradi michache yenye thamani kubwa. Hivyo, kuna haja ya kuendelea kuwajengea uwezo makandarasi wa ndani na vilevile Serikali kuendelea kutenga miradi ya upendeleo itakayowajengea uwezo makandarasi wa ndani. Tathmini inapendekeza umuhimu wa Makandarasi kulipwa kwa wakati na pale inapobidi kuwekwa utaratibu utakaowawezesha makandarasi wa kigeni watekeleze miradi mikubwa kwa ubia na makandarasi wa ndani na mamlaka za ununuzi kuondoa masharti magumu yasiyo na tija kwenye zabuni hususan za miradi mikubwa.

**Jedwali Na. 37** hapa chini linaonesha idadi ya miradi ya ubia na thamani zake iliyotekelezwa hapa nchini ambapo mwaka 2022/2023 miradi 63 ya ubia yenye thamani ya shilingi bilioni 487 ilitekelezwa ikilinganishwa na miradi 45 yenye thamani ya shilingi bilioni 382 iliyotekelezwa mwaka 2021/2022. Kumekuwa na ongezeko la miradi ya ubia inayofanywa baina ya makandarasi wa ndani huku thamani yake ikiwa ni shilingi bilioni 99 pungufu ya idadi ya miradi 6 yenye thamiani ya shilingi bilioni 287 iliyotekelezwa na makandarasi wa kigeni wenyewe kwa wenyewe. Sambamba na hayo ni idadi ya miradi 2 pekee yenye thamani ya shilingi bilioni 8 ilifanikiwa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia wa makandarasi wa ndani na wa kigeni. Hivyo, Serikali inapaswa kuendelea kuhimiza uingiaji wa ubia ili makampuni ya kitanzania yanufaike na fursa za urithishaji wa ujuzi, uhaulishaji wa

teknolojia na hatimaye thamani kubwa ya ziada kubaki hapa nchini na kuiwezesha ukuaji wa maendeleo ya sekta binafsi. Jedwali hapa chini linaonesha mchanganuo wa mwenendo wa hali halisi ya ushiriki wa makampuni ya makandarasi wa ndani na yale ya kigeni.

**Jedwali Na. 37:** Mwenendo wa Miradi ya Ubia

| Mwaka | Idadi ya miradi ya Ubia | Thamani ya miradi ya ubia (TZS Biln) | Idadi ya miradi ya ubia baina ya makandarasi wa ndani | Thamani ya miradi ya ubia makandarasi wa ndani wenyewe kwa wenyewe (TZS Biln) | Idadi ya miradi ya ubia makandarasi wa kigeni wenyewe kwa wenyewe | Thamani ya miradi ya ubia makandarasi wa kigeni wenyewe kwa wenyewe (TZS Biln) | Idadi ya miradi ya ubia makandarasi wa ndani na wa kigeni | Thamani ya miradi ya ubia baina ya makandarasi wa ndani na wa kigeni (TZS Biln) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2020** | 43 | 674 | 41 | 67 | 2 | 607 | 0 | 0 |
| **2021** | 47 | 379 | 42 | 174 | 3 | 133 | 2 | 72 |
| **2022** | 45 | 382 | 39 | 98 | 6 | 283 | 0 | 0 |
| **2023 June** | 63 | 487 | 55 | 99 | 6 | 287 | 2 | 8 |

***Chanzo:*** *Bodi ya Usajili wa Makandarasi, 2023*

### 2.6.2 Mawasiliano

Serikali imeendelea kuimalisha mfumo wa mawasiliano nchini ili kurahisisha mawasiliano baina ya mtu na mtu, taasisi kwa taasisi hata Taifa na Taifa kwa lengo la kuchoche shughuli za kiuchumi. Mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa uliokusudia kuongeza wigo wa mawasiliano ya simu na intaneti nchini na nchi jirani katika kuharakisha mapinduzi ya kidijitali ukijumuisha ujenzi vituo vya utoaji huduma na vituo vya kutunzia data. Aidha, Serikali imefanikiwa kununua mitambo kwa ajili ya vituo 137 vya kutolea Huduma (transmission and power equipments) ambapo usimikaji umefanyika kwenye vituo 26 vya kutolea huduma (Point of Presence-POPs and Optical Line Amplifiers OLA) kwenye maeneo ya Dar es Salaam, Chalinze Tanesco, Chalinze TTCL, Manga, Hale Tanesco, Hale TTCL, Tanga, Horohoro, Mkomazi, Same, Mwanga, Moshi, Arusha, Makuyuni, Babati, Namanga, Morogoro, Kidatu, Ifakara, Kihansi, Iringa, Mtera, Dodoma, Manyoni, Singida na Katesh.

### 2.6.3 Huduma ya Umeme

Maendeleo ya nchi yoyote yanahitaji uhakika wa upatikanaji wa nishati. Upatikanaji wa nishati ya uhakika na gharama nafuu ni kichocheo cha kukua kwa shughuli za kiuchumi nchini. Serikali imeweka mkazo katika Nishati kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ikiwa ni pamoja na kuongeza thamani katika bidhaa za kilimo, uvuvi, ufugaji, madini na maliasili. Mpango huu utachangia kupunguza gharama za utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na hivyo kuimarisha tija na ufanisi na upatikanaji wa mapato ya wananchi

na Serikali. Mwaka 2022/23, Serikali ilizamia kutekeleza miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme, ikiwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa bwawa la Nyerere (Rufiji), kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa katika Mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera na mradi mkubwa wa Kuimarisha Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization Project); kutekeleza Miradi ya Nishati Vijijini pamoja na kuanza utaratibu wa kupeleka umeme katika Vitongoji vyote nchini; kukamilisha mazungumzo ya mradi wa LNG na kuanza maandalizi ya utekelezaji wake; kutekeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwemo jotoardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya Nishati (Energy Efficiency and Conservation); kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini; na kuimarisha TPDC na Kampuni zake Tanzu za TAN-OIL na GASC. Hadi Juni, 2023 Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi, kupitia mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa umeme kwa asilimia 10.5 na kufikia MW 1,872.05 ikilinganishwa na MW 1,694.55 zilizokuwepo mwaka 2021/22. Kati ya kiasi hicho, MW 574.60 sawa na asilimia 30.69 zinatokana na nguvu ya maji, MW 1,198.82 sawa na asilimia 64.04 gesi asilia, MW 88.13 sawa na asilimia 4.71 mafuta na MW 10.50 sawa na asilimia 0.56 tungamotaka (biomass).

**2.6.4 Bwawa la Mwalimu Nyerere**

Huduma ya umeme ina mchango mkubwa katika kuchochea shughuli za kiuchumi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere. Hadi Juni, 2023 jumla ya mita za kina 160.51 kutoka usawa wa bahari zilifikiwa kuelekea mita 163 kutoka usawa wa bahari ikiwa ni kiwango cha chini cha maji kinachotakiwa itakachoweza kuzalisha umeme wa MW 2,115. Utekelezaji wa mradi huo katika maeneo yote kwa ujumla ulifikia asilimia 86.89 mwaka 2022/23 kutoka asilimia 60.22 zilizokuwa zimefikiwa mwaka 2021/22.

**2.6.5 Hali ya Usambazaji Umeme**

Serikali kupitia TANESCO imeendelea kusimamia utoaji wa huduma kwa wateja nchini ikizingatiwa kuwa wateja ni kipaumbele muhimu katika Mpango Mkakati wa Mpito wa Shirika. Shirika limeboresha masuala mbalimbali, ikiwemo kituo cha miito ya simu (unified call centre) ambacho kinafanya kazi saa 24. Mwaka 2022/23 Serikali kupitia REA iliongeza wigo wa njia za Msongo Mdogo kutoka kilomita moja (1) hadi kilomita tatu (3) na kuongeza wateja kutoka 22 hadi 66 kwa kila kijiji ili kuhakikisha maeneo muhimu na kaya nyingi zaidi zinafikiwa na huduma ya umeme.

Aidha, Serikali iliendelea na ujenzi wa njia za usambazaji wa umeme, kuhamasisha wananchi kuunganishiwa umeme na kuunganisha wateja uliofikia asilimia 68.66 ambapo jumla ya vijiji 1,880 kati ya 4,071 sawa na asilimia 46.18 vimeunganishiwa.

**2.6.6 Miradi ya Barabara na Madaraja**

Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imeendelea kuboresha barabara na madaraja ili kurahisha muingiliano wa watu kutoka eneo moja kwenda jingine kupitia Barabara, Reli, Vivuko na Viwanja vya Ndege. Katika mwaka 2022/23,

Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imeendelea kusanifu, kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa zenye jumla ya kilometa 36,760.29 ikiwa ni pamoja na ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 470, ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 33 na ujenzi wa madaraja makubwa matatu (3), ambayo ni Daraja la JPM (Kigongo – Busisi, Mwanza), Daraja la Pangani (Tanga) na Daraja la Wami (Pwani). Hadi Juni, 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 179.18 umekamilika, kilometa 290.82 unaendelea ambapo kilometa 161.49 za tabaka la juu la msingi (basecourse), kilometa 192.03 za tabaka la kati la msingi (Sub - Base) na kilometa 259.94 za tuta la barabara zimejengwa. Aidha, ujenzi wa daraja la Wami umekamilika; ujenzi wa madaraja mawili (2) ya JPM (Kigongo – Busisi, Mwanza) umefikia asilimia 72 na kwa daraja la Pangani (Tanga) ujenzi umeanza na umefikia asilimia 3. Kukamika kwa miundombinu hiyo kuchochea shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na usafirishaji wa mazao kutoka eneo moja kwenda sokoni.

### 2.6.7 Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko. Hadi Juni, 2023, miradi iliyokamilika ni ukarabati wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Magogoni na upanuzi wa eneo la maegesho katika kituo cha Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza ikiwa ni pamoja na kukamilisha usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukatia tiketi (N-Cards System). Aidha, ukarabati wa vivuko vya MV Kazi, MV TEMESA, MV Musoma na MV Tanga umekamilika. Sambamba na hizo, ujenzi wa maegesho ya Iramba – Majita upande wa Majita, ujenzi wa maegesho ya Bugolora – Ukara na miundombinu katika kituo cha Chato (Geita) umekamilika. Ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kisorya - Rugezi (Ukerewe) umefikia asilimia 57 na kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa umbo la kivuko (super structure) na ujenzi wa vivuko vya Ijinga – Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Ukerewe), Nyakarilo – Kome (Buchosa) umefikia asilimia 35.

### 2.6.8 Viwanja vya Ndege

Mwaka 2022/23, Serikali imeanza ujenzi wa viwanja vipya vya ndege vya Geita, Simiyu na Msalato. Serikali pia imeendelea kufanya ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege 20 nchini ambavyo ni pamoja na Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mwanza, Arusha, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Dodoma, Tanga, Lake Manyara, Lindi, Moshi, Bukoba, Julius Nyerere International (JNIA) na Viwanja vingine vya Ndege vya Mikoa.

### 2.6.9 Huduma ya Maji

Rasilimali za maji ni muhimu katika uzalishaji wa bidhaa na mazao pamoja na utoaji huduma. Rasilimali za maji zilizopo nchini zinakadiriwa kuwa mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka ambapo rasilimali za maji juu ya ardhi ni mita za ujazo bilioni 105 na zilizopo ardhini ni mita za ujazo bilioni 21 mahitaji ya maji kwa matumizi

mbalimbali nchini yanakadiriwa kuwa ni takribani mita za ujazo bilioni 47 kwa mwaka sawa na asilimia 37.37 ya maji yaliyopo nchini.

**2.6.10 Upatikanaji wa Huduma wa Maji Vijijini**

Katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi waishio vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, Serikali imeendelea kujenga, kukarabati, kupanua mitandao ya kusambaza maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma ya maji. Hadi Juni, 2022/23, upatikanaji wa huduma ya maji vijijini imefikia wastani wa asilimia 74.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 72.3 mwaka 2021/22. Kiwango hicho kinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa miradi mipya, ukarabati na upanuzi wa miradi 303 ambayo imeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 1,467,107.

**2.6.11 Ujenzi wa Miundombinu ya Uhifadhi wa Mazao ya Chakula**

Serikali imeendelea kukuza shughuli za kilimo kwa kufanya ujenzi wa miundombinu ya kilimo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ghala 38 za kuhifadhi mazao katika ngazi ya kata na vijiji. Hadi kufikia Juni, 2023, ujenzi wa ghala 28 katika Mkoa wa Ruvuma umefikia asilimia 40. Serikali kupitia mradi wa TANIPAC imekamilisha ujenzi wa ghala 10 (9 Tanzania Bara na 1 Zanzibar) za kuhifadhi mazao. Aidha, ukamilishaji wa ujenzi wa maghala manne (4) yaliyobaki unaendelea. Kukamilika kwa ghala zote 14 kutaongeza uwezo wa kuhifadhi tani 21,500. Serikali kupitia NFRA umefikia uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 90,000 katika kanda za Katavi (Mpanda), Rukwa (Sumbawanga) na Manyara (Babati) na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kutoka tani 251,000 mwaka 2021/22 hadi tani 341,000 mwaka 2022/23.

**2.6.12 Kuongeza hekta 95,000 za umwagiliaji**

Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kujenga skimu za umwagiliaji mpya 25, kukarabati skimu 30 na kujenga mabwawa 14. Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya mikataba 48 imesainiwa yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 406.8** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kati ya miradi hiyo, 19 ni ya ujenzi wa skimu mpya, 19 ni ya ukarabati wa skimu na 10 ni ya ujenzi wa mabwawa. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 95,000 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kuwa hekta 822,285.6 sawa na asilimia 68.5 ya lengo la kufikia hekta 1,200,000 za umwagiliaji ifikapo mwaka 2025.

**2.6.13 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Miundombinu ya Kiuchumi**

Kutokana na jitihada zilizofanyika katika kuboresha miundombinu ya kiuchumi, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Makandarasi wa ndani 865 walipewa mikataba ya ubia na makandarasi wa nje wanaotekeleza miradi ya kimkakati ikiwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR.

(b) Miradi 1,726 yenye thamani ya shilingi 754,467,282,939.28 ilitekelezwa na kukamilika chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA). Jumla ya makandarasi 1,927 walinufaika kwa kupata zabuni za

kazi za ujenzi wa barabara za vijijini na mijini. Makampuni ya wakandarasi wa nje yaliyonufaika ni 12 huku makampuni ya makandarasi wa ndani yakiwa ni 1,922. Aidha, kazi za matengenezo ya barabara na madaraja zenye thamani ya shilingi 405,723 milioni zilitekelezwa na makandarasi wa ndani katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2023.

(c) Kuongeza uwezo wa kuhifadhi nafaka kupitia NFRA kutoka tani 251,000 mwaka 2021/22 hadi tani 341,000 mwaka 2022/23.

(d) Kuongezeka kwa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere katika maeneo yote kwa ujumla ulifikia asilimia 86.89 mwaka 2022/23 kutoka asilimia 60.22 zilizokuwa zimefikiwa mwaka 2021/22.

Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu ya kiuchumi, bado kuna changamoto ambazo zinakwamisha shughuli za kiuchumi kutokana na miundombinu duni kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.38**.

**Jedwali Na. 38:** Changamoto na Mikakati ya Kuboresha Miundombinu ya Kiuchumi

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Makandarasi wa ndani bado wanakabiliwa na changamoto za ukosefu wa mitaji na mitambo katika kutekeleza miradi ya miundombinu ya kiuchumi.* | *(i) Kuanzisha Taasisi ya Wakala wa Dhamana Tanzania (Tanzania Credit Guarantee Agency) kwa ajili ya kuwawezesha wananchi, kampuni na makandarasi kupata mitaji na dhamana kwa ajili ya miradi wanayoanzisha wao wenyewe au ile ya ubia na wageni,* |
| *(ii) Ukosefu wa huduma za umeme za uhakika na kupelekea kuathiri shughuli za kiuchumi.* | *(ii) Kuondoa masharti magumu yasiyo na tija kwenye zabuni hususan za miradi mikubwa ya kimkakati.* |
| *(iii) Kuchelewa kukamilika kwa wakati miradi ya ujenzi na matengenezo ya barabara, reli, skimu za umwagiliaji na maji. Hali hiyo inakwamisha shughuli za kiuchumi kwa kuongeza gharama za uzalishaji pamoja na kuathiri uwekezaji nchini.* | *(iii) Kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na barabara, reli, skimu za umwagiliaji na maji ili kuchochea shughuli za kiuchumi na uwekezaji nchini* |
| *(iv) Kukosekana kwa miundombinu wezeshi na rafiki katika maeneo mengi. Miundombinu hiyo ni barabara, maji, mawasiliano, umeme wa uhakika, reli na bandari hivyo kupelekea uwekezaji mwingi wa miradi kujazana katika mikoa yenye miundombinu imara kama Dar es Salaam, Pwani, Arusha, na Mwanza* | |

## 2.7 UWEKEZAJI WA MASOKO YA MITAJI NA UMILIKI WA HISA

Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kushirikisha wananchi katika kumiliki uchumi kwa kuhamasisha wananchi katika uwekezaji wa mitaji pamoja na kumiliki hisa kwenye masoko ya mitaji na dhamana. Aidha, taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 katika kipindi cha mwaka 2022/23 imeainisha utekelezaji wa mikakati, na mafanikio yaliyopatikana katika uwekezaji wa masoko ya mitaji na umiliki wa hisa. Aidha, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Sheria ya Masoko na Mitaji ya Dhamana ya mwaka 2002, ambapo katika kipindi cha mwaka 2022/23, mwenendo wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ulikuwa mzuri. Ufanisi huu umetokana na juhudi za Serikali katika kutoa elimu kuhusu fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji. Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 uliongezeka kwa asilimia 4.21 na kufikia shilingi trilioni 10.83 ikilinganishwa na shilingi trilioni 10.39 katika kipindi kilichoishia Juni, 2022.

### 2.7.1 Ukuaji wa Thamani ya Hisa na Malipo ya Gawio

Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa fedha za mitaji na kutoa fursa ya kuwekeza na kukuza uwekezaji wa mtu mmoja mmoja, vikundi, taasisi binafsi na umma pia. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023, Soko la Hisa lilikuwa kutoka ukubwa wa soko wa shilingi bilioni **10.21** hadi shilingi bilioni **10.83** ambayo ni sawa na asilimia **6**. Ukuaji huu mtaji ulichangiwa na watanzania kuwekeza katika hisa ambapo umechangia kukuza uwekezaji ambao hauna athari za mfumuko wa bei. Moja ya faida kubwa ya kuwekeza katika masoko ya hisa ni kupata mapato halisi (real return) ambayo hayana madhara ya mfumuko wa bei (inflation). Pia moja ya malengo ya uwekezaji katika hisa ni kupata gawio linalotakana na faida iliyotengenezwa na kampuni husika ambayo mwekezaji humiliki hisa. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 kampuni sita (6) ikiwemo DSE yenyewe, zilitoa gawio yenye thamani ya shilingi bilioni **34.16** kwa wanahisa **26,684.** Huu ni wastani wa gawio/pato la shilingi 1,200,000 kwa kila mwana hisa.

### 2.7.2 Uhamasishaji wa Kukuza Masoko ya Mitaji na Dhamana

Serikali imetekeleza mikakati ya utoaji wa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa juu ya masoko ya mitaji na masoko ya bidhaa, ikiwa ni pamoja na kutoa machapisho magazetini; kutoa matangazo kwenye vyombo vya habari; kutengeneza na kusambaza shajara na vipeperushi na kuendesha semina kwa makundi mbalimbali ya kijamii. Jumla ya akaunti mpya za CDS 435 zilifunguliwa katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, Maonesho ya Kitaifa ya Kilimo, na Maonesho ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji. Tathmini iliainisha mchanganuo kuwa CDS 210 zilifunguliwa wakati wa maonesho sabasaba, 183 kipindi cha maonesho ya nanenane na 42 wakati wa maonesho ya mifuko na programu za uwezeshaji. Aidha, akunti za CDS 158 zilikuwa ni hisa, 46 hatifungani, na 189 za uwekezaji wa pamoja (Collective Investment Scheme) inayosimamiwa ma UTT-AMIS. Aidha, wawekezaji sita (6) walifanikiwa kusahihisha taarifa zao kwa kubadilisha nambari za simu na akaunti za benki.

**2.7.3 Mpango wa Hatifungani wa Benki ya Taifa ya Biashara**

Mpango wa Hatifungani wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) wenye lengo la kutoa hatifungani zenye thamani ya shilingi billioni 300 utakaotolewa kwa matoleo sita. Katika toleo la kwanza lililojulikana kama "Twiga Bond" lenye thamani ya shillingi billioni 30, ambapo NBC ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shillingi bilioni 38.9 sawa na asilimia 130. Toleo la kwanza la hatifungani ya NBC liliorodheshwa katika soko la hisa la DSE ili kuwapatia fursa wawekezaji kuuza hatifungani zao pale wanapohitaji fedha kwa ajili ya matumizi mengine; kujua thamani halisi ya hatifungani zao na kuwapatia fursa wawekezaji wapya kununua hatifungani hizo, ambapo wawekazaji hao hupata riba kama faida itokanayo na uwekezaji huo.

**2.7.4 Hatifungani ya Sukuk iliyotolewa na Benki ya KCB**

Hatifungani ya Sukuk iliyotolewa na Benki ya KCB iliyofahamika kama Fursa Sukuk yenye thamani ya shillingi bilioni 10 ambapo KCB ilifanikiwa kukusanya shillingi billioni 11.04 sawa na asilimia 110. Hatifungani ya Fursa Sukuk liliorodheshwa katika soko la hisa la DSE mnamo tarehe 13 Januari 2023 na imekuwa bidhaa ya kwanza yenye kuzingatia misingi ya Sharia kuorodheshwa kwenye soko la hisa la DSE. Aidha, Hatifungani ya Sukuk iliyotolewa na Imaan Finance yenye thamani ya shillingi bilioni 5 ilifanikiwa kukusanya shillingi billioni **11** sawa na na asilimia **220**. Fedha zilizopatikana zinatumika kugharamia biashara ndogo na za kati zinazokidhi matakwa ya Sharia. Sanjari na hayo, hatifungani ya Sukuk pia iliyotolewa na Benki ya Amana yenye thamani ya shillingi **bilioni 5** ilifanikiwa kukusanya shillingi billioni **6.75** sawa na asilimia **135**.

**2.7.5 Mauzo ya Toleo la Mpango wa Hatifungani**

Katika mwaka 2022/23, mauzo ya toleo la nne la Mpango wa Hatifungani kwa ajili ya kuendeleza Sekta ya Nyumba na Makazi iliyotolewa na Kampuni ya *Tanzania Mortgage Refinance* wenye thamani ya shilling **bilioni 120**. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 10 kiliweza kukusanywa katika toleo hili kwa ajili ya kuendeleza sekta ya nyumba na makazi.

**2.7.6 Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja unaoitwa Faida Fund**

Serikali kupitia Taasisi ya Watumishi Housing Investments *(WHI) imeendelea kuhimiza wananchi kuwekeza kwenye masoko ya mitaji na dhamana.* Mauzo ya awali ya Mfuko huo yaliwezesha kupatikana kiasi cha shilingi bilioni 12.95, ikiwa ni mafanikio ya asilimia 173. Mfuko huo unatoa fursa ya kuwekeza kwa kuanzia shilingi 10,000 hivyo kuwezesha waananchi ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake, makundi maalum kuwekeza katika masoko ya fedha; kujenga utamaduni wa kuweka akiba; na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi.

**2.7.7 Mauzo ya Hatifungani**

Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 yaliongezeka kwa asilimia 2.4 na kufikia shilingi trilioni 3.30, ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.22 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni, 2022. Aidha, mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia

Juni, 2023 yaliongezeka kwa asilimia 19.6 na kufikia shilingi milioni 981.93 ikilinganishwa na shilingi milioni 821.04 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Juni, 2022. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

**2.7.8 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 ulikuwa mzuri. Thamani ya uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 56.79 na kufikia shilingi trilioni 1.52 katika kipindi kilichoishia Juni, 2023 kutoka shilingi bilioni 971.68 katika kipindi kilichoishia Juni, 2022. Aidha, Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ambayo ni Umoja Fund, Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatigungani imeendelea kukua katika muktadha wa tahamani. **Jedwali Na.39** linaonesha mchanganuo wa thamani ya kila mfuko ulivyoanza hadi kufikia 30 Juni, 2023. Matokeo ya tathmini ya utekelezaji yanaonesha mifuko ya uwekezaji ilikuwa na thamani ya shilingi 120,148 milioni na kwa mwaka 2022/23 thamani ya mifuko ya uwekezaji imefikia shilingi 5,296,536 milioni huku mfuko wa ukwasi ukiongoza kwa kuwa na thamani ya shilingi milioni 2,522,486 na kufuatiwa na Mifuko ya Hatifungani yenye thamani ya shilingi milioni 1,403,711 na Umoja Fund wenye thamani ya shilingi milioni 1,228,206. Jumla ya kiasi cha shilingi milioni 20,170 kilitolea kama gawio ambapo Mfuko wa Hatifungani ulitoa gawio la shilingi milioni 19,154 na Mfuko wa Jikimu ulitoa gawio la shilingi milioni 1,016. Hadi kufikia Juni, 2023 Mifuko ya Uwekezaji ilikuwa na jumla ya wawekezaji 249,055 ambapo wanaume walikuwa ni 126,540 sawa na asilimia 51 na wanawake ni 122,515 sawa na asilimia 49.

**Jedwali Na. 39:** Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja na Idadi ya Wawekezaji

| Jina la Mfuko | Thamani ya Mfuko ulipoanzishwa (kwenye mil) | Thamani ya Mfuko hadi 30/06/2023 (kwenye mil) | Gawio hadi 30/06/2023 (kwenye mil) | Idadi ya Wawekezaji | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Me | Ke | Jumla |
| Umoja Fund | 117,656 | 1,228,206 | - | 70,848 | 68,829 | **139,677** |
| Wekeza Maisha (Invest Life) | 460 | 29,648 | - | 7,468 | 4,668 | **12,136** |
| Mfuko wa Watoto (Watoto Fund) | 720 | 35,266 | - | 8,564 | 9,158 | **17,722** |
| Mfuko wa Jikimu (Jikimu Fund) | 719 | 77,219 | 1,016 | 4,996 | 5,383 | **10,379** |

| Jina la Mfuko | Thamani ya Mfuko ulipoanzishwa (kwenye mil) | Thamani ya Mfuko hadi 30/06/2023 (kwenye mil) | Gawio hadi 30/06/2023 (kwenye mil) | Idadi ya Wawekezaji | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Me | Ke | Jumla |
| Mfukowa Ukwasi (Liquid Fund) | 593 | 2,522,486 | - | 24,250 | 24,390 | **48,640** |
| Mfuko wa Hati Fungani (Bond Fund) | - | 1,403,711 | 19,154 | 10,414 | 10,087 | **20,501** |
| **Jumla** | **120,148** | **5,296,536** | **20,170** | **126,540** | **22,515** | **249,055** |

***Chanzo***: *UTT AMIS, 2023*

### 2.7.9 Mchango wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Kampuni ya UTT AMIS imekuwa na mafanikio chanya katika uchangiaji wa mapato ya Serikali kupitia kodi kupitia uwekezaji unaofanywa katika ununuzi wa hisa. **Jedwali Na. 40** linaonesha mchango wa Kampuni ya UTT AMIS katika kulipa kodi tangu mwaka 2006 mpaka Juni, 2023 ambapo jumla ya kiasi cha shilingi bilioni **32.66** kililipwa kama kodi.

**Jedwali Na. 40:** Mchango wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

| Mwaka | Umoja Fund | Wekeza Maisha Fund | Watoto Fund | Jikimu Fund | Liquid Fund | Bond Fund | UTT/UTT AMIS | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | (000) | (000) | (000) | (000) | (000) | (000) | (000) | (000) |
| 2006 | 257,380 | - | - | - | - | - | 181,105 | 438,485 |
| 2007 | 823,854 | - | - | - | - | - | 243,936 | 1,067,790 |
| 2008 | 640,899 | 4,915 | - | - | - | - | 252,787 | 898,601 |
| 2009 | 611,814 | 8,100 | 5,814 | 5,952 | - | - | 276,772 | 908,452 |
| 2010 | 590,794 | 11,579 | 8,438 | 15,739 | - | - | 345,897 | 972,447 |
| 2011 | 717,632 | 14,986 | 8,250 | 35,779 | - | - | 307,544 | 1,084,191 |
| 2012 | 638,901 | 12,277 | 9,577 | 51,467 | - | - | 353,888 | 1,066,110 |
| 2013 | 888,552 | 24,685 | 12,175 | 55,443 | - | - | 645,622 | 1,626,477 |
| 2014 | 2,324,779 | 23,249 | 14,227 | 88,468 | 10,182 | - | 1,505,280 | 3,966,185 |
| 2015 | 1,328,370 | 20,453 | 17,339 | 116,872 | 5,161 | - | 1,076,983 | 2,565,178 |
| 2016 | 1,152,940 | 33,669 | 23,897 | 203,103 | 13,351 | - | 862,279 | 2,289,239 |
| 2017 | 869,793 | 28,890 | 27,341 | 173,462 | 82,889 | - | 929,515 | 2,111,890 |
| 2018 | 904,732 | 16,988 | 23,295 | 94,333 | 96,337 | - | 782,386 | 1,918,071 |
| 2019 | 132,784 | 1,232 | 3,820 | 24,849 | 38,709 | - | 723,845 | 925,239 |
| **2020** | 218,687 | 1,212 | 2,691 | 8,988 | 15,975 | 9,969 | 1,259,765 | 1,517,287 |
| **2021** | 362,403 | 2,690 | 2,573 | 9,239 | 56,045 | 30,632 | 1,124,468 | 1,588,050 |
| **2022** | 292,609 | 3,202 | 4,336 | 14,667 | 324,895 | 117,578 | 2,491,498 | 3,248,785 |
| **2023** | 320,218 | 4,520 | 5,271 | 14,746 | 329,428 | 243,403 | 3,550,478 | 4,468,064 |
| **Jumla** | **13,077,141** | **212,647** | **169,044** | **913,107** | **972,972** | **401,582** | **16,914,048** | **32,660,541** |

***Chanzo:*** *UTT AMIS, 2023*

### 2.7.10 Uchangiaji wa Mapato ya Serikali Kupitia Gawio

Uwekezaji wa Taasisi ya UTT AMIS imekuwa na mwenendo wa utendaji zuri ambao umechangia kulipa gawio (dividend) Serikalini. Jumla ya gawio lililolipwa na UTT AMIS kuanzia mwaka 2018 mpaka Juni, 2022 ni shilingi bilioni **3.00**. **Jedwal Na.41** linaonesha mwenendo wa UTT AMIS katika uchangiaji mapato ya Serikali kupitia gawio (dividend).

**Jedwali Na. 41:** Uchangiaji wa Mapato kutoka UTT AMIS

| Mwaka | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiasi Tzs (000)** | 500,000 | 550,000 | 550,000 | 600,000 | 800,000 | 3,000,000 |

***Chanzo:*** *UTT AMIS, 2023*

### 2.7.11 Mafanikio, Changamoto na Mikakati katika Uwekezaji wa Masoko ya Mitaji na Dhamana

Serikali imetekeleza jitihada mbalimbali ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika uwekezaji wa masoko ya mitaji na dhamana. Kutokana na jitihada hizo, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Kuongezeka kwa mchango wa Mifuko ya Uwekezaji ya pamoja kutoka milioni 438 mwaka 2006 hadi bilioni 32 Juni, 2023;

(b) Uchangiaji wa mapato ya Serikali kutoka UTT AMIS umeongezeka kutoka shilingi milioni 500 mwaka 2018 hadi kufikia shilingi bilioni 3 Juni, 2023; na

(c) Kuanzishwa kwa Umoja Fund, Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto, Mfuko wa Jikimu, Mfuko wa Ukwasi na Mfuko wa Hatigungani ambayo inachochea uwekezaji katika mitaji na ununuzi wa hisa.

Pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa masoko ya mitaji na ununuzi wa hisa, bado kuna changamoto zinakwamisha ushiriki wa wananchi kwenye masoko ya mitaji na dhamana kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 42.**

**Jedwali Na. 42:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Uwekezaji katika Masoko ya Mitaji na Ununuzi wa Hisa

| *Changamoto* | *Mikakati ya Kutatua Changamoto* |
|---|---|
| *(i) Kumekuwa na upungufu wa ushiriki wa wanunuzi wakuu wakiwemo mifuko ya hifadhi ya jamii kutokana na maboresho yaliyofanyika katika mifuko ya hifadhi ya jamii baada ya kuunganishwa mifuko ya jamii ya LAPF, GEPF, PPF, PSPF) na kuwa mmoja (PSSSF) iliyokuwa ikihudumia sekta ya umma.* | *(i) Kuhamasisha wanunuzi wakuu kushiriki kwenye masoko ya mitaji kwa lengo la kuongeza idadi ya wanunuzi wa ndani wa hisa na hivyo kuleta uwiano kati ya ugavi na mahitaji ya dhamana na kuogeza ukwasi katika Soko la Hisa.* |
| *(ii) Uelewa mdogo juu ya fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji na ununuzi wa hisa pamoja na Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.* | *(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji na dhamana.* |
| *(iii) Kufunguliwa kwa soko la mitaji la Afrika Mashariki kumeanza kuleta changamoto za ushindani na mabadiliko ya bei za bidhaa za fedha kwenye soko.* | *(iii) Kuanzisha mfuko wa "private equity fund" ambao utasaidia juhudi za Serikali katika uanzishaji wa viwanda na kutoa huduma za uwekezaji kwa watu na kampuni mbalimbali (private wealth management).* |
| *(iv) Ukuaji mdogo wa soko la mitaji kutokana na kubadilika mara kwa mara wa bei za hisa katika soko la hisa.* | |

## 2.8 MASOKO

Masoko ni maeneo maalumu ya kimkakati au yasiyo ya kimkakati yanayowakutanisha wauzaji ambao kwa kiasi kikubwa ni wazalishaji na wanunuzi ndani nan je ya nchi. Nchini Tanzania, moja ya masoko ya kimkakati ni Soko la Kibaigwa lililoko mkoani Dodoma. Masoko ni mchakato wa kupata bidhaa au huduma au mawazo, mahali, wakati, na bei sahihi, kwa kutumia mbinu za kukuza na kutumia watu wanaofaa kutoa huduma ya wateja inayohusishwa na bidhaa hizo, huduma, au mawazo. Dhana ya masoko ni matumizi ya data ya masoko kwa kuzingatia mahitaji na matakwa ya wateja ili kuendeleza mikakati ya masoko ambayo si tu kukidhi mahitaji ya wateja lakini pia kukamilisha malengo. Masoko yamekuwa na mchango mkubwa wa kutoa fursa kwa wananchi, kampuni na nchi kwa ujumla kufikia malengo. Masoko ya kimataifa yanaweza kuleta mabadiliko kwenye uwekezaji wa mtaji na kuuelekeza kwa maeneo ya masoko.

### 2.8.1 Masoko ya Mazao Ndani na Nje ya Nchi

Serikali kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imepewa mamlaka ya kufanya biashara katika masoko ya ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu. Ili kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinapata soko kubwa, Bodi imejikita katika kuongeza thamani kwenye bidhaa kwa kuzingatia ubora, usafi wa hali ya juu pamoja na kutumia teknolojia za kisasa kwenye viwanda katika kuzalisha bidhaa zake. Hadi kufikia Juni, 2023 Serikali imewezesha kupatikana kwa fursa za masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwemo soko la korosho katika nchi ya Marekani ambapo tani 74.19 za korosho zenye thamani ya Dola za Marekani 455,729.95 zilibanguliwa na kuuzwa na jumla ya tani 62 za zao la tumbaku zilipata soko nchini Japan. Masoko hayo yametokana na ushiriki wa Serikali na Sekta binafsi katika makongamano, maonesho ya kibiashara na uwekezaji katika nchi mbalimbali ikiwemo Japan, Umoja wa Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Ujerumani, India, Qatar na Italia kwa lengo la kutangaza bidhaa na maeneo ya uwekezaji. Masoko mengine yaliyopatikana na masoko ya zao la mahindi na mchele kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.43**.

**Jedwali Na. 43:** Mwenendo wa Mauzo ya Mazao ya Nafaka Nje ya Nchi 2022/23

| Mauzo ya Nje (Tani) | | | | Thamani (USD) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Zao** | **2020** | **2021** | **2022** | **2020** | **2021** | **2022** |
| Mahindi | 73,232 | 223,495 | 415,105 | 20,359,786 | 57,097,279 | 71,543,641 |
| Mchele | 222,145 | 475,744 | 352,735 | 91,396,150 | 223,269,815 | 181,012,052 |
| **Jumla** | **297,397** | **701,260** | **769,862** | **111,757,956** | **280,369,115** | **252,557,715** |

***Chanzo****: Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2022*

### 2.8.2 Masoko ya Mazao ya Ndani

Katika kuimarisha soko la ndani, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (National Food Reserve Agency – NFRA) imenunua mahindi tani 17,257.85 na mtama tani 1,036.46 kutoka kwenye vikundi 35 vya wakulima, vituo vikuu pamoja na vituo vya muda katika kanda zake. Aidha, Bodi ya Nafaka na

Mazao Mchanganyiko (Cereal and Other Produce Board – CPB) imenunua mahindi tani 34,484, alizeti tani 2,776, mafuta ghafi tani 85.82, mchele tani 1,797, ngano tani 277, maharage tani 406, mtama tani 3,035.06, maharage ya soya tani 393, maharage ya njano tani 30, korosho ghafi tani 523 na mpunga tani 7,065 kutoka kwa wakulima.

Mwaka wa fedha 2022/23, Soko la Bidhaa Tanzania ilihuisha miongozo ya mauzo ya bidhaa za ufuta, korosho, kahawa, na kakao kulingana na mazingira na changamoto zinazojitokeza ili kuboresha taratibu za Soko la Bidhaa Tanzania. Hadi Juni, 2023 wanunuzi waliosajiliwa kushiriki kununua bidhaa mbalimbali kupitia Soko la Bidhaa Tanzania walifikia 126 kutoka wanunuzi 93 katika mwaka 2021/22. Aidha, jumla ya tani 953,621.65 za kakao, ufuta na kahawa zenye thamani ya shilingi bilioni 115.2 ziliuzwa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania mwaka 2022/23 ikilinganishwa na tani 14,683.06 za ufuta, choroko na kakao zenye thamani ya shilingi bilioni 24.7 zilizouzwa mwaka 2021/22 kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.44**.

**Jedwali Na. 44:** Ununuzi wa Bidhaa kupitia Soko la Bidhaa Tanzania

| Mwaka | 2021/22 | | 2022/23 | |
|---|---|---|---|---|
| Wanunuzi Waliosajiliwa | 93 | | 126 | |
| **Tani za Mazao Zilizonunuliwa** | | | | |
| **Zao** | **Tani** | **Thamani "billion"** | **Tani** | **Thamani "billion"** |
| Kakao, ufuta na kahawa | Hazitumiki | | 953,621.65 | 115.2 |
| Ufuta, choroko na kakao | 14,683.06 | 24.7 | Hazitumiki | |

***Chanzo**: Wizara ya Kilimo, 2023*

### 2.8.3 Masoko ya Madini

Serikali kupitia Wizara ya Madini imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kukuza masoko ya madini kwa kuanzisha masoko na vituo vya ununuzi wa madini. Uanzishwaji huo ni kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura ya 123 ya mwaka 2010 iliyorekebishwa mwaka 2017 na kuanza rasmi Mwezi Machi, 2019. Masoko na vituo hivyo vimetoa fursa kwa wachimbaji wadogo kupata nguvu ya soko, kurahisisha uuzaji wa madini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya masoko 42 na vituo 86 vilianzishwa ikilinganishwa na masoko 40 na vituo 70 mwaka 2021/22. Jumla ya tani 18.7 zenye thamani ya shillingi trilioni 2.2 ziliuzwa ikilinganishwa na tani 18.3 zenye thamani ya shillingi trilioni 2.2 zilizouzwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, karati 23,913.2 za madini ya almasi zenye thamani ya shillingi bilioni 12.37 ziliuzwa ikilinganishwa na karati 17,858.7 zenye thamani ya shillingi bilioni 5.9 mwaka wa fedha 2021/22. Katika mwaka 2022/23, mapato ya masoko na vituo yaliyotokana na mrabaha yalikuwa shilingi bilioni 138.3, ada ya ukaguzi shilingi bilioni 22.7 na tozo ya huduma shilingi bilioni 6.9 ikilinganishwa na mrabaha shilingi bilioni 132.2, ada ya ukaguzi shilingi bilioni 22.2 na tozo ya huduma shilingi bilioni 6.6 kwa mwaka 2021/22 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.45**.

**Jedwali Na. 45:** Mauzo ya Madini kwa mwaka 2022/23

| Mwaka | 2021/22 | | 2022/23 | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina** | **Masoko** | **Vituo** | **Masoko** | **Vituo** |
| Idadi | 40 | 70 | 42 | 86 |
| | | | | |
| **Karati za Madini Zilizonunuliwa** | | | | |
| **Aina ya Madini** | **Karati** | **Thamani "billioni"** | **Karati** | **Thamani "billioni"** |
| Almasi | 17,858.7 | 5.9 | 23,913.2 | 12.37 |
| | | | | |
| **Mapato Yaliyopatikana** | | | | |
| | **Thamani "billioni"** | | **Thamani "billioni"** | |
| Mrabaha | 132.2 | | 138.3 | |
| Ada ya ukaguzi | 22.2 | | 22.7 | |
| Tozo za huduma | 6.6 | | 6.9 | |

***Chanzo**: Wizara ya Madini, 2023*

### 2.8.4 Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

Serikali imeendelea kutekeleza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ulianzishwa nchini Tanzania mnamo mwaka 2000 chini ya Sheria Na. 10 ya 2005 na kutekelezwa kwa kanuni za mfumo za mwaka 2006. Mfumo huu unatoa fursa kwa wakulima wadogo na wakati wakiwa kwenye ushirika au vikundi vya wakulima kupata nguvu ya soko na kuingia katika soko la ushindani. Mfumo huu unasaidia kuzuia upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi dhaifu kwa kuhifadhi mazao ili kusubiri kuuza wakati muafaka na pia kuongezea bidhaa thamani kabla ya kuziuza.

Serikali ya Tanzania kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na wadau wa sekta binafsi ikiwa ni pamoja na asasi za fedha, waendesha maghala, viwanda vya kusindika mazao, makampuni ya kusimamia dhamana, mfuko wa Mazao Duniani (Common Fund for Commodities - CFC) pamoja na Bodi za mazao iliendelea kuimarisha mifumo ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo ikiwemo soko la bidhaa, stakabadhi za ghala, minada na kilimo cha mkataba. Katika mwaka 2022/23, mazao ya kahawa, ufuta, mbaazi, korosho na kakao yaliuzwa kwa bei iliyowanufaisha wakulima kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

### 2.8.5 Masoko Tengefu

Serikali chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suruhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuhakikisha wananchi hususan wa hali ya chini na wafanyabiashara wadogo (Machinga) wanashiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi kwa kujenga, kukarabati na kuongeza ukubwa wa masoko tengefu nchi ili kukuza uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla. Mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2022/23 jumla ya shilling billion 5.09 zilitengwa kwa ajili ya kujenga, kukarabati na kuongeza ukubwa wa masoko tengefu yaliyowezesha

wananchi 9,400 kupata maeneo ya kufanyia biashara katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Songwe, Dodoma, Arusha, Mwanza, Morogoro na Tanga kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.46**.

**Jedwali Na. 46:** Masoko Tengefu

| Na. | Mkoa | Mamlaka | Kiasi "Million" | Maelezo | Hatua ya Utekelezaji | Idadi ya Wajasiriamali |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dar es Salaam | Jiji | 263.13 | Ujenzi wa soko la Kigogo Fresh. | Limekamilika na linatumika | 430 |
| | | Manispaa ya Ubungo | 398.50 | Soko la wajasiriamali simu 2000 na Mabibo Gamit. | Limekamilika na linatumika | 276 |
| | | | | Soko la wajasiriamali Mbezi Luis. | Limekamilika na na linatumika | 50 |
| | | | | Soko la wajasiriamali Mbezi njia ya Goba. | Limekamilika na linatumika | 84 |
| | | Manispaa ya Temeke | 441.95 | Kupauwa soko la Buza | Limekamilika na linatumika | 154 |
| | | | | Ujenzi wa soko la TAZARA | Limekamilika na linatumika | 622 |
| | | | | Ujenzi wa miundombinu ya soko la Mbande, Mabanda Matatu katika soko la TAZARA | Umekamilika na inatumika | 400 |
| | | Manispaa ya Kinondoni | 441.99 | Ujenzi wa Soko la Bunju B | Limekamilika na linatumika | 1500 |
| 2. | Mbeya | Jiji | 540.97 | Ujenzi wa Soko la Airport ya zamani | Limekamilika na linatumika | |
| 3. | Songwe | Tunduma | 383.00 | Ujenzi wa Soko Tunduma | Limekamilika na linatumika | 1500 |
| 4. | Dodoma | Jiji | 500.00 | Ujenzi wa soko la wazi la Machinga | Limekamilika na linatumika | 3000 |
| 5. | Arusha | Jiji | 500.00 | Bado kupata eneo la ujenzi | Ujenzi bado kuanza | Haitumiki |
| 6. | Mwanza | Jiji | 500.00 | Ujenzi wa soko la Mchafukoge | Limekamilika na linatumika | 754 |
| 7. | Morogoro | Manipaa ya Morogoro | 490.21 | Ujenzi wa soko – FIRE | Limekamilika na linatumika | 200 |
| 8. | Tanga | Jiji | 540.34 | Ujenzi wa jengo la Wamachinga Kange | Limekamilika na linatumika | 430 |
| | **Jumla** | | **5,000.09** | **Hazitumiki** | | **9,400** |

***Chanzo**: OR-TAMISEMI, 2023*

**2.8.6 Soko la Pamoja**

Serikali kupitia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ni hatua ya pili ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Maeneo ya msingi yanayotekelezwa katika Itifaki hiyo ni pamoja na soko huru la bidhaa; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kutoka na kuingia ndani ya Jumuiya; uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kupata ajira ndani ya Jumuiya; uhuru wa kufanya biashara ya huduma; uhuru wa kuwekeza mitaji; haki ya raia wa Afrika Mashariki kuanzisha na kuendesha shughuli za kiuchumi na biashara ndani ya Jumuiya; na haki ya ukaazi kwa raia wa Afrika Mashariki.

Mwezi Julai, 2022, Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walikuwa na Mkutano Maalum wa Kilele kuhusu utekelezaji wa Soko la Pamoja *(The High-Level Summit Retreat on the EAC Common Market*). Mkutano huo ulipokea taarifa na kujadili mafanikio, fursa, na changamoto katika miaka 11 ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Mkutano uliazimia namna ya kuongeza kasi ya utekelezaji kwa ajili ya ustawi wa Nchi na wananchi wa Afrika Mashariki. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika Mkutano huo ni pamoja na: kuchochea biashara ili kuongeza kiwango cha biashara miongoni mwa nchi wanachama; kuongeza uzalishaji na kiwango cha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya; na kuwezesha uhamishaji wa matumizi ya bima za afya za umma ndani ya nchi wanachama.

**2.8.7 Maonesho ya Nanenane na Maonesho ya Sabasaba**

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara imeendelea kukuza masoko ya bidhaa na mazao kupitia Maonesho ya Wakulima Nanenane na Maonesho ya Sabasaba. Maonesho ya Nanenane huazimishwa kila mwaka kwa lengo la kuwatambua na kuwaenzi wadau wakuu wa sekta ya kilimo wakiwemo wakulima, wafugaji, wavuvi, wanaushirika, wasindikaji na wanunuzi wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa mchango mkubwa mnaoutoa ukizingatia ukweli kwamba, Sekta hizo ndizo zinazotoa ajira kwa zaidi ya asilimia 65.6 ya wananchi wa Tanzania. Kwa mwaka 2022/23 Maonesho ya Nanenane yalihudhuriwa na waoneshaji wapatao 470 na watanzania takribani 500,000 walipata fursa ya kujifunza teknolojia mbalimbali za kilimo, mifugo na uvuvi, usindikaji wa mazao, huduma za fedha. Maonesho hayo yanawaunganisha wadau mbalimbali na masoko ndani na nje ya nchi ikiwemo upatikanaji wa taarifa sahihi za upatikanaji wa bidhaa na huduma. Maonesho ya Nanenane yalihudhuriwa na mabalozi kutoka nchi mbalimbali na wageni kutoka nchi zinazozunguka Tanzania ikiwemo Zambia, Malawi na Msumbuji ambao hufikia kuangalia fursa za uwekezaji kupitia wadau mbalimbali wanaoshiriki Maonesho ya Nanenane Kitaifa.

Mamlaka imefanikiwa kuratibu Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (47th DITF) yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni hadi 13 Julai, 2023. Maonesho ya Sabasaba yalikuwa jukwaa mahususi la kutangaza na kuimarisha biashara katika soko la ndani na nje. Maonesho yalikuwa na jumla ya washiriki 3,500 ikiwemo kampuni za ndani 3,233 na kampuni za nje ya nchi 267 kutoka nchi 19 wakionesha na kunadi bidhaa na huduma kwa sekta na tasnia mbalimbali. Ajira

za kazi za muda **11,687** zilipatikana katika maeneo ya utoaji huduma mbalimbali zikiwemo usafirishaji (pikipiki, bajaji, daladala, taxi, uber, bolt), usafi, ukarabati, mapambo, migahawa, usadizi katika mabanda ya maonesho na burudani. Kutokana na maonesho hayo, mauzo ya papo kwa papo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 3.51** yalifanyika yakichangiwa zaidi na wafanyabiashara wakati na wadogo. Aidha, miadi yenye thamani ya **Shilingi bilioni 12.28** za Kitanzania kwa mauzo ya ndani (Domestic Order) na **Shilingi bilioni 8.61** kwa mauzo ya nje ilipatikana.

### 2.8.8 Ushiriki wa Kampuni za Tanzania katika Makongamano

Serikali imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika makongamano yanayofanyika ndani na nje ya nchi kwa lengo la kukuza masoko ya biashara. Katika uratibu huo jumla ya Wafanyabiashara **205** wa Tanzania walishiriki Kongamano la Biashara nchini Malawi na Sudani Kusini yaliyofanyika tarehe 26 hadi 28 Aprili, 2023 nchini Malawi na tarehe 22-23 Machi, 2023 Nchini Sudani Kusini kwa lengo la kuwezesha kampuni shiriki kupata fursa za masoko na ushirikiano kibiashara na kampuni za nje. Kupata ushiriki huo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kampuni kutangaza bishaa, huduma na kufanya mauzo ya papo kwa papo ya Shilingi milioni 234.5 na miadi ya mauzo yenye thamani ya Shilingi bilioni 28.684 na uwekezaji wa thamani ya shilingi bilioni 7.254. Mafanikio haya, yanawezesha kampuni kuwa na uwezo wa kuendelea kutoa ajira na kipato kwa wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma zinazo endelea kuzalishwa.

### 2.8.9 Kuimarisha Ushindani wa Kibiashara

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali kupitia TanTrade imeratibu programu 21 za mafunzo kwa washiriki 1,890 ambao ni wafanyabiashara wa kawaida na wazalishaji kundi la MSM'Es. Uwezeshaji ulilenga katika kujenga uwezo wa kiushindani katika kufikia malengo ya kibiashara kwa MSMEs kutoka maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Tanga, Dar es Salaam, Dodoma, Pwani, Morogoro, Mtwara, Lindi, Kigoma, Tunduma, Kilimanjaro, Geita, Tabora, Mwanza, Njombe, na Zanzibar. Washiriki hao waliwezeshwa kwa kuwajengewa uwezo katika nyanja za utafutaji masoko, utengenezaji bidhaa, mikakati ya masoko, ufungashaji (packaging & labelling), na rajam (branding), utunzaji wa taarifa na takwimu za kibiashara na usimamizi na uendeshaji biashara na kupatiwa ushauri na kushiriki kivitendo.

### 2.8.10 Mafanikio, Changamoto na Mikakati katika Kukuza Masoko

Kutokana na jitihada zilizofanyika katika kukuza masoko, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya masoko 42 na vituo 86 vilianzishwa ikilinganishwa na masoko 40 na vituo 70 mwaka 2021/22. Jumla ya tani 18.7 zenye thamani ya shillingi trilioni 2.2 ziliuzwa ikilinganishwa na tani 18.3 zenye thamani ya shillingi trilioni 2.2 zilizouzwa mwaka wa fedha 2021/22.

(b) Katika mwaka 2022/23, kumepatikana kwa fursa za masoko mapya ya mazao nje ya nchi ikiwemo soko la korosho katika nchi ya Marekani ambapo tani 74.19 za korosho zenye thamani ya Dola za Marekani 455,729.95 zilibanguliwa

na kuuzwa na jumla ya tani 62 za zao la tumbaku zilipata soko nchini Japan.

(c) Katika mwaka 2022/23 mazao ya kahawa, ufuta, mbaazi, korosho na kakao yaliuzwa kwa bei iliyowanufaisha wakulima kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za Serikali katika kukuza masoko ya bidhaa na mazao ya ndani na nje ya nchi, bado kuna changamoto kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.47.**

**Jedwali Na. 47:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Masoko

| Changamoto | Mikakati |
|---|---|
| *(i) Ukosefu wa ubora wa bidhaa zinazozalishwa ili kufikia viwango vya kimataifa.* | *(i) Kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma bora ili kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa.* |
| *(ii) Gharama za uzalishaji mazao na bidhaa kuwa juu pamoja na ufungashaji usiokidhi viwango hivyo kushindwa kupata soko.* | *(ii) Kuboresha miundombinu ya kiuchumi ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuwezesha ubora wa bidhaa na mazao.* |

## 2.9 USHIRIKA

Ushirika ni chimbuko la kujenga nguvu ya wananchi kuwa na sauti ya pamoja katika kufanya shughuli zza kiuchumi. Katika mazingira ya uchumi wa soko huru wanaushirika wanahitaji vyama vilivyoundwa katika umoja kwa lengo la kuunganisha nguvu za rasilimali zao katika kuendesha shughuli zao za biashara kwa ufanisi ili waweze kuhimili ushindani wa wafanyabiashara wengine katika soko. Vyama vya Ushirika pia vina mchango chanya katika kuwawezesha wananchi kiuchumi wakiwemo wakulima, wafugaji, wafanyabiashara, wenye viwanda, wachimba madini na wengineo ambao vinginevyo wasingeweza kushinda kwenye soko kama wafanyabiashara binafsi.

### 2.9.1 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika na Uanzishaji wa Benki ya Maendeleo ya Ushirika

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali iliendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika (NCB) ambayo itamilikiwa na wana ushirika wenyewe. Hadi kufikia Juni, 2023, mtaji wa Benki ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika uliongezeka hadi shilingi bilioni **5.7** sawa na asilimia **31.6** kutoka shilingi bilioni **1.8** kwa mwaka 2021/22**.** Lengo ni kufikisha mtaji wa Shilingi Bilioni **15** ili kukidhi matakwa ya kisheria ya kusajiliwa kama Benki ya Taifa ya Ushirika. Aidha, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa iliendelea na uhamasishaji wa uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi. Hadi kufikia Juni 2023, Vyama vya Ushirika 7,349 vilisajiliwa ikilinganishwa na vyama 9,741 vilisajiliwa mwaka 2021/22. Jumla ya vyama vya ushirika 2,392 havikukidhi matakwa ya Sheria ya Maendeleo ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 hali iliyochangia kufutwa na kupunguza idadi ya vyama vya ushirika.

Vyama vya ushirika vilifanikiwa kutengeneza faida ya shilingi **bilioni 17** kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi **bilioni 13** kwa mwaka 2021/22. Jitahada hizo zinatokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kuhamasisha vyama vya ushirika nchini kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika.

Aidha, Serikali ilifanikiwa kuratibu uanzishwaji wa viwanda **296** vya Korosho (5) Kahawa (143), Pamba (22), viwanda vya mchanganyiko wa mpunga, mahindi na maziwa (126) vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika ambavyo vimechangia kuzalisha ajira 1,617 ambapo ajira za kudumu ni 1,129 huku wanaume wakiwa ni 686 na wanawake ni 433 na za muda 487 ambapo wanaume ni 123 na wanawake 364. Miongoni mwa viwanda hivyo ni pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Tandahimba na Newala (TANECU) Ltd ambacho kinajihusisha na ubanguaji wa korosho. Serikali pia imeendelea kuratibu na kusimamia zoezi la ufufuaji wa viwanda vya kuchakata zao la pamba na kahawa katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita, Mara na Simiyu ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2023 jumla ya viwanda vitano (5) vilikuwa vimefufuliwa.

### 2.9.2 Mitaji ya Vyama vya Ushirika na Minada ya Mazao

Mitaji ya vyama vya ushirika iliongezeka na kufikia shilingi **trilioni 1.02** kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na shilingi **bilioni 900** kwa mwaka 2021/22. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko la wanachama kujiunga na vyama vya ushirika. Aidha, uendeshaji wa minada ya mazao ilifanyika kwa Serikali kuratibu na kusimamia uendeshwaji wa minada, masoko na mauzo ya mazao ya wakulima. Hali ya utekelezaji inaonesha mauzo ya vyama vya ushirika ya tani **1,826,850.97** za mazao mbalimbali yenye thamani ya Shilingi Trilioni **1.75** za mazao mbalimbali yaliuzwa ikilinganishwa na tani **597,298.58** zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.55 ambazo ziliuzwa katika msimu wa mwaka 2021/22.

### 2.9.3 Elimu na Mafunzo ya Ushirika

Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliendelea kuhimiza na kutoa elimu na mafunzo kwa vyama vya ushirika ili kujenga uwezo wa viongozi, watendaji, wanachama, watoa huduma, na maofisa ushirika. Lengo la elimu na mafunzo hayo ya ushirika ni kuongeza uwajibikaji, kudhibiti wizi, ubadhirifu na hujuma. Mafunzo yaliyotolewa ni kuhusu: uongozi na utawala bora; uandishi na ufungaji wa vitabu vya mahesabu; uandishi wa taarifa za kifedha; usimamizi wa majanga; ukaguzi kwenye vyama vya ushirika; na taratibu za kufanya kazi na vyama vya ushirika, maadili na uaandaji wa taarifa za utekelezaji kila robo mwaka; mifumo ya masoko na faida zake; haki na wajibu wa mwanachama; masuala ya TEHAMA; utumishi; udhibiti wa ndani; utawala wa mikopo; na taratibu za kufanya kazi na vyama vya ushirika. Elimu na mafunzo yaliyotolewa kwa washiriki 261,110 wakiwemo wanaume ni 224,751; wanawake 20,984; vijana 5,167; na walemavu 111 kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.48**.

**Jedwali Na. 48:** Idadi ya Wanufaishwa wa Elimu na Mafunzo ya Ushirika

| Walionufaika na Mafunzo | Jumla ya Idadi | Jinsi | | Vijana | Walemavu |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Me | Ke | | |
| Wanachama | 229,057 | 201,810 | 17,470 | 2,700 | 67 |
| Viongozi | 24,649 | 18,655 | 2,512 | 950 | 23 |
| Watendaji | 7,095 | 4,161 | 940 | 1,400 | 16 |
| Maofisa Ushirika | 208 | 75 | 38 | 90 | 5 |
| Watoa Huduma | 101 | 50 | 24 | 27 | 0 |
| **Jumla** | **261,110** | **224,751** | **20,984** | **5,167** | **111** |

***Chanzo:*** *Tume ya Maendeleo ya Ushirika, 2023*

### 2.9.4 Ajira katika Vyama vya Ushirika

Vyama vya ushirika vimeendelea kutoa mchango mkubwa katika ajira kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi ambapo pamoja na mambo mengine iliwezesha vyama vya ushirika kuzalisha jumla ya ajira za watendaji wa vyama vya ushirika uliongezeka na kufikia idadi ya watendaji **14,000** wakiwemo wanawake ni **5,240**, wanaume ni **8,750** na walemavu 10 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na ajira **13,000** ambapo wanawake ni **5,245,**

wanaume **7,750** na walemavu **5** kwa mwaka 2021/22. Aidha, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika iliongezeka kutoka wanachama **6,965,272** ambapo wanawake **ni 2,979,561,** wanaume **3,985,660** na wenye ulemavu **51** kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia wanachama **8,358,326** ikiwa wanawake ni **3,861,063, wanaume 4,497,200** na wenye ulemavu **63.**

**2.9.5 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Vyama vya Ushirika**
Mafanikio ya ushirika katika uwezeshaji wananchi kiuchumi katika kipindi cha mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:-

(a) Mtaji wa Benki ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika umeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 1.8 na kufikia shilingi bilioni 5.7 sawa na asilimia 31.6.

(b) Mauzo ya tani 1,826,850.97 za mazao ya vyama vya ushirika yenye thamani ya shilingi trilioni 1.75 yalifanyika ikilinganishwa na tani 597,298.58 za mazao zenye thamani ya shilingi trilioni 1.55 katika msimu wa 2021/2022.

(c) Makusanyo ya mazao yaliongezeka kwa **asilimia 67.30** kutoka tani **597,298.58** kwa msimu wa 2021/22 ikilinganishwa na tani **1,826,850.97** kwa mwaka 2022/23.

(d) Thamani ya mauzo ya mazao ya wakulima yaliongezeka kwa **asilimia 11.30** kutoka shilingi **1,552,635,769,446** za mauzo ya mazao ya wakulima msimu wa 2021/22 na kuongezeka hadi kufikia shilingi **1,752,128,795,530** kwa mwaka 2022/23. Jumla ya shilingi **1,560,131,402,133** zilipatikana baada ya makato ya kisheria kwa mwaka 2022/23.

(e) Viwanda kupitia viwanda **142** vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika ambapo vimewezesha wananchi kujipatia ajira zaidi ya **773** (ajira za kudumu **343** na ajira za muda **430**), kuuza na kuchakata mazao yao pamoja na kulipwa malipo ya pili baada ya mazao yao kuchakatwa na kuuzwa kupitia Vyama vya Ushirika.

(f) Vyama vya ushirika **4,661** vilisajiliwa na TCDC katika mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za Serikali katika kukuza masoko ya bidhaa na mazao ya ndani na nje ya nchi, bado kuna changamoto kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.49.**

**Jedwali Na. 49:** Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Vyama vya Ushirika

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu dhana ya ushirika.*<br><br>*(ii) Upungufu wa watalaam katika kuendesha viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika.*<br><br>*(iii) Kuwepo kwa makatazo ya utumiaji wa mfumo rasmi wa masoko kwa baadhi ya mazao katika mikoa. Mfano zao la ufuta ambalo linaendeshwa katika Mfumo wa Sakabadhi za Ghala kwenye mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani na Songwe. Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha ufuta unaozalishwa katika Mikoa ya Singida, Dodoma, Morogoro na Katavi unauzwa katika mfumo usiokuwa rasmi. Hali hii inasababisha mkulima kutofaidika na hatimaye na kukata tamaa na kilimo cha ufuta ukizingatia kuwa, mikoa yenye mfumo rasmi bei za ufuta kwa kilo zilikuwa kubwa.*<br><br>*(iv) Uhaba wa maghala ya kuhifadhia mazao ambao unachangia baadhi ya mazao kuhifadhiwa nje na wakati mwingine kuharibika kwa maghala kutokana na kulemewa na mzigo ikiwa ni pamoja na baadhi ya maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kuharibiwa na mvua na kusababisha baadhi ya mazao kuharibika na kupoteza ubora.*<br><br>*(v) Miundombinu ya barabara kwa baadhi ya maeneo unaathiri zoezi la ukusanyaji wa mazao kutoka kwenye Vituo vya Makusanyo ya AMCOS kwenda kwenye maghala na baadhi ya maeneo kushindwa kufikika kirahisi na watoa huduma ya usafirishaji wa mazao ya wakulima kwenda sokoni.*<br><br>*(vi) Mabadiliko ya kupanda na kushuka kwa bei za baadhi ya mazao katika soko la dunia na kuwepo kwa miongozo kinzani katika baadhi ya maeneo.* | *(i) Kuimarisha mfumo wa uhamasishaji, utoaji wa elimu na uwekaji wa mfumo rasmi wa masoko kwa mikoa ambayo haijaingia kwenye mfumo katika mazao ya ufuta, zabibu, chikichi, vitunguu maji, pareto, pamba, mihogo, maharage, choroko, dengu, mbaazi, iriki, soya, mpunga/ mchele pamoja na mazao yatokanayo na mifugo na uvuvi.*<br><br>*(ii) Kujenga maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuboresha mazingira ya ukusanyaji wa mazao kuanzia ngazi ya chini.*<br><br>*(iii) Kuhakikisha kwamba wakulima wananufaika na kilimo ikiwa ni pamoja na kulipwa fedha zao kwa wakati.* |

## 2.10 ARDHI

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004 inatambua ardhi kama rasilimali ya msingi na chombo cha kuchochea shughuli za kiuchumi katika kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Uwezeshaji pia ni mhimili wa maisha ya wananchi walio wengi hususan waishio vijijini. Mipango ya matumizi ya ardhi huwezesha jamii kufanya maamuzi na kutafsiri malengo mahususi ili kupata maendelo endelevu kwa kutumia ardhi katika kuleta maendeleo ya kaya na Taifa kwa ujumla. Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 imeweka misingi ya upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi wenye lengo la kuimarisha miliki za ardhi, kuwezesha matumizi endelevu ya rasimali zilizo juu ya ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upangaji wa matumizi ya ardhi unatoa mwongozo wa jumla wa usimamizi wa rasilimali ardhi na kuweka uhusiano mpana baina ya mifumo ya asili, ya kijamii na kiuchumi katika uzalishaji. Sera nyingine za kisekta zimeendelea kutoa msisitizo juu ya misingi ya usimamizi endelevu wa rasilimali ardhi na mazingira nazo ni:- Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997, Sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000, Sera ya Madini ya mwaka 2009, Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998, Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015, Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 na Sera ya Nishati ya mwaka 2015.

### 2.10.1 Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria

Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa hati za ardhi na mashamba ili kuwawezesha wananchi kutumia hati hizo katika kujiletea maendeleo. Katika mwaka 2022/23 jumla ya Vyeti vya Ardhi (CVL's) 67 vilitolewa, Hati za Haki Miliki za Kimila (CCRO's) 51,762 zilitolewa na Viwanja 9,078 vimepimwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kwa mwaka 2022/23 hatimiliki na nyaraka za kisheria zilizosajiliwa zilikuwa 183,072 ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 141,630 zilizosajiliwa mwaka wa fedha 2020/21, sawa na ongezeko la asilimia 29.3 kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.50**.

**Jedwali Na. 50:** Hali ya Usajili wa Hatimiliki za Ardhi na Nyaraka za Kisheria

| Hati zilizosajiliwa | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Hati za kumiliki ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334** | 41,522 | 47,948 | 57,180 | 61,527 | 83,195 |
| **Hati za Sehemu ya Jengo chini ya Sheria ya Usajili wa Hati za Sehemuya Jengo (Unit Title Act No.17/2008)** | 844 | 321 | 924 | 232 | 380 |
| **Jumla Hatimiliki** | **42,366** | **48,269** | **58,104** | **61,759** | **83,575** |

| Hati zilizosajiliwa | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Miamala na Nyaraka zilizosajiliwa** | | | | | |
| **Miamala iliyosajiliwachini ya Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura 334** | 27,716 | 15,018 | 35,477 | 39,252 | 51,413 |
| **Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura 117** | 21,807 | 26,096 | 33,938 | 36,354 | 42,112 |
| **Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika, Sura 210** | 1,817 | 3,129 | 5,698 | 4,265 | 5,972 |
| **Jumla Nyaraka za Kisheria** | **51,340** | **44,243** | **75,113** | **79,871** | **99,497** |
| **Jumla ya Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria** | **93,706** | **92,512** | **133,217** | **141,630** | **183,072** |

***Chanzo**: Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Tanzania mwaka 2022*

### 2.10.2 Upimaji na Umilikishaji Ardhi

Serikali kupitia Mamlaka ya Upangaji Miji kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa maeneo yakijumuishwa maeneo ya makazi, biashara, makazi na biashara na mashamba. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 jumla ya maeneo 43,376 yamepimwa ikiwamo makazi 35,196, biashara 1,074, makazi na biashara 2,386 na mashamba 2,590 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.51.** Takwimu zinaonesha upimaji wa maeneo ya biashara, makazi na biashara na mashamba umeongezeka kwa mwaka wa fedha 2022/23 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita 2021/22. Aidha, upimaji wa viwanja vya makazi umepungua kwa kutoka 131,084 mwaka wa fedha 2021/22 hadi 35,196 mwaka wa fedha 2022/23 sawa na viwanja 95,888.

**Jedwali Na. 51:** Hali ya Upimaji wa Maeneo

| Maeneo | 2021/2022 | 2022/23 |
|---|---|---|
| Maeneo ya makazi | 131,084 | 35,196 |
| Maeneo ya biashara | 1,004 | 1,074 |
| Maeneo Makazi na Biashara | 1,932 | 2,386 |
| Maeneo ya Mashamba | 356 | 2,590 |
| **Jumla** | 134,376 | 41,376 |

***Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, 2023*

Katika kuhakikisha wananchi wanamilikishwa ardhi pasipo vikwazo, Serikali imefanikiwa kumilikisha maeneo 41,164 kwa wananchi wakiwemo wanawake 13,957 na wanaume 27,207 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.52.** Takwimu zinaonesha kuwa, kwa mwaka wa fedha 2022/23 umiliki wa maeneo umeendelea kuongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2021/22 hususan kwa wanawake ikiwa ni juhudi za kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ilitokana na kuendelea kwa utekelezaji wa Mradi wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria.

**Jedwali Na. 52:** Umiliki wa Maeneo

| Maeneo | 2021/22 | | 2022/23 | |
|---|---|---|---|---|
| | **Me** | **Ke** | **Me** | **Ke** |
| Makazi | 20,256 | 10,716 | 22,847 | 12,271 |
| Biashara | 690 | 300 | 800 | 272 |
| Makazi na Biashara | 1,356 | 568 | 1,668 | 716 |
| Mashamba | 217 | 139 | 1,892 | 698 |
| **Jumla** | **22,519** | **11,723** | **27,207** | **13,957** |

***Chanzo**: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, 2023*

### 2.10.3 Upatikakanaji wa Ardhi ya Uwekezaji

Jitihada za kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji kuboresha mazingira ya uwekezaji ziliendelea kutekelezwa na kuwezesha Benki ya Ardhi ya Uwekezaji ambapo kumilikishwa maeneo ya uwekezaji matano (5) na kupatiwa Hati za Ardhi zenye jumla ya Hekari 78,144. Maeneo haya yanatumika kama Benki ya Ardhi na kuweza kusaidia kwa uharaka pale mwekezaji anapopatikana mwenye kukidhi vigezo vya uwekezaji. Serikali kupitia TIC imefanikiwa kuandikisha jumla ya maeneo ya ardhi viwanja 111 yenye ukubwa wa hekta 4,102.51 kutoka kwa wadau mbalimbali. Vile vile, Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi (National Land Allocation Committee) iliidhinisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji yapatayo 91. Kituo kiliandikisha *Derivative Rights* zipatazo 50 katika kipindi husika.

### 2.10.4 Mafanikio, Changamoto na Mikakati katika Ardhi

Serikali imetekeleza jitihada za kuhakikisha huduma ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Kutokana na jitihada hizo zimewezesha mafanikio yafuatayo:-

(a) Hati za Haki Miliki za Kimila (CCRO's) zilitolewa 51,762 na viwanja 9,078 vilipimwa.

(b) Jumla ya hatimiliki 76,746 zilizotolewa kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa

na hati miliki 65,441 zilizotolewa mwaka 2021/2022 na hii sawa na ongezeko la hatimiliki 11,305 katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

(c) Benki ya Ardhi ya Uwekezaji kumilikishwa maeneo ya uwekezaji matano (5) na kupatiwa Hati za Ardhi zenye jumla ya hekari 78,144. Maeneo haya yanatumika kama Benki ya Ardhi na kuweza kusaidia kwa uharaka pale mwekezaji anapopatikana mwenye kukidhi vigezo vya uwekezaji.

(d) Jumla ya maeneo ya ardhi viwanja 111 yenye ukubwa wa hekta 4,102.51 kutoka kwa wadau mbalimbali yameandikishwa na TIC.

(e) Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi (National Land Allocation Committee) iliidhinisha maeneo ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji yapatayo 91 na TIC iliandikisha Derivative Rights zipatazo 50.

Pamoja na jitihada zilizfanywa na Serikali katika kuwezesha ardhi iliyopimwa kwa wananchi na wawekezaji, bado kuna changamoto mbalimbali kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 53.**

**Jedwali Na. 53:** Changamoto na Mikakati katika Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Ukosefu wa Ardhi ya Uwekezaji. Baadhi ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji yana migogoro ya ardhi, mengine yamevamiwa na wananchi na yanahitaji fidia. Hali hii huchelewesha na kusababisha usumbufu kwa wawekezaji.* | *(i) Kutenga maeneo na kuyawasilisha TIC yakiwa tayari kwa uwekezaji na bila kuwa na mzigo mkubwa wa gharama za fidia na kodi ya pango la ardhi.* |
| *(ii) Kuwepo kwa mlolongo mrefu wa uhaulishaji wa ardhi: Ili mwekezaji aweze kupata ardhi ya uwekezaji, baada ya kukidhi vigezo vya awali kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 4 ya 1999 pamoja na Sheria ya Ardhi Na. 5 ya 1999, Utaratibu unaofuatwa ni kuhaulisha ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya jumla ndipo hatimaye ardhi hiyo hupewa mwekezaji kupitia TIC endapo mwekezaji ni mgeni. Mchakato huu wa uhaulishaji wa ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya jumla unachukua muda mrefu kati ya miaka miwili hadi mitatu (kwa wawekezaji wa nje na hata wa ndani) kiasi kwamba wawekezaji walio wengi hushindwa kuvumilia kuendelea kusubiri. Aidha, hata pale ardhi inapopatikana kumekuwa na migogoro mingi kati ya wawekezaji na wakazi wa maeneo husika. Migogoro hii imekuwa ikiwakatisha tamaa wawekezaji kuwekeza nchini.* | *(ii) Kuimarisha utaratibu wa uhawilishaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji ili kuwezesha kuchukua muda mfupi.* |
| *(iii) Wananchi kuchelewa kupata fidia ambayo imechukuliwa kwa ajili ya uwekezaji na Serikali au wawekezaji wa ndani au nje* | *(iii) Kuhakikisha wananchi wanapata fidia kabla ya uwekezaji kufanyika ili kuondoa migogoro na kuwezesha uendelevu wa uwekezaji katika eneo husika.* |


## 2.11 USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA MIRADI YA KIMKAKATI NA UWEKEZAJI

Serikali imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji (Local Content) ili kuwezesha ushiriki wa wananchi na kampuni za Kitanzania kunufaika na fursa katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya madini, mafuta na gesi, ujenzi, usafirishaji, mawasiliano, kilimo, mifugo na uvuvi, viwanda na biashara, utalii , elimu, afya, ununuzi wa umma, na fedha. Miradi ya kimkakati inayoendelea kutelekezwa nchini na Serikali ni pamoja na: Mradi wa ujenzi wa Bwawa la kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), ujenzi wa barabara, miradi ya maji, Miradi ya Umeme Vijijini, ujenzi na maboresho ya Madaraja na barabara na uwekezaji katika migodi (Madini), Nishati, Mafuta na Gesi Asilia.

### 2.11.1 Ajira kwa Watanzania

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi imeendelea kufuatilia ajira kwenye uwekezaji na miradi y akimkakati inayotekelezwa nchini. Hadi kufikia Juni, 2023, miradi ya kimkakati ilizalisha ajira 146,645 za moja kwa moja na 462,170 zisizo za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 83,254 za moja kwa moja na 361,975 zisizo za moja kwa moja zilizozalishwa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 43.2% kama inavyoonesha kwenye **Mchoro Na. 7.** Hali hiyo ilichangiwa na kuongezeka kwa miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali. Aidha, ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji uliendelea kupewa kipaumbele kwa kuzingatia ajira za wenye ujuzi wa juu, ujuzi wa kati na wasio na ujuzi. Kati ya ajira hizo, ajira zilizozalishwa kwa wanawake ni 29,299 na wanaume 117,316, na ajira 101,082 zilikuwa ni kwa vijana kati ya umri wa miaka 18 – 35 ambapo zaidi ya asilimia 78 wanafanya shughuli zenye ujuzi wa chini na asilimia 14 ni za ujuzi wa kati na asilimia 8 ujuzi wa juu. Miradi ya kimkakati ilitoa fursa kwa watu wenye ulemavu 237 kupata ajira za ujuzi wa kati na juu. Mwaka 2022/23, makandarasi wa miradi ya kimkakati waliingia mikataba na kampuni 2,827 za watanzania kwa ajili ya kandarasi (848), kazi za ushauri elekezi (83) na huduma (1,896) za chakula, ulinzi, usafiri, bima na bidhaa za ujenzi ikilinganishwa na kampuni 2,019 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 40.0.

**Mchoro Na. 7:** Mwenendo wa Ajira Katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji




***Chanzo:** PURA, EWURA, Tume ya Madini, TRC, et al, 2023*

### 2.11.2 Ununuzi wa Bidhaa na Huduma za Ndani

Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa thamani ya ziada inayotokana na uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati inabaki nchini na kunufaisha watanzania kwa kuhakikisha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa na huduma za ndani. Ununuzi wa bidhaa za kampuni za kitanzania na watoa huduma wa kitanzania uliendelea kuzingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini. Katika kipindi cha mwaka 2022/23, Serikali inatoa kipaumbele kuhakikisha kuwa manunuzi ya bidhaa na huduma za ndani na kwa bidhaa ambazo hazipo ndani manunuzi ya nje yalifanyika kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na.54**.

**Jedwali Na. 54:** Manunuzi katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji

| **Aina ya Mradi** | **Aina za bidhaa/ huduma zilizonunuliwa** | **Thamani ya manunuzi yote (TZS/USD)** | |
|---|---|---|---|
| | | **Nje ya nchi** | **Ndani ya Nchi** |
| **Shirika la Reli Tanzania (TRC)** | | | |
| Mradi wa Reli ya Kisasa (*Lot 2*) | | 107,883,511,797.45 | 259,512,097,223.2 |
| **Wakala wa Barabara nchini Tanzania (TANROADS)**<br>Miradi ya Ujenzi na Uboreshaji wa Barabara kwa Kiwango cha Lami | | | |
| Kasulu – Manyovu (68.25 Km) | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | - | 1,120,000.00 |
| Kanyani – Mvugwe (68.25 Km) | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | 218,460.00 | 10,902,400.00 |
| Mvugwe – Nduta (59.35 Km) | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | 3,597,645.00 | 15,462,504.00 |
| Nduta – Kibondo - Kabingo (62.50 Km) | saruji, mchanga nyenzo za kazi za ardhini | - | 4,054,600.00 |
| Project of Kigongo/ Busisi Bridge | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | 10,750,000,000.00 | 30,733,000,000.00 |
| Project of Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (52.3 Km) | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | - | 7,508,704.00 |
| Project of Ihumwa Dry Port – Matumbulu - Nala (60 Km) | saruji, mchanga na nyenzo za kazi za ardhini | - | 5,242,000.00 |

| **Aina ya Mradi** | **Aina za bidhaa/ huduma zilizonunuliwa** | **Thamani ya manunuzi yote (TZS/USD)** | |
|---|---|---|---|
| | | **Nje ya nchi** | **Ndani ya Nchi** |
| TARURA | Mikataba ya Ujenzi wa Barabara katika miradi 1,841 | | 705,739,991,198.28 |
| Tume ya madini | | 229,306,240.28 USD | 1,224,807,893.45 USD |
| ARA | Usaidizi wa Vifaa, Chakula, Matibabu, Magari, Vipuri, Usafiri, Vifaa vya IT, | 9,243,545.23 USD | 5,836,831.67 USD |
| EACOP | - | - | 46,763,273 USD |
| M &P Exploration | kukodisha nyumba, kukodisha ghala, usalama, kukodisha gari, matengenezo ya magari, huduma ya malipo, huduma ya matibabu, ufukizaji | - | 915,795.00 USD |
| Equinor | huduma za afya, matengenezo ya kinga ya fm200 2022-2023, na huduma zingine | 188,185 USD | 2,107,340 USD |
| Songas’ | Manunuzi ya Vifaa vya utendaji kazi, Matengenezo ya magari | 24,927.96 GBP | 2,536,574,072.35 |

| Aina ya Mradi | Aina za bidhaa/ huduma zilizonunuliwa | Thamani ya manunuzi yote (TZS/USD) | |
|---|---|---|---|
| | | Nje ya nchi | Ndani ya Nchi |
| PAN - AFRICA Energy Tanzania Limited | Vifaa vya kiufundi, mafuta na kemikali, kukodisha huduma za kiufundi na zisizo za kiufundi. | 31,568,977.00 USD | 18,679,750.00 USD |
| ARA | Usaidizi wa Vifaa, Chakula, Matibabu, Magari, Vipuri, Usafiri, Vifaa vya IT | 9,243,545.23 USD | 5,836,831.67 USD |

***Chanzo**: TANROADS, TRC, TARURA, PURA, EWURA, Tume ya madini, 2022/2023*

### 2.11.3 Urithishaji wa Ujuzi na Uhaulishaji wa Teknolojia kwa Watanzania

Serikali imeendelea kufuatilia utekelezaji wa urithishaji ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia ili kuwezesha ongezeko la ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Mafunzo ya vitendo na nadharia mahali pa kazi yameendelea kupewa kipaumbele kwa watanzania waliopo kwenye miradi na uwekezaji katika ngazi zote yaani kuanzia wenye ujuzi, ujuzi wa kati na wasio na ujuzi. **Jedwali Na.53** linaonesha idadi ya wafanyakazi waliopata mafunzo katika miradi ya kimkakati.

**Jedwali Na. 55:** Hali ya Urithishaji wa Ujuzi na Uhaulishaji wa Teknolojia kwa Watanzania

| Jina la Mradi | Wafanyakazi wa Kitanzania waliopata Mafunzo | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Wenye ujuzi | Wenye Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | Aina ya mafunzo na mahali mafunzo yalifanyika |
| **Shirika la Reli Tanzania – TRC** | | | | |
| SGR LOT 2 | 104 | 278 | 1923 | Afya na Usalama kazi, utoaji wa huduma ya kwanza |
| SGR LOT 3 | 357 | 2332 | 1338 | Usimamizi kazini, Afya na Usalama |
| SGR LOT 5 | 83 | 37 | - | Mafunzo ya Utendaji kazi |

| Jina la Mradi | Wafanyakazi wa Kitanzania waliopata Mafunzo | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Wenye ujuzi** | **Wenye Ujuzi wa Kati** | **Wasio na Ujuzi** | **Aina ya mafunzo na mahali mafunzo yalifanyika** |
| LOT1 | 5 | 6 | 16 | Afya na Usalama, SEA |
| LOT2 | 6 | 3 | 4 | Afya na Usalama, Mpango wa VVU/UKIMWI |
| LOT3 | 2 | - | - | Afya na Usalama |
| LOT4 | 3 | 2 | 1 | Afya na Usalama |
| Mradi wa Daraja la Kigongo / Busisi | 121 | 710 | 109 | Programu ya Usalama Makazini |
| Mradi wa bandari kavu Nala, Veyula – Mtumba – Ihumwa (52.3 k Km) | 8 | 8 | 1745 | *SEAP*, Mpango wa Huduma ya Kwanza na VVU/UKIMWI |
| Mradi wa Bandari kavu Ihumwa – Matumbulu - Nala (60 Km) | 10 | 139 | 135 | *SEAP*, Afya na Usalama, Uokoaji |
| Tanesco | 162 | | | Mafunzo ya Makanikia, Usimamizi mahali pa kazi na Mafunzo ya Umeme |
| Tume ya Madini | 2,824 | 2,919 | 235 | Programu za Viwadani, Mafunzo ya Uokoaji na uzimaji moto, mafunzo ya uendeshaji mitambo, mafunzo ya uongozi mahali pa kazi |
| EACOP | 2,499 | - | - | Mafunzo ya Ujuzi |
| Songas' | 229 | - | - | Mafunzo ya Utendaji ngazi ya usaidizi, mafunzo ya huduma ya kwanza |
| Equinor | 9 | - | - | Elimu ya kodi, Afya na Usalama, uokoaji |
| M & P Exploration | 23 | - | - | Mafunzo ya manunuzi na usambazaji, ujuzi na uokoaji |

| **Jina la Mradi** | **Wafanyakazi wa Kitanzania waliopata Mafunzo** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Wenye ujuzi** | **Wenye Ujuzi wa Kati** | **Wasio na Ujuzi** | **Aina ya mafunzo na mahali mafunzo yalifanyika** |
| Shell Exploration and Production Tanzania Limited | 8 | - | - | Mafunzo ya Ukaguzi wa mahesabu, mafunzo ya kudili na biashara, Usalama na Afya |

***Chanzo**: PURA, EWURA, Tume ya Madini et al, 2022/23*

Serikali imeendelea kufuatilia uhaulishaji wa teknolojia kwa watanzania ili kuweza kukuza ujuzi na kuwawezesha watanzania kutekeleza miradi ya kimkakati na kufanya uwekezaji. **Jedwali Na.56** linaonesha idadi ya watanzania 1,189 walionufaika na fursa za uhaulishaji wa teknolojia katika sekta ya uziduaji na ujenzi. Takwimu zinaonesha kuwa, kati ya wanufaika 1,189, walionufaika 1,050 ni kutoka TARURA, 124 kutoka PAET, 9 kutoka Equinor, na wanufaika 6 kutoka Maurel et Prom.

**Jedwali Na. 56:** Idadi ya Watanzania Walionufaika na Uhaulishaji wa Teknolojia

| **Na.** | **Jina la Mradi** | **Aina ya Uhamisho wa Teknolojia** | **Muda wa Uhamisho wa Teknolojia** | **Idadi ya Watanzania walionufaika** | **Gharama** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PAET | Uendeshaji wa Vifaa vya Slickline, kubuni na upatikanaji wa data ya 3D seismic na uchambuzi wa data | - | 124 | - |
| 2 | Equinor | Kufundisha kwa kiwango cha MSc katika Uhandisi wa Teknolojia ya Petroli | - | 9 | 93686.24 USD |
| 3 | Maurel et Prom | Mafunzo kwa vitendo katika Ununuzi | Miezi 2 | 6 | 3,000,000 |
| 4 | TARURA | Ujenzi wa madaraja 130 ya upinde wa mawe, Ujenzi wa barabara za mawe km 8 mkoa wa Mzanza na kilometa . 0.35 Mkoa wa Rukwa | 2022/2023 | 1,050 | Billioni 8 |
| | **Jumla** | | | **1,189** | |

***Chanzo:** PURA, EWURA, TARURA, 2023*

### 2.11.4 Huduma kwa Jamii

Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi imeendelea kuhakikisha kuwa jamii inashirikishwa katika upangaji, utekelezaji na kunufaika na uwekezaji na utekelezaji wa miradi unaofanyika nchini kupitia utekelezaji wa Programu za Huduma kwa Jamii (CSR) na ulipaji fidia. Programu ya huduma kwa jamii imeendelea kutekelewa kupitia makampuni, wakandarasi na wawekezaji wakubwa na watoa huduma waliopata kandarasi mbalimbali. Ushirikishwaji wa jamii umeendelea kuzingatiwa na kunufaisha na jamii zinazozunguka maeneo ya miradi na uwekezaji. Programu za huduma kwa jamii zimewezesha upatikanaji wa huduma bora za kijamii mfano ujenzi na uboreshaji wa miundombinu, zahanati, mashule na visima kama inavyoonesha katika **Jedwali Na.57**.

**Jedwali Na. 57:** Hali ya Huduma kwa Jamii kupitia Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji

| Jina la Mradi | Aina ya huduma Zinazotolewa kwa Jamii | Jina la Wilaya, Kijiji au Kata Iliyonufaika na Huduma hiyo | Walengwa wa Huduma Inayotolewa | Thamani ya Huduma Zinazotolewa kwa Jamii (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| **Shirika la Reli Tanzania – TRC** | | | | |
| SGR Lot 2 | Ujenzi wa madarasa, zahanati, ofisi ya Serikali ya mtaa, soko la mtaa, ukumbi wa mikutano wa wilaya, na uchimbaji wa mtaro wa kufukia mabaki ya mifugo inayohofiwa kufa kwa sumu | Wilaya ya Bahi, Chamwino Kilosa, Mpwapwa na Dodoma | Jamii | 101,496,177.09 |
| MIT Lot 3 | Upatikanaji wa maji, Mchango wa matofali (200), lori 2 za mbao kwa ajili ya Gereza la Uyui na matengenezo ya barabara ya umma (5km) | Mkoa wa Tabora | Jamii | - |

| Jina la Mradi | Aina ya huduma Zinazotolewa kwa Jamii | Jina la Wilaya, Kijiji au Kata Iliyonufaika na Huduma hiyo | Walengwa wa Huduma Inayotolewa | Thamani ya Huduma Zinazotolewa kwa Jamii (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| MDM Lot 5 | Ujenzi wa chumba cha wagonjwa mahututi (ICU jengo), na<br><br>jengo la wagonjwa wa dharura.<br><br>Hospitali ya rufaa ya Mkoa, Nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala wa Wilaya, Mabweni Sita na Kumalizia Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Matongo | Mkoa wa Simiyu | Jamii | 238,400,000 |
| **Wakala wa Barabara Tanzania – TANROAD** | | | | |
| LOT 1 | Uboreshaji wa barabara za vijiji, na ununuzi wa zana za michezo kwa wanafunzi | Wilaya za Wilaya za Kasulu na Buhingwe | Jamii | 68,000,000 |
| LOT 2 | Matengenezo ya matrekta, Kusaidia pampu ya Maji na huduma ya Crane | Wilaya ya Kasulu | Mtabila JKT | 2,000,000 |
| LOT 3 | Kuunga mkono Uchaguzi Mkuu wa Kisiasa (CCM) | - | Jamii | 200,000 |

| Jina la Mradi | Aina ya huduma Zinazotolewa kwa Jamii | Jina la Wilaya, Kijiji au Kata Iliyonufaika na Huduma hiyo | Walengwa wa Huduma Inayotolewa | Thamani ya Huduma Zinazotolewa kwa Jamii (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| LOT 4 | Ujenzi wa Hospitali na msikiti | Wilaya ya Kibondo na Kakonko | Jamii | 9,700,000 |
| Mradi wa Kigongo/ Busisi Bridge | Ujenzi wa madarasa na tanki la maji, usambazaji wa vumbi la mashine kwa wasichana wa bukumbi, vumbi la mashine kwa ajili ya ujenzi wa SDA - kanisa na ukarabati wa hospitali ya bukumbi. | Wilaya ya Misungwi | Jamii | 26,680,000 |
| Mradi wa Nala – Veyula – Mtumba – bandari kavu ya Ihumwa (52.3 Km) | Kujumlisha kozi, saruji na mchanga na kutunza barabara ya mtaa wa Kijiji cha Mundemu wilayani Dodoma | Wilaya ya Dodoma | Jamii | 29,858,000 |
| Mradi wa bandari kavu ya Ihumwa– Matumbulu – Nala (60 Km) | Mifuko ya saruji, bomba la maji na vitalu vya saruji | Wilaya ya Dodoma | Jamii | 5,215,000 |

| Jina la Mradi | Aina ya huduma Zinazotolewa kwa Jamii | Jina la Wilaya, Kijiji au Kata Iliyonufaika na Huduma hiyo | Walengwa wa Huduma Inayotolewa | Thamani ya Huduma Zinazotolewa kwa Jamii (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| JNHPP - TANESCO | Ujenzi wa Chuo cha ICT mkoa wa Kigoma ,Ujenzi wa Chuo cha Afya mkoa wa Tanga na Dodoma, Ujenzi wa chuo cha ufundi Mkoa wa Lindi | Kigoma, Tanga, Dodoma na Lindi | Jamii | 262,343,199,340.01 |

***Chanzo:*** *TRC (SGR), TANROADS, TANESCO (JNHPP) 2022/2023*

**2.11.5 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kukuza Ushiriki wa Watanzania**
Kutokana na jitihada zinzofanywa na Serikali katika kukuza ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji, mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kutekelezwa kwa Programu za Huduma kwa Jamii (CSR) na ulipaji fidia kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo miradi ya kimkakati na uwekezaji unafanyika.

(b) Uwepo wa kiwango kikubwa cha manunuzi ya bidhaa zinazozalishwa ndani na huduma za Kitanzania ambapo kwa mwaka 20222/23, manunuzi ya Dola za Marekani 5,836,831.67 yalifanyika.

(c) Kuongezerka kwa ajira za watanzania ambapo kwa mwaka 202/23, miradi ya kimkakati ilizalisha ajira 146,645 za moja kwa moja na 462,170 zisizo za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 83,254 za moja kwa moja na 361,975 zisizo za moja kwa moja zilizozalishwa mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 43.2.

Pamoja na jitihada zilizofanyika katika kukuza ushiriki wa watanzania kwenye miradi ya kimkakati na uwekezaji, bado kuna changamoto mbalimbali kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na. 58.**

**Jedwali Na. 58:** Changamoto na Mikakati ya Kukuza Ushiriki wa Watanzania

| *Changamoto* | *Mikakati* |
|---|---|
| *(i) Kutokuwepo kwa Sera na Sheria ya Taifa ya Local Content kama miongozo ya jumla kwa sekta zote ili kuwezesha ushiriki wa watanzania wenye tija kwa kampuniza ndani pamoja na ukuaji wa sekta binafsi.* | *(i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Local Content na kutunga Sheria ya Ushiriki wa Watanzania.* |
| *(ii) Kampuni za ndani bado zinakabiliwa na changamoto katika kutekeleza miradi. Changamoto hizo pamoja na mambo mengine ni ukosefu wa mitaji ikiwemo mitambo na hivyo kushindwa kutekeleza miradi yenye thamani kubwa. Takwimu zinaonesha makandarasi wa ndani wanafanya miradi mingi lakini yenye thamani ndogo kulinganisha na makandarasi wa nje wanaofanya miradi michache yenye thamani kubwa.* | *(ii) Kutenga miradi na manunuzi ya upendeleo ili kuwawezesha watanzania kushiriki kwa kuondoa masharti magumu yasiyo na tija kwenye zabuni.* |
| *(iii) Ukosefu wa ubora na kiwango kidogo cha bidhaa kinachozalishwa na kupelekea manunuzi ya nje* | *(iii) Kuhamasisha ubia ili kuwezesha kampuni za kitanzania na kigeni kutekeleza miradi mikubwa na uwekezaji.* |

## 2.12 VITUO VYA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Serikali imeendelea kuhimiza uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji kiuchumi katika ngazi za mikoa na halmashauri ili huduma za uwezeshaji ziwafikie wananchi walio wengi. Huduma hizo ni pamoja na: mitaji (mikopo nafuu, vifaa, mashine au mitambo); urasimishaji ardhi; urasimishaji biashara, huduma za msimbomilia; ujuzi katika uongezaji thamani bidhaa; ithibati ya bidhaa; vyama vya ushirika; na ukaguzi wa bidhaa. u uanzishaji wa Vituo vya Uwezeshaji unatokana na maelekezo yaliyotolewa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 katika Ibara ya 26 (k) anzishaji wa Vituo vya Uwezeshaji unatokana na maelekezo yaliyotolewa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 katika Ibara ya 26 (k) pamoja na Sheria ya Fedha ya mwaka 2022 Ibara ya 83 (3) ambayo imeelekeza kila Mamlaka ya Wilaya kuanzisha kituo kwa ajili ya kuratibu, kuhimiza, kukuza na kuwezesha biashara ndani ya eneo lake ya mamlaka.

### 2.12.1 Hali ya Uanzishaji wa Vituo vya Uwezeshaji Kiuchumi

Katika kipindi cha mwaka 2022/23 jumla ya vituo vya uwezeshaji kiuchumi vitatu vilianzishwa na kufikia vituo 20 kutoka vituo 17 mwaka 2021/22. Vituo hivyo vipo katika mikoa na halmashauri ambavyo ni Mkoa wa Shinyanga (2), Geita (1), Dodoma (7), Singida (1), Kigoma (6), Pwani (1), Morogoro (1) na Rukwa (1). Vituo vya uwezeshaji hujumuisha mahala pamoja taasisi mbalimbali zinazotoa huduma

za uendelezaji wa biashara na fedha ikiwa ni pamoja na benki, taasisi za udhibiti, mifuko na programu za uwezeshaji. Miongoni mwa taasisi hizo ni NEEC, SELF Microfinance, SIDO, AGTF, Mfuko wa Kilimo wa Pass Trust, VETA, TRA, TCCIA, Benki ya NBC, Kampuni ya GS1 Tanzania, VICOBA FETA, Chuo Kikuu Huria (OUT), watoa huduma za biashara, na TWCC. Aidha, Kituo cha kwanza cha Mfano kilianzishwa katika Mkoa wa Shinyanga katika Manispaa ya Kahama (KEEC) ambacho kilizinduliwa Novemba 18, 2018.

**2.12.2 Huduma kwa Wananchi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2022/23, vituo vimeweza kutembelewa na wananchi **9,988** ambapo wanaume ni **5,002** na wanawake 4,986 na kupata ongezeko la wateja **2,026** ikilinganishwa na mwaka 2021/22 ambapo vituo vilitembelewa na wananchi **7,962.** Hamasa bado inaendelea kutolewa ili kuwezesha wananchi walio wengi kuvitembelea ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za uwezeshaji kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza biashara. Wananchi wamekuwa wakinufaika na fursa za huduma za uwezeshaji ikiwa ni pamoja na: mitaji (mikopo nafuu, vifaa, mashine au mitambo); urasimishaji ardhi; urasimishaji biashara, huduma za msimbomilia; ujuzi katika uongezaji thamani bidhaa; ithibati ya bidhaa; vyama vya ushirika; ukaguzi wa bidhaa, na pembejeo za kilimo.

**2.12.3 Huduma za Fedha**

Vituo vya uwezeshaji vimeendelea kutoa huduma za fedha ikiwa ni pamoja na: mikopo, vifaa, mashina na mitambo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2022/23, kiasi cha mikopo chenye thamani ya **shilingi bilioni 7.64** kimetolewa kwa waombaji 1,174 ambapo wanawake walikuwa 433 na wanaume ni 689 na taasisi za kifedha 14. Taasisi zilizotoa huduma za kifedha katika vituo vya Uwezeshaji ni pamoja na SELF Microfinance, SIDO, PASS TRUST, AGTF na Benki ya NBC ambapo zilitoa huduma hizo kulingana na mahitaji ya wateja. Katika mikopo iliyotolewa, kiasi cha **Shilingi Milioni 570.6** kilitolewa kwa **Taasisi 14** za kifedha ambazo ni Monuru Micro Credit Company, Milikare Microfinance, Rupia Microcredit, Rosanya Micro Credit, Cacose Investment Ltd, Maricha Credit Company, Misana Microfinance Ltd, JM& J Microcredit Co. Ltd, Kishery Micro Credit Ltd, Jj Three Microfinance, KGR Finance, Ihacha Finance na Michael Farida Babara. Katika mgawanyo wa fedha hizo za mikopo kiasi cha **Shilingi bilioni 2.73** zilienda katika sekta ya Kilimo na kufanikisha zoezi la ununuzi wa Matrekta **51** na Power Tillers **16** zilizoenda kwa wakulima ikilinganishwa na mwaka 2021/22 ambapo matrekta sita (6) yenye thamani ya **Shilingi Milioni 300** yalitolewa kwa mkopo.

**2.12.4 Huduma za Mafunzo**

Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia Vituo vya Uwezeshaji imeendelea kutoa huduma za mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, elimu ya mifuko ya uwezeshaji, biashara, na kilimo kwa wahitaji mbalimbali. Miongoni mwa mafunzo yaliyotolewa katika kipindi cha kuanzia mwezi Juni, 2022 mpaka Juni, 2023 yanahusiana na elimu ya mifuko na program za uwezeshaji, Mama na Baba Lishe, huduma za ugani, urasimishaji biashara, utengenezaji wa sabuni, usindikaji na uongezaji thamani kwa vyakula, uandishi wa miradi, utengenezaji wa batiki, ufungashaji, masoko, mafuta ya




*Mheshimiwa Sophia Mjema aliekuwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga akikabidhi mfano wa ufunguo wa trekta wakati wa zoezi la utoaji wa mikopo ya Matrekta katika Kituo Cha Uwezeshaji cha Kahama, mikopo iliyo dhaminiwa na PASS kupitia Kampuni yake Tanzu ya PASS Leasing.*

kupaka na utengenezaji wa keki. Katika kipindi cha mwaka 2022/23 vituo vimetoa huduma za mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali **1,917** ambapo wanawake ni **1,188** na wanaume **725.**

Vituo vya uwezeshaji vimekuwa pia vikitoa huduma za elimu rasmi kupitia Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) ambapo katika mwaka 2022/23 vimeweza kudahiri wanafunzi 306 kwa ngazi za Cheti, Diploma, Shahada, *Masters* na PHD ambapo wanawake ni **95** na wanaume **211.** Aidha, kupitia elimu ya ufundi na mafunzo stadi, vituo vimeweza kuendesha kozi fupi za ufundi mitambo, udereva, umakenika, ufundi mwashi, umeme na kompyuta wanufaika **408** wakiwemo wanawake ni **120** na wanaume ni **288**.

**2.12.5 Urasimishaji wa Biashara**

Vituo vya uwezeshaji vimewezesha huduma za urasimishaji wa biashara kwa lengo la kujenga uwezo na kuwahamasisha wafanyabiashara kusajili na kurasimisha biashara. Huduma ya urasimishaji imekuwa ikitolewa kupitia Taasisi za SIDO, BRELLA, TBS, TRA, GS1 Tanzania, TCCIA, TWCC na Verdy Mark Company Limited ambazo zinapatikana katika vituo vya uwezeshaji vilivyopo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2022/23, jumla ya kampuni **206** za biashara zimeweza kurasimishwa. Aidha, vituo vya uwezeshaji vimefanikisha kuratibu uanzishaji wa viwanda vya kati vitatu ambavyo ni DEA wanaozalisha maji na maziwa ya Yorghurt, Kiwanda cha vinywaji vikali cha *Ambulance Gin Distilers na Saint Fransis* wanaozalisha Wine ambavyo vinahudumia Mikoa ya Kanda ya Ziwa na kuajiri jumla ya wafanyakazi 106 wa ajira za moja kwa moja.

### 2.12.6 Huduma za Ushauri wa Kitaalam

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, vituo vya uwezeshaji vimeendelea kutoa huduma za ushauri wa kitalaam kwa wananachi **8,622** wakiwemo wanawake **4,908** na wanaume **3,714**. Ushauri ulitolewa katika maeneo ya ushauri wa mahesabu ya kifedha; uandaaji wa taarifa za mapato na matumizi ya mwaka ili kupata kodi stahiki; urasimishaji biashara; upatikanaji wa vifungashio; usimikaji wa mashine za viwandani; utunzaji wa kumbukumbu; na elimu ya huduma za mikopo. Vituo vya uwezeshaji pia vimekuwa vikifanya ziara za kutembelea viwanda mbalimbali kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo ya usimikaji wa mitambo na uhalalishaji wa kutoa leseni za biashara. Zoezi la kutembelea viwanda limekuwa likifanywa kupitia SIDO ambapo katika mwaka wa fedha wa 2022/23 viwanda **93** vilifikiwa tofauti na mwaka wa fedha wa 2021/22 ambapo viwanda **78** vilifikiwa. Zoezi hili limekuwa na manufaa makubwa kwa Kituo cha Uwezeshaji cha Kahama kwa kuwaunganisha wafanyabiashara na fursa za leseni za biashara kwa biashara ambazo hazipo katika mfumo usio rasmi.

### 2.12.7 Mafanikio, Changamoto na Mikakati katika vituo vya Uwezeshaji

Kutokana na jitihada zilizofanyika katika uanzishaji wa vituo vya uwewzeshaji, mafanikio mbalimbali yamepatikana. Miongoni mwa mafanikio hayo ni pamoja na:-

(a) Vituo vya Uwezeshaji Kiuchumi vilifanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 2,734,814,500.00 na kuwezesha wakulima kunufaika na matrekta 51 na Power Tiller 14 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na matrekta sita (6) yenye thamani ya shilingi 300,000,000.00 yaliyotolewa katika matrekta 6 kwa mwaka 2021/22.

(b) Katika mwaka 2022/23, vituo vya uwezeshaji vimeweza vilitembelewa na wananchi 9,988 ikilinganishwa na wananchi 7,962 waliotembelea vituo mwaka 2021/22. Mwamko wa wananchi kutembelea vituo vya uwezeshaji umekuwa ukiongezeka kutokana na jitihada za uhamasishaji zinazoendelea kufanyika.

(c) Idadi ya vituo vya uwezeshaji vimeongezeka kutoka vituo 17 mwaka 2021/22 na kufikia vituo 20 kwa mwaka 2022/23.

(d) Urasimishaji biashara kupitia vituo vya uwezeshaji umeongezeka kutoka biashara 78 kwa mwaka 2021/22 hadi kufikia biashara 93 kwa mwaka 2022/23.

(e) Mwitikio wa Halmashauri za Wilaya na Mikoa kujifunza katika Kituo cha Mfano cha Kahama namna ya kuanzisha vituo vya Uwezeshaji umeongezeka ambapo katika mwaka 2022/23 Halmashauri ya Mufindi, Rukwa, Geita, Nyangware, Kilimanjaro na Dar es Salaam zilifanya ziara kwa lengo la kujifunza.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na vituo vya uwezeshaji, bado kuna changamoto zinaathiri upatikanaji wa huduma za uwezeshaji. Changamoto hizo ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 59**.

**Jedwali Na. 59:** Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Vituo vya Uwezeshaji Kiuchumi

| *Changamoto* | *Mikakati* |
|---|---|
| *(i) Mwitikio wa Halmashauri kuanzisha vituo vya Uwezeshaji bado upo chini na takwimu zinaonesha katika Halmashauri 184 ndani ya Mikoa 26 ya Tanzania, ni Halmashauri 20 tu ndizo ambazo zimeanzisha vituo vya Uwezeshaji.* | *(i) Kuongeza jitihada za kuhakikisha kila Halmashauri inakuwa na kituo kimoja cha uwezeshaj.* |
| *(ii) Ukosefu wa baadhi ya Taasisi muhimu za Uwezeshaji katika vituo.* | *(ii) Kuendelea kutumia kituo cha Kahama kama Kituo cha Mfano ili kutoa hamasa kwa Halmashauri zingine kuwa na vituo vya Uwezeshaji,* |
| *(iii) Hati za kimila za waombaji wa mikopo kutotambuliwa na taasisi za kifedha kama dhamana za mkopo* | *(iii) Kuhimiza taasisi zinazotoa huduma za uwezeshaji kushiriki katika kutoa huduma katika Vituo vya Uwezeshaji.* |

## 2.13 MAJUKWAA YA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ilianzisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kwa lengo la kukuza ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za kiuchumi. Majukwaa ya uwezeshaji wanawake yanalenga kuwaunganisha wanawake ili waweze kujadili fursa za kiuchumi na kisha wawe na fikra za kimapinduzi na kimaendeleo katika kujiletea mabadiliko ya kiuchumi.

Uanzishwaji wa majukwaa hayo pia unalenga kuwakutanisha wanawake wote katika ngazi zote za kijamii ili kujadili fursa, changamoto na jinsi ya kushirikiana katika shughuli za kiuchumi hususan biashara, kilimo, madini, ujenzi, uchukuzi, na shughuli nyingine za kijamii; kutoa fursa za kuongeza uelewa kwa wanawake kuhusu masuala ya kiuchumi na biashara; kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya kiuchumi ili kuwanufaisha na fursa za masoko na mikopo yenye masharti nafuu; na kupeana taarifa za fursa za kiuchumi, biashara, mitaji, sheria na masoko.

Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yameundwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa hadi Taifa yakiwa na mfumo wa uongozi kuanzia ngazi ya chini hadi Taifa unaorahisisha utendaji na utekelezaji wa majukumu. Kupitia majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wanawake wamekuwa wakipatiwa fursa za mikopo, mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, uongozi, urasimishaji wa biashara, usindikaji wa bidhaa, upakiaji wa bidhaa na misimbo milia.

### 2.13.1 Uzinduzi wa Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Uendeshaji Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

Serikali imeendelea na jitihada za uimarishaji wa Majukwa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kwa kuratibu maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Uendeshaji Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi. Mwongozo huo ulizinduliwa tarehe 12 Septemba, 2022 na unalenga kuimarisha na kuboresha uanzishaji, uendeshaji, usimamizi, uratibu na muundo wa Jukwaa la Uwezeshaaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi ya Taifa, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Malengo mahsusi ya mwongozo huo ni:Kuweka utaratibu wa kuunda, kuendesha na kuboresha Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi za mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa; Kuelekeza utaratibu au hatua za uanzishwaji wa Jukwaa; Kuainisha utaratibu au hatua za uanzishwaji wa jukwaa; Kuainisha majukumu ya wasimamizi wa jukwaa katika kila ngazi; na Kufafanua mfumo au muundo wa utekelezaji wa majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa Jukwaa.

### 2.13.2 Uzinduzi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi la Kitaifa

Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalumu imeratibu uzinduzi wa jukwaa la wanawake kitaifa lililofanyika tarehe 17 Mei, 2023. Katika uzinduzi huo, viongozi wa majukwaa walisisitizwa kuhakikisha fursa zilizopo zinawafikia wanawake hasa waliopo vijijini pamoja na kuweka mazingira wezeshi hali itakayowasaidia kushiriki kwenye nafasi za uongozi na shughuli za kiuchumi. Kufuatia kuzinduliwa kwa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi ya Taifa, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuratibu uanzishwaji wa majukwaa katika ngazi nyingine.

### 2.13.3 Uanzishwaji wa Majukwaa katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji

Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilianzishwa katika kipindi cha mwaka 2022/23 pamoja na mikoa 26 ya Tanzania Bara ilifanikiwa kuzindua Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi katika ngazi za mikoa. Majukwaa ya uwezeshaji wanawake ya halmashauri yaliongezeka kutoka 140 kwa mwaka 2021/22 na kufikia majukwaa 152 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 7.9 na utekelezaji wa asilimia 82.6 kwa lengo la kuanzisha majukwaa ya uwezeshaji ya halmashauri. Majukwaa ya kata yaliongezeka na kufikia 1,354 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na majukwaa 1,140 kwa mwaka 2021/22. Majukwaa ngazi ya vijiji/mitaa yalikuwa 1,859 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na majukwaa 1,776 kwa mwaka 2021/22 kama linavyoonesha katika **Jedwali Na. 60** na **Jedwali Na. 61**.

**Jedwali Na. 60:** Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Yaliyoanzishwa

| Aina ya Jukwaa | Lengo | 2021/22 | 2022/23 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi | 1 | 0 | 1 | 100 |
| Majukwaa ya Mikoa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi | 26 | 26 | 26 | 100 |
| Majukwaa ya Uwezeshaji ya Halmashauri | 184 | 140 | 152 | 82.6 |
| Majukwaa ya Kata | 3,956 | 1,149 | 1,354 | 34.2 |
| Majukwaa ya Vijiji/ Mitaa | 12,328 | 1,776 | 1,859 | 15.1 |

**Jedwali Na. 61:** Idadi ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Yaliyo Anzishwa kwa Kila Mkoa

| Na | Mikoa | Mkoa | Halmashauri | | Kata | | Mitaa/ Vijiji | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Zenye Majukwaa | Zisizo na Majukwaa | Zenye Majukwaa | Zisizo Na Majukwaa | Yenye Majukwaa | Isiyo na Majukwaa |
| 1. | Arusha | 1 | 0 | 7 | 0 | 158 | 0 | 548 |
| 2. | Iringa | 1 | 5 | 0 | 54 | 73 | 120 | 562 |
| 3. | Dar Es Saalam | 1 | 5 | 0 | 102 | 0 | 664 | 80 |
| 4. | Dodoma | 1 | 8 | 0 | 55 | 39 | 177 | 541 |
| 5. | Katavi | 1 | 5 | 0 | 10 | 17 | 214 | 51 |
| 6. | Kigoma | 1 | 6 | 2 | 147 | 128 | 234 | 482 |
| 7. | Lindi | 1 | 5 | 0 | 15 | 136 | 340 | 382 |
| 8. | Kilimanjaro | 1 | 7 | 0 | 56 | 168 | 193 | 579 |
| 9. | Mwanza | 1 | 7 | 1 | 26 | 166 | 210 | 890 |
| 10. | Mara | 1 | 9 | 0 | 5 | 173 | 0 | 700 |
| 11. | Ruvuma | 1 | 5 | 3 | 173 | 153 | 817 | 649 |
| 12. | Pwani | 1 | 9 | 0 | 132 | 0 | 716 | 198 |
| 13. | Manyara | 1 | 7 | 0 | 2 | 178 | 240 | 440 |
| 14. | Morogoro | 1 | 9 | 0 | 217 | 123 | 443 | 753 |
| 15. | Mtwara | 1 | 5 | 4 | 191 | 175 | 891 | 773 |
| 16. | Shinyanga | 1 | 6 | 0 | 99 | 31 | 415 | 181 |
| 17. | Singida | 1 | 7 | 0 | 119 | 136 | 328 | 494 |
| 18. | Tanga | 1 | 11 | 0 | 79 | 166 | 321 | 806 |
| 19. | Tabora | 1 | 8 | 0 | 207 | 113 | 460 | 0 |
| 20. | Geita | 1 | 0 | 6 | 0 | 122 | 0 | 551 |
| 21. | Mbeya | 1 | 7 | 0 | 279 | 106 | 764 | 714 |
| 22. | Kagera | 1 | 8 | 0 | 0 | 192 | 0 | 814 |
| 23. | Rukwa | 1 | 4 | 0 | 59 | 468 | 0 | 506 |
| 24. | Songwe | 1 | 4 | 1 | 0 | 94 | 0 | 387 |

| Na | Mikoa | Mkoa | Halmashauri | | Kata | | Mitaa/ Vijiji | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Zenye Majukwaa | Zisizo na Majukwaa | Zenye Majukwaa | Zisizo Na Majukwaa | Yenye Majukwaa | Isiyo na Majukwaa |
| 25. | Njombe | 1 | 0 | 6 | 8 | 100 | 312 | 463 |
| 26. | Simiyu | 1 | 6 | 0 | 133 | 0 | 0 | 571 |
| | **Jumla** | **26** | **151** | **33** | **1,354** | **2,885** | **1,859** | **14,110** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum*, 2023

### 2.13.4 Bunifu na Miradi ya Wanawake katika Mikoa

Baadhi ya miradi iliyoibuliwa katika mikoa na Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi yamewezeshwa ni pamoja na:-

(a) **Tabora:–**Miradi iliyoanzishwa ni utengenezaji wa sabuni, usindikaji wa asali, karanga na mafuta ya kupikia pamoja na mradi wa batiki ambapo wanawake zaidi ya 6,170 ndani ya Halmashauri zote za Mkoa wa Tabora wamenufaika. Jukwaa lina ekari 5 ambazo zinazolimwa alizeti na kisha kukamua mafuta kwa ajili ya biashara.

(b) **Shinyanga:–** Miradi ya Kakola Ubunifu Batiki cha Msalala na Kazi Iendelee cha Kahama Manispaa. Vikundi hivi vinatengeneza bidhaa za ubunifu kama makoti ya baridi yenye Nembo ya ‘‘Royal Tour’’ yanayotumika katika Mradi wa Dhahabu wa Bulyankulu/Buzwagwi na kwa wateja wa nje ya Shinyanga wakiwemo watalii. Mradi wa Wanawake Wachimbaji Wadogo wa Madini (Tanzania Women Miners Association - TAWOMA) na Kikundi cha Wanawake ISONDA vilivyoanzishwa katika Halmashauri ya Msalala na wanawake zaidi ya 500 wamenufaika kiuchumi. Mradi wa usindikaji wa mboga ya kiasili iitwayo ‘Nsasa’ umeanzishwa katika Halmashauri ya Ushetu ambapo wanawake na vijana wapatao 100 wananufaika. Mradi wa Mama Lishe na Baba Lishe umeanzishwa katika Manispaa ya Kahama, watu wapatao 120 wamefikiwa kwa kuwezeshwa na kupewa bidhaa kwa ajili ya kuendeleza biashara zao za migahawa. Manispaa ya Shinyanga imeboresha na kutenga masoko matatu ya Ngokolo, Ibinzamata na Soko kuu kwa ajili ya wajasiriamali wanawake na vijana zaidi ya 350 kuweza kuuza bidhaa zao. Aidha, Manisipaa ya Kahama imetenga Eneo la Bukondamoyo kwa ajili ya shughuli za uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa zaidi ya wanawake na vijana wasiopungua 200.

(c) **Dodoma:-** SACCOS ya Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Mkoa wa Dodoma iitwayo Dodoma Women Saccos (DOWOSA) imeanzishwa. SACCOS hii inahudumia wanawake zaidi ya 400.

(d) **Kilimanjaro:-** Viwanda viwili vya maziwa vya Nronga na Kalali katika Wilaya ya Hai vimeanzishwa. Kiwanda cha wanawake wajasiriamali cha Kutengeneza vyungu katika Halmashauri ya Mwanga kimeanzishwa pamoja na miradi ya vikundi vya kutengeneza batiki.

(e) **Mwanza:- J**ukwaa la wanawake mkoa limeanzisha SACCOS iitwayo Mwanza Jukwaa SACCOS na wanawake zaidi ya 400 wananufaika.

(f) **Pwani:-** Jukwaa limeanzisha Kampuni ya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za mazao inayoitwa "Go Mama PLC LTD". Kampuni imesajiliwa rasmi na Msajili wa Kampuni (BRELA).

(g) **Mbeya:-** Miradi ya Vikundi vya kutengeneza Batiki, Ufumaji wa Vikapu, Sabuni na unga vimeanzishwa. Bidhaa hizo zimetangazwa na kuuzwa kupitia makongamano ya kibiashara.

**2.13.5 Mafanikio, Changamoto na Mikakati ya Kuimarisha Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi**

Uanzishwaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi umewezesha mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

Kuongezeka kwa idadi ya majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoka 3,091 mwaka 2021/22 hadi 3,391 mwka 2022/23;

(a) Kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Jukwaa ngazi ya Mkoa kwenye mikoa mbalimbali ili kutoa dira ya mikakati ya Mkoa katika kuwa kwamua wanawake kiuchumi. Mikoa ya Shinyanga, Songea na Pwani imefanikiwa kuzindua Mpango Kazi wa Jukwaa Mkoa kwa mwaka 2023-25;

(b) Kuanzishwa kwa Kampuni ya Usafi ya Wanawake katika Halmashauri ya Ushetu chini ya Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi la Mkoa wa Shinyanga. Kampuni hii imesajiliwa na Msajili wa Kampuni hapa nchini (BRELA);

(c) Uendelezaji wa soko la Ngokolo (Shinyanga) kwa kuboresha miundombinu kwa ajili ya wajasiriamali wanawake na vijana kuweza kuuza bidhaa zao;

(d) Kutenga nafasi za biashara kwa ajili ya wajasiriamali wanawake 250 katika maeneo 11 ya Stendi za mabasi, sokoni, minada na maeneo ya machinga mkoani Njombe;

(e) Kuandikisha kwa majukwaa 12 mkoani Dar es Salaam yajulikanayo kama JUWADU mahali pakazi kwa ajili ya masuala ya uwezeshaji wanawake kiuchumi;

(f) Kuratibu usajili wa Vikundi 17 vya Wanawake Wakandarasi wanaofanya kazi na TANROADS na TARURA mkoani Songwe; na

(g) Kuanzishwa kwa SACCOS ya Wanawake Dodoma (Dodoma Women SACCOS) na JUKWAA LA WANAWAKE SACCOS ya jijini Mwanza ambazo zimewafikia wanachama wake zaidi ya 400 kila moja.



*Bibi Beng'i Issa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC) pamoja na uongozi wa SACCOS ya Wanawake wa Mkoa wa Dodoma (DOWOSA) katika mkutano wa pili wa DOWOSA uliofanyika Jijini Dodoma*

Licha ya mafanikio mengi yaliyopatikana kutokana na kazi kubwa inayofanywa na majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi nchini, bado kuna changmoto mbalimbali zinazokwamisha jitihada za kuwafikia wanawake wengi na kuwaunganisha na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya changamoto na mikakati kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 62**.

**Jedwali Na. 62:** Changamoto na Mikakati ya Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

| ***Changamoto*** | ***Mikakati*** |
|---|---|
| *(i) Baadhi ya Mikoa kutotoa msukumo katika uanzishaji wa Majukwaa ya uwezeshaji wananwake kiuchumi hususan ya ngazi ya kijiji na Kata.* | *(i) Kuongeza kasi ya uanzishaji wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ili kuchoichea shughuli za kiuchumi.* |
| *(ii) Ukosefu wa maeneo rasmi ya kufanyia biashara kwa wanawake wajasiriamali katika baadhi ya mikoa.* | *(ii) Kutenga maeneo wezeshi ya kufanyia biashara kwa wanawake wajasiriamali katika baadhi ya mikoa.* |
| *(iii) Uelewa mdogo wa wanawake na wadau mbalimbali kuhusu majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi na shughuli zake.* | *(iii) Kuwakutanisha wanawake wajasiriamli na watoa huduma za uwezeshaji wanawake ili kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata uelewa wa fursa mbalimbali za kiuchumi.* |

## SURA YA TATU:

## MAMBO YA KUJIFUNZA, SIMULIZI NA SHUHUDA ZA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mbali na mambo ya msingi ya kujifunza ambayo ni best practices and lessons learnt pia tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 katika kipindi cha mwaka 2022/2023 imeainisha simulizi za mafanikio ya wanufaika wa PASS TRUST kama ifuatavyo:

### 3.1 MAMBO YA MSINGI YA KUJIFUNZA NA KUFANYIWA KAZI

#### 3.1.1. Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi ni mtambuka na zenye kuhusisha wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi hivyo ipo haja ya kuwa na mfumo wa usimamizi utakaogusa sekta zote za uchumi ili kutekeleza mipango ya uwezeshaji katika sekta mbalimbali. Mfumo huo pamoja na mambo mengine utawezesha kubuni, kupanga, kuratibu na kufuatilia maamuzi mbalimbali ya uwezeshaji wa wananchi. Mfumo huo wa kidigitali wa utekelezaji utatoa mgawanyo mzuri wa kazi na ufafanuzi wa wajibu na majukumu ya wahusika wote katika ngazi mbalimbali. Serikali pia inashauriwa kuendelea kuweka mazingira yatakayozingatia kwamba, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji inatekelezwa kwa kuzingatia misingi ya ushirikishwaji wa wadau wote. Mfumo wa kielektroniki ni muhimu hususani katika kipindi hiki ambacho Serikali kupitia e-GA imeendelea kuunganisha mifumo ili iweze kusomana na kubadilishana taarifa kwa matumizi ya Serikali na Umma kwa ujumla wake. Taarifa za e-GA zinaonesha Ofisi za Taasisi za Umma 356 zimeuganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Communication Network- GovNet).

#### 3.1.2 Vituo Vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

*Vituo vya uwezeshaji vimeonesha mchango mkubwa katika kuchochea ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Kuna haja ya kuongeza wigo wa uanzishwaji na uimarishaji wa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi ikiwa sambamba na kuhakisha wadau wote muhimu wa huduma za uwezeshaji wanatoa huduma katika vituo hivi ambavyo vina matokeo chanya ya kuwafikia wananchi waishio vijijini na mijini. Vituo hivyo vina mchango mkubwa katika kuongeza wigo wa usajili na urasimishaji wa biashara ambao ni muhimu kwa maendeleo ya kodi kupitia mifumo iliyo rasmi. Vituo vya uwezeshaji kwa mwaka 2022/23 vimefikia* ***20*** *kati ya halmashauri* ***184*** *sawa na* ***asilimia 10.3*** *ya lengo la uanzishwaji wa vituo na hivyo. Kituo cha mfano cha uwezeshaji cha Kahama ambacho kimefanikiwa kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya* ***shilingi 6,265,113,500*** *kwa wajasiriamali* ***964*** *na taasisi ndogo za kifedha* ***25*** *ambazo zilipatiwa mkopo wa* ***shilingi 570,000,000****.*

### 3.2 Simulizi na Shuhuda za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Taasisi ya PASS Trust

Jitihada za uwezeshaji wananchi kiuchumi zimendelea kufanyika kupitia wadau na taasisi za utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambapo Taasisi ya Binafsi ya Kusaidia Sekta Kilimo (PASS TRUST) imekuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya kuwezesha wakulima na wajasiriamali kunufaika na fursa mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2022/2023, PASS Trust Fund imeanisha simulizi na shuhuda mbalimbali za wanufaika wake kutokana na juhudi zilizofanyika.

#### 3.2.1 Vituo Atamizi

PASS Trust ina vituo viwili atamizi (incubator) kwa ajili ya vijana ambapo kituo kimoja kipo Mkoani Morogoro katika eneo la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) kinacho shughulikia na kilimo cha mbogamboga na matunda. Kituo kingine kipo Mkoani Dodoma katika eneo la TALIRI Wilayani Kongwa kinacho jishughulisha na biashara ya unenepeshaji wa mbuzi. Lengo kuu la vituo hivi ni kumpatia kijana ujuzi, ufahamu, uzoefu na ushauri juu ya njia bora na za kisasa za ujasiriamali, uendeshaji wa kilimobiashara, utafutaji wa masoko na masuala ya kiufundi kwenye kilimo cha mbogamboga na matunda pamoja na unenepeshaji wa mbuzi. Katika vituo hivi, vijana huatamiwa kwa mwaka mmoja, ambapo wanakabidhiwa kitalu nyumba (screen house) pamoja na mtaji, chini ya usimamizi huku wanaendelea kuendesha biashara zao.




*Bw. Daniel Chongolo,Katibu Mkuu wa CCM akitembelea Kituo Atamizi cha Kilimobiashara kwa Vijana cha AIC - SUA ambacho ni Idara ya Taasisi ya PASS Trust kilichopo mkoani Morogoro*

Katika kipindi cha mwaka 2022/23, jumla ya waatamiwa **46** kati ya **80** ambao walianza kuatamiwa mwezi Oktoba, 2021 walikamilisha kipindi chao cha mwaka mmoja wa atamizi. Jumla ya waatamiwa **21** waliweza kufidia gharama za uendeshaji na waatamiwa **18** walipata ziada **(9,700 /- 6.2m /-)**. Hadi kufikia Juni 2023, jumla ya waatamiwa **32** wanaendelea na uzalishaji wa mazao ya mbogamboga na matunda katika atamizi ya Morogoro. Aidha, katika kituo atamizi cha Kongwa hakikuwa na waatamiwa kutokana na kusimamisha kupokea waatamiwa ili kupisha upanuzi wa mnyororo wa thamani katika sekta ya unenepeshaji mbuzi ikiwemo kumalizia ujengaji wa maduka ya kuuzia nyama, machinjio ya kisasa ya mbuzi na sehemu za kuchomea nyama.



*Mjasiriamali, Ezekiel John kutoka Kituo cha Ubunifu wa Kilimo Biashara (AIC-PASS) kilichopo SUA mkoani Morogoro kinachohoatamia vijana wajasiriamali katika kilimo biashara cha mbogamboga na matunda.*

### 3.2.2 Simulizi Kutoka Wanufaika wa PASS TRUST

*PASS TRUST imeendelea kutekeleza uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa vitendo na kuwezesha utoaji wa huduma za uhakika kwa wananchi wakiwemo wajasiriamali, wakulima, na wafugaji katika kuchochea ujasiriamali wa kijani kwa vijana.*

*Moja ya simulizi ya mafanikio ya vijana inaonesha namna ujasiriamali wa kijani unavyoweza kuwa suluhisho la ukosefu wa ajira kwa vijana na uharibifu wa mazingira nchini Tanzania. Geofrey Yohana ni kijana wa miaka 30 mkazi wa mkoa wa Mbeya. Kijana huyu kutoka ahitimu masomo yake hakuwahi kuajiriwa lakini alihudhuria mafunzo ya ujasiriamali ya PASS Trust ambayo yalimjengea uwezo katika usimamizi wa biashara na teknolojia ya kijani kisha alianza uwekezaji katika usindikaji wa mbolea za asili kutokana na mabaki ya mimea. Uwekezaji huo aliofanya umetoa ajira tano (5) kwa vijana wengine, kuhudumia mamia ya wakulima katika mikoa ya nyanda za juu za kusini na mbolea ya asili ya bei nafuu kwa shughuli zao za kilimo.*

***(a) Simulizi ya Mwalimu Geofrey Yohana***

*Geofrey ambaye kitaaluma ni Mwalimu, ambaye kwa sasa ni mwanzilishi na Mkurugenzi wa Eco Post, biashara ya mbolea ya kijani yenye makao yake makuu jijini Mbeya. Kampuni husindika mabaki ya mimea na samadi kuwa mbolea ya kikaboni, mbolea isiyo na kemikali kwenye udongo inayodumu na rafiki kwa mazingira kusaidia ukuaji wa mimea. Biashara hiyo inalenga kutatua changamoto za wakulima katika eneo la usimamizi wa taka za mazao, uharibifu wa udongo, na ukosefu wa ajira kwa watu ambao wanaweza kupata faida kutokana na ubunifu na kupanga mpango wa biashara kitaalamu. Geofrey huzalisha zaidi ya tani tatu za taka kila siku. Aidha, nchi inakabiliwa wimbi kubwa la ukataji miti na uchomaji wa misitu. Hii inatishia zaidi maisha ya binadamu hasa ikizingatiwa kuwa takribani asilimia 70 ya Watanzania wanapata mapato yao kutokana na kilimo, hivyo basi misitu hukatwa mara kwa mara kwa ajili ya kilimo cha mazao na shughuli za malisho kunaweza kuathiri ustahimilivu wa sekta hiyo kwa baadaye na kuathiri maisha ya watu.*



***Bw. Geofrey akiwa katika kiwanda chake cha kusindika mbolea Igawa, Mbeya akionesha kifurushi chake cha mbolea-hai tayari kwa mauzo.***

*Mafanikio ambayo Joffrey anayapata kutokana na uwekezaji katika teknolojia ya kijani kibichi unaowezeshwa na PASS Trust ambao umethibitisha kusaidia kukabiliana na athari za kiikolojia na kijamii ambazo zinaweza kurudisha somo kwa vijana wengi kufanya uvumbuzi na kutafuta kuungwa mkono na PASS Trust katika nyanja zingine nyingi za miradi ya kijani na kupata kipato cha kujikimu maisha yao. Kwasasa, kijana huyo anaweka wazi kuwa ameweza kupata mafanikio makubwa katika biashara hiyo kwani anapata faida ya zaidi ya milioni 1 kwa mauzo ya kila mwezi.*



***Bw. Geofrey akifanya kazi katika shamba lake la kijani kibichi***

*Joffrey Agribusiness Enterprise (JAB), huajiri wafanyakazi wake wa kiwanda kutoka katika jamii inayomzunguka na kuwapatia kazi za kudumu. Kwa kupewa fursa hii, wafanyakazi wengi wao wameweza kubadilisha maisha yao kutokana na ujira wanaopata. JAB enterprise inapokea malighafi yake kutokana na maganda, majivu na mabaki ya mazao mengine na samadi kutoka kwa wakusanyaji kutoka Mbeya, ambao wengi wao hawakuwa wakipata faida kutokana na takataka hizo ambazo sasa zinageuka kuwa fursa ya biashara.*

***(b) Simulizi za Bw. Kisangani***

*Udhamini wa PASS Trust kwa wakulima wa parachichi wanaofanya kazi chini ya miradi ya kijani umewanufaisha wanakijiji wa Ludewa mkoani Njombe. **Bw. Kisangani**, ambaye huzalisha parachichi huko Ludewa ni mzalishaji maarufu wa umeme na msambazaji kwa jamii zinazomzunguka.*



***Bw. Kisangani akivuna parachichi katika shamba lake***



***Bw. Kisangani akiangalia maporomoko ya maji ambako anazalisha umeme na kuhudumia vijiji jirani***

*Bw. Kisangani alinufaika na dhamana ya mikopo na elimu ya uhifadhi wa mazingira kuhusu teknolojia ya kijani chini ya mpango wa Ukuaji wa Kijani Shirikishi yaani, Inclusive Green Growth (IGG) wa PASS Trust. Dhamana ya mkopo ya asilimia 80 kutoka PASS Trust ilimsaidia Bw.Kisangani kuimarisha uwekezaji wake na kupanua fursa zaidi za ajira kwa vijana wengi na kusaidia vijiji jirani kunufaika na usambazaji wa nishati ya umeme anaoufanya. Mkulima huyo wa parachichi, Bw.Kisangani licha ya uwekezaji wake mkubwa katika mashamba ya miti na mabwawa ya uvuvi, alianzisha mradi wa umeme wa maji kwenye maporomoko ya maji asilia karibu na shamba lake. Maporomoko ya mito ambayo yalitengenezwa kusaidia shughuli za umwagiliaji kwa mazao mbalimbali, yanazalisha umeme katika shamba lake na vijiji vya jirani.*

*Bw. Kisangani anathibitisha manufaa ya elimu yake ya kulinda mazingira kwani pia anazalisha gesi ya bayogesi katika mradi huo huo. Shughuli zote hizo zinafanyika kutoka shambani mwake baada ya michakato tofautitofauti. Bw.Kisangani anatumia mabaki ya mimea kama majiani, magunzi ya mahindi na taka zingine kwa matumizi ya mbolea ya mboji kwa ajili ya uzalishaji wa kilimo. Tangu mradi huo uanze kutumika, kampuni yake ya umeme iitwayo Kisangani Smith imechangia katika kupunguza ukataji miti na kupunguza uharibifu wa rutuba ya udongo kwa kutoa chanzo mbadala cha mbolea na umeme wa maporoko ya maji. Bw. Kisangani Smith imeongeza nafasi za ajira kwa vijana za kudumu na za muda ili kusaidia shughuli mbalimbali katika shamba lake lenye ukubwa wa ekari 200. Pia anabeba jukumu muhimu katika kueneza elimu ya mazingira huku akiwajengea uwezo wakulima wengine katika kutekeleza shughuli za kilimo kwa kuzingatia kanuni za Ukuaji wa Kijani Shirikishi kama alivyoelekezwa na PASS Trust ili kuepusha shughuli hizo kuathiri mazingira ya asili.*



***Mfanyakazi wa Bw. Kisangani akifanya kazi katika shamba la parachichi huko Ludewa, Njombe***

***Bw. Kisangani*** *anakuwa mmoja wa wanufaika wengi wa PASS Trust wa udhamini wa mikopo na huduma za maendeleo ya biashara ambao mafanikio yao yanaendelea kunufaisha idadi kubwa ya watu maskini nchini kwa kuunda fursa mpya zinazowasaidia kupata mahitaji yao ya kila siku ya kujikimu. Kituo cha umeme cha Kisangani kilianzishwa na kuimarishwa kupitia udhamini wa PASS Trust ilipomuunga mkono mkulima huyo. Mradi huo sasa unahudumia zaidi ya watu 2,000 wanaoishi vijiji jirani na anaunga mkono mipango ya ulinzi wa mazingira kwa kuandaa mikutano ya wakulima na kutoa elimu ya mazingira kuhusu kilimo bora kinachoendana na mabadiliko ya hali ya hewa na mbinu za kilimo mseto kwa ajili ya rutuba ya udongo na ulinzi wa viumbe hai.*

*(c) **Simulizi Kutoka kwa Mama Mfugaji wa Kuku Bi. Magreth Sanga***

***Bi. Magreth Sanga** ni mwanamke mjasiriamali wa kilimo biashara, anayewekeza katika ufugaji wa kuku amenufaika na kuboresha biashara yake kupitia udhamini wa PASS Trust katika kupata mkopo wa mtaji wa kuongeza na kuwafuga kuku katika mabanda ya kisasa. Hii inathibitisha kuwa ufugaji wa kuku, kama ilivyo kwa biashara zingine, unahitaji mtaji wa uhakika ili kupata tija kutokana na ufugaji wa kisasa katika mabanda mazuri kwa vifaranga wenye afya bora. Simulizi hii kutoka kwa Bi. Magreth Sanga aliyenufaika na kuzitambua faida za uwekezaji imara katika sekta ya ufugaji wa kuku alipopata mkopo na kuongeza uzalishaji wa vifaranga wake na kwa tija.*



***Bi. Magreth akiwa katika banda lake la kuku***

***Bi. Magreth h**apo awali alikuwa akifuga kuku wachache kwenye mabanda ya kienyeji hali iliyofanya aendelee kupata mayai machache na uzalishaji mdogo kutokana na kuvunjika kwa mayai na hali nyingine mbaya ikiwemo kufa kwa mifugo yake. Uzalishaji wa mwanamke huyo ulizidi kuwa na tija baada ya kupata mtaji wa kutosha aliopata akidhaminiwa na taasisi ya PASS Trust ambayo ilimsaidia kupata mkopo kwa mtaji zaidi wa kuwekeza katika ufugaji wa kuku. Lengo la PASS Trust ni kusaidia wanawake na vijana zaidi kupata huduma za kifedha na maendeleo ya biashara ili kusaidia ukuaji wa biashara zao za kilimo, mifugo na uvuvi. Tofauti na makundi mengine, vijana na wanawake hunufaika kwa kipaumbele cha hadi asilimia 80 ya dhamana ya kiasi cha mkopo kilichoombwa kama usaidizi kutoka PASS Trust. Lengo ni kuhakikisha wanawake na vijana wanaondokana na umaskini na kufurahia fursa za kifedha zilizopo nchini.*

*Bi.Magreth anatoa maoni kuwa, msaada kutoka PASS Trust uliomwezesha kuongeza idadi ya kuku na kuweka mabanda yake ya kuku katika hali ya kisasa na hivyo umeboresha biashara yake na kuongeza tija na ubora wa mazao yake. "**PASS Trust ilinisaidia kupata mkopo wa fedha ambao umeleta tija zaidi, kwa sasa nakusanya zaidi ya trei 270 za mayai kila siku kutoka kwenye trei 40 nilizokuwa nikikusanya kabla ya msaada wa PASS Trust"** anasema mnuf*aika huyo.



***Mfanyakazi wa Bi. Magreth akikusanya mayai kutoka kwenye vifaa vya kisasa vya kufugia kuku***

*Bi. Magreth anaweka wazi kuwa, dhamana ya mkopo ya PASS Trust ilimsaidia kuongeza idadi ya kuku wake kutoka kuku 2,000 hadi 11,000 na mahitaji ya wafanyakazi yaliongezeka kwani kwa sasa ameajiri vijana sita wapya kusaidia huduma mbalimbali za kuku katika shamba hilo. Mbali na kuongeza idadi ya kuku, Bi. Magreth anaripoti kuwa mkopo aliopata kutokana na dhamana ya PASS Trust ulimsaidia kuboresha upatikanaji wa chakula bora na maji, pia inakuwa rahisi kusimamia huduma zingine za uendeshaji wa kuku.*

*Bi. Magreth anaishukuru PASS Trust kwa udhamini huo na anatoa wito kwa wafugaji wengine wa kuku hasa wanawake na vijana wasiogope kuchukua mikopo kwa dhamana kutoka PASS Trust ili waweze kupata faida zaidi. PASS Trust inasaidia wajasiriamali wa biashara za kilimo ambao dhamana zao hazitoshi kupata mikopo na huduma za kukuza biashara ili kusimamia biashara zao kitaalamu. Hii inafanywa kwa ushirikiano na taasisi mbalimbali za fedha na washirika wengine wa maendeleo nchini.*

***Chanzo:** PASS TRUST, 2023*

# SURA YA NNE:

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 4.1 HITIMISHO

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi (NEEC) itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004 ili kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Taarifa ya mwaka 2022/23 ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi inaonesha kuwa pamoja na jitihada zilizofanyika bado kuna changamoto ambazo zinzathiri ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Changamoto hizo ni pamoja na: ukosefu wa miundombinu wezeshi na rafiki katika maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji. Miundombinu hiyo ni barabara, maji, umeme wa uhakika, reli na bandari hivyo kupelekea uwekezaji mwingi wa miradi kujazana katika mikoa yenye miundombinu imara kama Dar es Salaam, Pwani, Arusha, na Mwanza; bidhaa zinazozalishwa ndani kushindwa kuhimili ushindani katika soko kutokana na ukosefu wa ubora; ukosefu wa umeme wa uhakika na kuathiri shughuli za uzalishaji na biashara kwa ujumla; Uelewa mdogo juu ya fursa na faida za kutumia masoko ya mitaji na ununuzi wa hisa pamoja na Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja; kiwango kidogo cha walipakodi ikilinganishwa na nguvukazi iliyopo nchini; uwepo wa idadi kubwa ya biashara ndogo zinazofanywa na wananchi katika mifumo isiyo rasmi; uwepo wa mikopo chechefu; kutokuwepo kwa Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ambayo itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi; kampuni za ndani bado zinakabiliwa na changamoto za ukosefu wa mitaji ikiwemo mitambo katika kutekeleza miradi; kuwepo kwa mlolongo mrefu wa uhaulishaji wa ardhi; na kutokuwepo kwa Sera na Sheria ya Taifa ya Local Content kama miongozo ya jumla kwa sekta zote ili kuwezesha ushiriki wa watanzania wenye tija kwa kampuniza ndani pamoja na ukuaji wa sekta binafsi.

Kutokana na matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi yana mchango mkubwa kwa Serikali kutambua jitihada zilizofanyika katika sekta mbalimbali za kiuchumi ili kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi. Tathimini hii inawezesha Serikali na wadau katika kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo ambazo zinaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi nchini. Hivyo, matokea ya taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi yana mchango mkubwa katika kuishauri Serikali namna ya kuendelea kuweka mazingira wezeshi ambayo yanalenga kuhakikisha sehemu kubwa ya uchumi unamilikiwa na watanzania wenyewe kupitia sekta binafsi na hatimaye kufanikisha malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ifikapo 2025.

## 4.2 MAPENDEKEZO YA JUMLA

Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi. Hivyo, mikakati mbalimbali inapendekezwa kutekelezwa ili

kuwezesha juhudi za masuala ya uwezeshaji kuwa na mchango na kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (TDV, 2025).

### 4.2.1 Kuimarisha Upatikanji wa Ardhi Iliyopimwa

*Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2004 inatambua ardhi kama rasilimali ya msingi na chombo cha kuchochea shughuli za kiuchumi katika kuleta maisha bora kwa kila mtanzania. Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa mwaka 2022/23 inaonesha bado kuna changamoto ya upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kupata mikopo na uwekezaji. Ili kukuza shughuli za kiuchumi na uwekezaji nchini, ni muhimu kuongeza kasi ya upimaji na utengaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji pamona na kuhakikisha wananchi wanapata fidia kabla ya uwekezaji kufanyika ili kuondoa migogoro na kuwezesha uendelevu wa uwekezaji katika eneo husika. Mipango ya matumizi ya bora ya ardhi huwezesha jamii kufanya maamuzi na kutafsiri malengo mahususi ili kupata maendelo endelevu kwa kutumia ardhi katika kuleta maendeleo ya kaya na Taifa kwa ujumla.*

### 4.2.2 Kuboresha Miundombinu ya Kiuchumi

*Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi imebaini uwepo wa changamoto ya miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na barabara, reli, umeme, mawasiliano na miundombinu ya kilimo. Hivyo, ili kukuza shuguli za uchumi na uwekezaji nchini, ni vyema kuongeza kasi ya uwekezaji katika miundombinu kama barabara, bandari, viwanja vya ndege, umeme, mawasiliano na miundombinu ya kilimo ambayo inahitaji kufanyiwa maboresho kwa ajili ya kuifanya nchi kuwa mahala salama pa uwekezaji na kuwa kituo cha biashara kwa nchi za EAC na SADC. Hatua madhubuti ni muhimu zikachukuliwa katika kujenga na kukarabati miundombinu ya kiuchumi ili kuchochea shughuli za kiuchumi hasa maeneo ya pembezoni na vijijini ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya uboreshaji wa upatikanaji wa huduma za umeme na mawasiliano.*

### 4.2.3 Kuandaa Sera na Sheria ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania

*Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa mwaka 2022/23 inaonesha ushiriki mdogo wa watanzania katika shughuli za kiuchumi. Hivyo kuandaliwa kwa Sera na Sheria ya Taifa ya Ushiriki wa Watanznaia (National Local Content Policy na Nationa Local Content Act) ili kuendana na mabadiliko katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia na kuwezesha thamani inayopatikana katika uchumi inanufaisha watanzania na Taifa kwa ujumla kupitia ajira kwa watanzania, ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani, na uhaulishaji wa teknolojia. Hatua hiyo itatoa mwongozo wa kitaifa katika utekelezaji wa dhana ya Ushiriki wa Watanzania (Local Content) katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji nchini.*

*Ili kuweza kuongeza ushiriki wa watanzania katika miradi mikubwa ya kimkakati, Serikali pamoja na mambo mengine inapendekezwa kuyafanyia kazi mikakati ifuatayo:Kuendelea kutenga miradi ya upendeleo itakayowajengea uwezo kampuni za ndani na hatimaye kunufaika na thamani kubwa ya miradi hiyo ambayo imeendelea kunufaisha kampuni ya kigeni kupata thamani kubwa licha ya uchache wa kampuni hizo ikilinganishwa na kampuni za ili kuongeza ushiriki wa kampuni*

*za ndani na hatimaye kiasi cha thamani kubwa ya ziada kubaki nchini kuendeleza ukuaji wa uchumi na uwekezaji kwa ujumla; na Kuondoa masharti magumu yasiyo na tija kwenye zabuni hususan za miradi mikubwa ili kuendeleza watoa huduma wa ndani na wazalishaji bidhaa pamoja na malighafi zinazopatikana nchini kwa lengo la kukuza ushiriki wa watanzania.*

**4.2.4 Uanzishaji wa Taasisi na Mifuko ya Uwezeshaji**
*Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ambayo pamoja na mambo mengine inaelekeza Serikali itaunda taasisi maalum na mifuko itakayoongoza uendeshaji, usimamizi na utekelezaji wake. Taaasisi ambazo zimeundwa hadi kufanikisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi ni pamoja NEEC, TADB, NIDA, REA, EPZA, UTT-AMIS, Benki ya Maendeleo ya Ushirika, n.k.*

*Hivyo, kulingana na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi inapendekezwa kuanzishwa kwa taasisi na mifuko ya uwezeshaji iliyoelekezwa ili kukuza shughuli za kiuchumi. Taasisi na mifuko ya uwezeshaji hiyo ni pamoja na:-*

**4.2.4.1 Wakala wa Dhamana ya Mikopo**
*Kutokana na changamoto ya upatikanaji wa mitaji mikubwa, Wakala wa Dhamana ya Mikopo (Tanzania Credit GuaranteeAgency) ianzishwe ili kuwawezesha wananchi kupata mitaji na dhamana kwa ajili ya miradi wanayoanzisha wao wenyewe au ile ya ubia na wageni. Taasisi hiyo itakuwa na kazi ya kutathmini miradi ya wananchi na pale inaporidhika, kutoa,dhamana ili wananchi waweze kukopeshwa na benki za ndani na za kimataifa, au kutoa mitaji kwa wananchi watakaoanzisha kampuni za ubia na wawekezaji wa nje. Taasisi hiyo haitatoa mikopo ya mojakwa moja na pale ambapo mfuko huo utakuwa umetoa dhamana, hisaza wananchi zitabakia mikononi mwa taasisi hiyo hadi hapo mkopoutakapokuwa umerejeshwa.*

**4.2.4.2 Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi**
*Ili kuwafikia wananchi wengi hasa wenye miradi midogo, Mfuko wa Uwezeshaji Mwananchi (Mwananchi Empowerment Fund) uanzishwe ili utumike katika kuwezesha wananchi kunufaika na fursa za mikopo yenye riba na masharti nafuu kupitia dhamana. Mfuko huu ni muhimu kuimarishwa kwa kuwa una wigo mpana katika uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mfuko huu pia ni vyema ukawezesha wahitimu wa vyuo wenye maandiko ya kuanzisha miradi yenye tija na manufaa katika kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na wahitimu mbalimbali nchini. Mitaji ya kuanzisha biashara ama miradi imekuwa ni changamoto kwa vijana na wahitimu wa vyuo katika kufanikisha ari ya kuajirika.*

**4.2.5 Mapitio ya Mfumo wa Elimu Unaozingatia Elimu na Ujuzi**
*Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika eneo la kuinua viwango vya ujuzi na maarifa inaelekeza mitaala ya shule inapaswa kurekebishwa ili kutoa elimu na ujuzi wa masuala mbalimbali pamoja na ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kumwezesha mhitimu kujiamini, kuwa mbunifu na kuwa na ari ya kufanya kazi kwa makini na ustadi mkubwa. Hii pia itaongeza weledi kwa wahitimu kuajirika katika*

*soko la kazi ikiwa ni pamoja na kujiajiri na kuchangia ukuaji wa maendeleo ya uchumi wa nchi. Hivyo, inapendekezwa mapitio na maboresho ya mfumo wa elimu unahitajika kuhuisha masuala ya ujasiriamali katika mitaala ili kuzalisha wahitimu wenye ujuzi na maarifa kulingana na mahitaji ya soko la ndani na kimatifa.*

*Katika kuendeleza ujasiriamali, Taasisi ya Kuendeleza Ujasiriamali (Entrepreneur Development Institute (EDI) ianzishwe ili kuongeza ujuzi kwa wananchi, hasa katika maarifa ya kiufundi, masoko na maendeleo ya biashara. Sambamba na hayo, EDI itasimamia masuala yote ya kuwawezesha wananchi kwa njia ya kuwaongezea ujuzi.*

### 4.2.6 Kuongeza Wigo wa Uwezeshaji kwa Wahitimu Kunufaika na Kodi ya Kuendeleza Ujuzi

*Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya wanafunzi kupata mikopo kwa ajili ya kuongeza ujuzi kupitia vyuo vya kati na vyuo vikuu hapa nchini. Ili kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana na wahitimu, inapendekezwa kuboresha utaratibu wa kuwezesha wahitimu kunufaika na SDL katika kuendeleza ujuzi na uzoefu mahali pa kazi, maofisini, viwandani, au kwenye miradi ya kimkakati. Uwezeshaji vijana na wahitimu kupitia SDL itawezesha mafunzo ya utarajali (internship) kuwa na matokeo chanya kwa maendeleo ya vijana wahitimu na Taifa kwa ujumla. Hatua hii itachochea kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na uzoefu wa kuajirika katika soko la ajira ambapo nguvu kazi ya vijana inahitajika.*

### 4.2.7 Uanzishwaji wa Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

*Katika kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi hasa maeneo ya pembezoni ya miji au vijijini, ni muhimu kuhakikisha kila mkoa kusimamia uanzishwaji wa vituo vya uwezeshaji kiuchumi ili kusogeza huduma kwa wananchi walio wengi kunufaika na huduma za uwezeshaji mahali pamoja na hivyo kuondoa urasimu na gharama za urasimishaji wa biashara. Mikoa pia ihakikishe vituo hivyo vinakuwa na watoa huduma mbalimbali kutoka taasisi za umma na binafsi. Hivyo, mikoa na halmashauri zinashauriwa pia kutembelea Kituo cha mfano cha Kahama cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambacho kimekuwa na matokeo chanya kufikia malengo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Hivyo, kuna umuhimu kwa watendaji na viongozi waandamizi wa mikoa na halmashauri kufanikisha uanzishaji na uimarishaji wa vituo hivi ili kuwafikia wananchi walio wengi hususan wale waishio vijijini.*

### 4.2.8 Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

*Majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ni nyenzo muhimu na jitihada za makusudi katika uwezeshaji wanawake kunufaika na fursa za kiuchumi. Hivyo, iko haja kuhakikisha mifumo ya majukwaa inaanzishwa, inasimamiwa na kuratibiwa ipasavyo kuanzia ngazi ya Kijiji hadi Taifa ili kuwezesha upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa wananwake. Mafunzo na elimu iendelee kutolewa kupitia semina, warsha, maonesho na makongamano ili kukuza uelewa wa wanawake wa kuwa na sauti ya pamoja katika utekelezaji wa shughuli za kiuchumi kuanzia ngazi ya kijiji, kata, tarafa, wilaya, mkoa hadi Taifa.*

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1:** Orodha ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji 72 Zilizopo kwa Umiliki

## A. MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI

1. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (Youth Development Fund - YDF);
2. Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (Women Development Fund - WDF)
3. Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF);
4. Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (Agricultural Inputs Trust Fund - AGITF);
5. Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund);
6. Mfuko wa Kilimo Kwanza (Kilimo Kwanza Fund - KKCF);
7. Mfuko wa Mzunguko katika Mikoa (Regional Revolving Fund - RRF);
8. Mfuko wa Usambazaji wa Maji kwa Umeme wa Jua;
9. Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Global Climate Fund – GCF);
10. Mfuko wa Maendeleo ya Michezo;
11. Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa;
12. Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wakulima Wadogo (Smallholders' Credit Guarantee Scheme - SCGS);
13. Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF);
14. Mfuko wa Kuendeleza Umeme Jadidifu Tanzania (Tanzania Energy Development and Expansion - TEDAP);
15. Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba (Housing Microfinance Fund);
16. Mfuko wa Dhamana za Mikopo kwa Wajasiriamli katika Sekta ya Kilimo (SIDO SME –CGS);
17. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund –TASAF);
18. Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund –TaFF);
19. Mpango wa kuwawezesha Wavuvi na Wakuzaji Viumbe Maji;
20. Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme);
21. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu;
22. Mpango wa kuwawezesha Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu (Asilimia 10 za Halmashauri;
23. Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali;
24. Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Serikali Kuu (Public Service Advances Fund);
25. Mfuko wa Nishati Vijijini (Rural Energy Fund –REF);
26. Bodi ya Mfuko wa Barabara;
27. Mfuko wa Kuchochea Kilimo Tanzania (Tanzania Agricultural Catalytic Trust-TACT);
28. Mfuko wa Mawasiliano kwa Umma (UCSAF);
29. Mfuko wa Elimu Tanzania (Tanzania Education Fund - TEF);

30. Mfuko wa Kuongeza Ujuzi na Stadi za Kazi (SDF);
31. Mfuko wa Fidia ya Ardhi Tanzania;
32. Mfuko wa Taifa wa Maji (National Water Fund - NWF);
33. Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania (TWPF);
34. Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund - EAMCEF);
35. Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale (The National Fund For Antiquities);
36. Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL);
37. Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF);
38. Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika;
39. Mfuko wa Taifa wa Dhamana ya Hifadhi ya Mazingira;
40. Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo;
41. Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa;
42. Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba;
43. Mfuko wa Kuendeleza Uzalishaji wa Sukari;
44. Mfuko wa Kuendeleza Zao la Korosho;
45. Mfuko wa Wafanyabiashara Ndogondogo na Watoa huduma Zisizo Rasmi (Machinga);
46. Samia Scholarship Fund;
47. Mfuko wa Utafiti na Maendeleo;
48. Mfuko wa Maendeleo ya Reli;
49. Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi;
50. Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
51. Kampuni ya UTT AMIS;
52. Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Miradi Midogo na ya Kati (SME-CGS);
53. Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi (MEF);
54. Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu;
55. Programu ya Ajira kwa Vijana kupitia Sekta ya Kilimo (Build A Better Tommorrow - BBT);
56. Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta (Fuel Price Stabilization Fund - FPSF);
57. Mfuko wa Uhamasishaji wa Matumizi ya Ethanol kama Nishati mbadala ya kupikia;
58. Mfuko wa Taifa wa Umwagiliaji;
59. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;
60. Mfuko wa Uwezeshaji wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
61. Mpango wa Kutambua na Kurasimisha Ujuzi wa vijana uliopatikana nje ya Mfumo rasmi *(Recognition of prior learning);*
62. Mpango wa kuwawezesha Vijana kushiriki katika Kilimo cha Kisasa kwa kutumia Teknolojia ya Kitalu Nyumba; na
63. Mpango wa kuwapatia vijana Mafunzo ya Kilimo nchini Israel.

## B. MIFUKO NA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI ZINAZOMILIKIWA NA SEKTA BINAFSI

1. Mfuko wa Kusaidia Sekta Binafsi ya Kilimo (Private Agricultural Sector Support Trust – PASS Trust);
2. Asasi ya Kusaidia Wajasiriamali Wadogo na Wakati (African Guarantee Fund) – NMB;
3. African Trade Insurance - NMB;
4. Kituo cha Ubunifu wa Kilimo Biashara (AIC);
5. Women Trust Fund;
6. Social Action Trust Fund;
7. Mfuko wa Kuendeleza Sekta Binafsi za Fedha Tanzania (Financial Sector Deepening Trust- FSDT);
8. Mfuko wa SMEs Impact Fund; na
9. Programu ya Kuongeza ujuzi kwa Vijana na Wanawake – Programu ya 2jiajiri (KCB)

PRIVATE AGRICULTURAL SECTOR SUPPORT

**Piga Simu Bure: 0800 75 0037**


**OFISI KUU:**

Jengo la PSSSF Commercial Complex, Ghorofa ya 5, Mtaa wa Sinza C, P.O. Box 9490 Dar-es-Salaam.

@passtrust pass trust @pass_trust pass@pass.otz pass trust wwwpass.ortz Tel: +255 (0) 22 2110 394

**OFISI ZA KANDA:**

Kanda ya Kaskazini **(Arusha)** / Kanda ya Mashariki **(Morogoro)** / Kanda ya Nyanda za Juu Kusini **(Mbeya)** / Kanda ya Magharibi **( Tabora)** / Kanda ya Kusini **( Ruvuma )** / Kanda ya Ziwa **(Mwanza)**


"Tunaboresha Maisha kupitia Mapinduzi ya Kilimobiashara"